



# MASOMO YA SHULE YA JUMAPIILI

KWA WATOTO

Nakala ya 22

# **MASOMO**

**YA SHULE YA JUMAPILI**

**KWA WATOTO**

Hati Miliki © 2020 Shirika la Uchapishaji Mnazareti Afrika  
Hati Zote Zimemilikiwa.  
ISBN 978-0-7977-1499-1

Chapa ya 2020

Kitabu hii kilichapishwa mwanzo katika lugha ya Kiingereza na Kichwa cha:

*Elementary Teacher's Guide Year 3*

Huduma ya Uanafunzi ya Jimbo la Mesoamerika

[www.SDMIresources.mesoamericaregion.org](http://www.SDMIresources.mesoamericaregion.org)

Hatimiliki © 2017

Hati zote zimehifadhiwa.

Toleo hili limechapishwa na Shirika la Uchapishaji la Mnazareti Afrika

Hatimiliki © 2020

Hati zote zimehifadhiwa.

Kimechapishwa na  
Shirika la Ushapishaji la Mnazareti Afrika

# **MPANGO WA MWAKA WA JIMBO LA AFRIKA**

## **MASOMO YA BIBLIA KWA WATOTO**

### **Nakala ya 22 Nambari ya 21**

#### **YALIYOMO**

<b>Mawazo ya Kuwafundisha Watoto</b>	5
<b>Jinsi ya Kutayarisha Masomo</b>	5
<b>Jinsi ya Kuwasilisha Masomo</b>	6
<b>Mawazo ya Zoezi la Kuwafundisha Watoto</b>	10
<b>Jinsi ya kuomba na wale wanaotafuta uso wa mungu</b>	8
<b>Kitengo cha I Masomo:</b>	9
Somo la 1: Yesu Ajifunza Kutii	10
Somo la 2: Yesu Abatizwa	13
Somo la 3: Yesu Ajaribiwa	16
Somo la 4: Yesu Achagua Wanafunzi Wake	19
<b>Kitengo cha II Masomo</b>	22
Somo la 5: Yesu Amponya Mtu Mwenye Ukoma	23
Somo la 6: Yesu Ambadilisha Mathayo	26
Somo la 7: Yesu Anawapenda Watoto	29
Somo la 8: Yesu Amsamehe Petro	32
<b>Kitengo cha III Masomo:</b>	35
Somo la 9: Yesu, Mwalimu Bora Zaidi	36
Somo la 10: Yesu, Daktari Bora Zaidi	39
Somo la 11: Yesu, Mwenye Nguvu Zaidi	42
Somo la 12: Yesu, Kiongozi Bora Zaidi	45
<b>Kitengo cha IV Masomo:</b>	48
Somo la 13: Yesu Alikufa kwa Ajili Yesu	49
Somo la 14: Yesu Alifufuka	52
Somo la 15: Yesu ni Mwokozi Wetu	55
<b>Kitengo cha V Masomo:</b>	58
Somo la 16: Sheria za Kuishi na Hekima	59
Somo la 17: Lazima Mungu Awe katika Sehemu ya Kwanza	62
Somo la 18: Kuwashemtu Wazazi Wetu	65
Somo la 19: Chunga Mawazo Yako	68
Somo la 20: Kuiba na Kudanganya Inaleta Matokeo Mabaya	71
Somo la 21: Ulafi ni Hatari	74
<b>Kitengo cha VI Masomo:</b>	77

Somo la 22: Enenda Mbele Bila Uoga	78
Somo la 23: Enenda Mbele kwa Ujasiri	81
Somo la 24: Enenda Mbele Kwa Utiifu	84
Somo la 25: Enenda Mbele kwa Nguvu za Mungu	87
Somo la 26: Enenda Mbele kwa Ahadi za Mungu	90
<b>Kitengo cha VII Masomo:</b>	93
Somo la 27: Tafuta Amani	94
Somo la 28: Tafuta Upendo	97
Somo la 29: Mtafute Mungu	100
Somo la 30: Tafuta Uhai	103
<b>Kitengo cha VIII Masomo</b>	106
Somo la 31: Habari Njema kwa Mtoashi	107
Somo la 32: Habari Njema kwa Mtu wa Roma	110
Somo la 33: Habari Njema kwa Watu wa Antokia	113
Somo la 34: Habari Njema kwa Kila Mtu wa Sehemu ya Masomo	116
<b>Kitengo cha IX Masomo</b>	119
Somo la 35: Hadithi ya Huzuni ya Kaini na Habilii	120
Somo la 36: Mtu mzuri katika ulimwengu mbaya	123
Somo la 37: Mungu Amuokoa Nuhu	126
Somo la 38: Mungu Afanya Ahadi	129
<b>Kitengo cha X Masomo</b>	132
Somo la 39: Ruthu	133
Somo la 40: Boazi	136
Somo la 41: Hana	139
Somo la 42: Samwelii	142
<b>Kitengo cha XI Masomo</b>	145
Somo la 43: Mungu Ampa Muza Misheni Maalum	146
Somo la 44: Mungu Awakomboa Watu Wake	149
Somo la 45: Mungu Awapa Watu Wake	152
Somo la 46: Mungu Awalinda Watu Wake	155
Somo la 47: Mungu Aonyesha Nguvu Zake	158
<b>Kitendo cha XII Masomo</b>	161
Somo la 48: Kipawa cha Utiifu	162
Somo la 49: Kipawa cha Wokovu	165
Somo la 50: Kipawa cha Sifa	168
Somo la 51: Kipawa cha Ibada	171

## ***Mawazo ya Kuwafundisha Watoto***

Kuna sifa mbili muhimu za kuwa mwalimu: Ni lazima upende Mungu na uwapende watoto. Jambo muhimu unalohitaji kufanya ni kuwasaidia watoto darasani mwako waone upendo wa Mungu. Unaweza kufanya hivi kwa kuonyesha mfano wa uhusiano wa maisha yako binafsi na Yesu mbele yao na kuwafundisha kuwa na uhusiano wa binafsi na Mungu. Ni lazima pia tuwafundishe watoto jinsi ya kuwatendea wengine na upendo wa Kikristo.

Unaweza kutaka kupanga mradi wa mwaka wa kutengeneza “Kitabu Chao cha Mstari wa Kukariri”. Kila wiki kuwa na makatasi yako au ya watoto ya ukubwa wa A5 au A6 ya kuandikia mstari wa kukariri wa kila wiki katika lugha ambayo wanaelewa. Weka maratasi haya pamoja ili kutengeneza kitabu.

### **JINSI YA KUTAYARISHA SOMO**

#### **Mwanzo wa Mwaka:**

Mwanzoni mwa mwaka wa kufundisha, chukua kama masaa mawili kuweka vitu vyote ambavyo kwa kawaida ungetumia katika shule ya Jumapili kwenye pakiti moja au sanduku. Hii itapunguza wakati kwa kila wiki ambao unaweza vinginevyo, kutumia kutafuta vitu tofauti, kwani utajua viko wapi.

Weka rekodi ya anwani, siku za kuzaliwa, na maelezo ya mawasiliano ya wanafunzi wote darasani mwako.

Kwa ufupi pitia kitabu chote cha masomo ili kupata wazo la sisitizo mbali mbali za mwezi. Hii itakupa muhtasari na hali ya mwelekeo. Utafahamu ni masomo ngapi yaliyomo kwa kila kichwa na kukosa kwenda mbele ya mafundisho.

#### **Masaa mawili ya Kila Wiki**

- Dakika 30** Pitia somo ili ulifahamu. Jumapili mchana, wiki nzima kabla ya kufundisha somo, chukua muda wa kujifahamisha na somo. Muombe Mungu akupe hekima na ufahamu wa njia bora ya kuwasilisha vifaa kwenye darasa lako.
- Dakika 10** Weka rekodi ya fikira na mawazo yako ya wiki. Weka kijitabu kidogo au karatasi ya shule ya Jumapili pamoja nawe. Wazo linapokujia, liandike kwenye karatasi ili ulikumbuke baadaye.
- Dakika 20** Soma kifungu cha Biblia mara 3 au 4 wakati wa wiki. Ruhusu Neno la Mungu likubadilishe unapolifikiria na kulisoma. Kusoma huku kutaruhusu ukweli unaotaka kufunza darasa lako kubalidisha maisha yako kwanza.
- Dakika 50** Leta somo lako pamoja. Kusanya kila kitu unachohitaji kutoka kwa pakiti lako la rasilimali. Pitia maandishi yako na upange somo katika mtindo unaokupendeza na ambaio utaweza kuufuata na kuuelewa vyema.
- Dakika 10** Ukaguzi wa dakika ya mwisho. Hili ni jambo la mwisho kufanya kabla ya kwenda darasani Jumapili asubuhi. Hakikisha kwamba unayo Biblia, somo lako na vifaa vingine unavyohitaji. Rejelea maandishi yako au nakala katika mwelekeo wako wa uongozi mara ya mwisho. Mwishowe, chukua dakika moja au mbili kulikabithi somo hili kwa Bwana na umuombe akutumie. Labda tayari umeomba hili mara kadhaa wakati wa ibada zako, lakini tambua utegemezi wako kwake mara nyingine.

## JINSI YA KUWASILISHA SOMO

Watoto wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kujifunza kwa kubadilishana uzoefu na hisia, kutambua ukweli, na kuchagua kitu wanachoweza kufanya kila wiki kulingana na ujumbe waliojifunza katika somo.

Muda wa somo lako unapaswa kupangwa kwa uangalifu na mpangilio ili kuweka katika matendo matayarisho na mawazo yako. Tungependa kupendekeza muhtasari wa msingi ufuatao kwa wakati wako wa darasa la shule ya Jumapili. Nyakati zilizopewa zinategemea darasa la saa. Nambari zilizo kwenye mabano ni dakika 45 za darasa.

Wasili angalau dakika kumi kabla ya darasa ili kutayarisha sehemu ya mafunzo yako na kupanga vifaa vyovytote veya masomo ambayo waweza kuhitaji.

Tumia **dakika 10 (5)** za kwanza kuwasalimu wanafunzi wako wanapofika. Anza somo kwa maombi (unaweza kutaka kuwaruhusu watoto kuchukua zamu kuomba kwa wakati huu). Wape nafasi washiriki habari yoyote ya kufurahisha na matukio ambayo yamewatokea tangu wiki iliopita. Chukua mahudhurio na upokee matoleo. Fuatilia kazi yoyote tangu wiki iliopita na kurejelea somo.

**Dakika 10 (5)** zinazofuata zitumike kutambulisha somo na kuangazia fikira za wanafunzi juu ya lengo lenyewe la somo la leo.

Somo linapaswa kuzungumziwa pamoja na wanafunzi katika **dakika 15**. Kumbuka KUTOWAHUBIRIA au KUWASOMEA. Wasilisha somo kama hadithi katika maneno yako mwenyewe.

**Dakika 20 (15)** zinazofuata zitumike kufanya shughuli na kuzungumzia vyombo veya mjadala vilivyoceanwa mwisho wa somo. Wasaidie watoto kuona jinsi kweli uliosomwa katika somo unavyotumika katika maisha yao ya kila siku.

Wakati wa **dakika 5** za mwisho, funga kwa maombi na uwaambie watoto wasaidie kusafisha eneo la darasa kabla ya kwenda kanisani. Huu ni wakati mzuri wa mwingiliano wa moja kwa moja na watoto.

Rejelea mafanikio ya somo mara unavyoweza. Kwa kumbukumbu ya baadaye, tumia dakika chache ukitengeneza mukhtasari wa kili kilitimia na kile ambacho hakikutimia.

### Wanafunzi, Tabia zao na Mwalimu

#### 1. Waelewe Wanafunzi Wako na Ruhusu Tabia ya Kawaida.

- Watoto ni hai na wadadisi.
- Sio watu wazima wadogo: lazima kila mara tutofautishe tabia mbaya na kutokomaa.

#### 2. Unda Hali Ambayo Inakuza Tabia Nzuri.

- Acha watoto wajue kuwa unawapenda na unawathamini.
- Onyesha hamu kwa yale yanayotendeka nje ya darasa.
- Jipange katika jinsi unavyoshughulikia wanafunzi.
- Toa miongozo iliyo wazi na thabiti; acha watoto wajue matarajio yako kwoo.
- Usionyeshe upendeleo.

#### 3. Tambua Nafasi Yako Kama Mwalimu.

- Kuwa msimamizi wa darasa.
- Kuwa kielelezo cha mamlaka ambayo wanafunzi wanawenza kufuata.
- Kuwa rafiki kwa wanafunzi wako.
- Waeleze kile wanachotarajia kufanya na uwape mifano mizuri.

#### **4. Tumia Njia Zinazohusisha Watoto na Kukamata Maslahi Yao.**

- Jitayarishe na ufile darasani kabla ya mtoto yeyote.
- Toa shughuli tofauti ambazo zinfaa kwa umri wa wanafunzi wako.
- Tumia shughuli ambazo zinavutia masilahi na uwezo wao.
- Ruhusu watoto wachague shughuli zingine.

#### **5. Zingatia Tabia nzuri.**

- Punguza idadi ya sheria.
- Unaposahihisha mtoto, jadili na mzazi wao, mlezi wao, au mtu anayewajibika nao.

### **UNAFANYA NINI MTOTO ANAPOKOSEA?**

#### 1. Pata Sababu ya Tatizo.

- Je! Mtoto ana shida ya kusoma au matibabu ambayo inazuia ushiriki wao darasani?
- Je! Yeye hujaribu kudhibiti darasa?
- Je! Ana talanta ya kitaaluma na kwa hivyo amechoshwa na darasa?
- Unapojuwa sababu ya shida, unaweza kusahihisha baada ya kuzungumza na wazazi wa mtoto.

#### 2. Chukua Udhhibit wa Hali hiyo.

- Puuza tabia isiyokatiza darasa
- Husisha mtoto katika shughuli za kujifunza.
- Acha aone kuwa unaangalia mwenendo wake mbaya.
- Mkaribie mtoto kwa njia ya upendo.
- Wafundishe wanafunzi matokeo ya utovu wa nidhamu.

#### 3. Ongea na Wazazi au Mtu anayewajibika kwa Mtoto.

- Kama unajua kwamba utataka hasa kuzungumza na wazazi wake au mlezi, fanya hivyo, usikawie.
- Anza kwa kuwaambia wazazi unachofurahia juu ya mtoto wao.
- Eleza tatizo na uulize maoni yao jinsi ya kutatua tatizo.

### **MAWAZO YA ZOEZI KWA KUWAFUNDISHA WATOTO**

Tia maanani kwamba watoto wa umri tofauti wana akili tofauti. Jisikie huru kuzoea tabia zao, jadili maswali na hadithi ya Biblia ili watoto waweza kuelewa unachowafunza. Tumia maarifa ya watoto wako kwa mfano, kama wanaweza kusoma, wahca wasome baadhi ya mistari kutoka kwa hadithi ya Biblia; wakusaidie kwa shughuli na kusafisha darasa.

#### *Kazi ya Mstari wa Kukariri*

Watoto wasome mistari hii ya kukariri kwa lugha wanayoifahamu ‘Lugha ya Nyumbani’. Kwa watoto wachanga unafaa muda kidogo katika mstari wa kukariri.

**Mifano** - Andika mstari wa kukariri katika karatasi (iliyopigwa chapa ama karatasi ya kuchorea n.k). Tumia kalamu kubwa ya wino, chora juu ya maneno halafu uyakate kisha uwape watoto ili waweze kuunganisha tena mstari wa kukariri.

**Futa Neno** - Kama una ubao wa chaki ama ubao mweupe, andika maneno ya mstari juu yake. Watoto wasome mstari. Kisha umwache mtoto mmoja afute neno moja. Darasa lafaa lisome huo mstari tena wakikumbuka kulitaja neno lililofutwa. Ruhusu mtoto mwengine aondoe neno lingine. Endelea kufanya zoezi hili mpaka wafute maneno yote ya mstari.

**Kuwa Neno** - Gawa neno au fungu la maneno kwa mstari wa kukariri kati ya watoto. Baada ya kurudia mstari huo mara kadha, watoto wasimame kulingana na sehemu ambayo gawanyo la mstari linafaa. Kisha watoto wasome kila neno au fungu moja baada ya fungu mpaka wakamilishe mstari.

### *Mawazo ya Zoezi*

**Udongo wa Kufinyanga** - Watoto hupenda kuwa wabunifu kwa kutumia mikono yao. Hapa kuna vichanganyo rahisi vya kutengeneza udongo wa nyumbani wa kufinyanga. Viweke ndani ya chombo kilichofunikwa ili kisitoe hewa na utadumu kwa muda mrefu. Iwapo unayo rangi ya chakula au rangi ya nguo, pengine utapenda kutengeneza udongo wa rangi tofauti ili kuifanya mradi wa watoto kuwa wa kusisimua kwao.

<p><b>Gramu 10 (Vijiko viwili ya ugaga; Gramu 250 ya kikombe kimoja cha unga;</b>  <b>Gramu 2.5 ya nusu kijiko ya chumvi</b>  <b>Gramu 15 ya kijiko kimoja cha mafuta ya kupika;</b>  <b>Robo ya lita ya maji (250)</b></p>	<p><b>Weka miseto yote pamoja ndani ya nyungu ya kupikia mpaka gundi nyororo iweze kutengenezwa. Pika pole pole juu ya moto kidogo mpaka kinyunga kitoka kando ya nyungu. Ondoa kinyunga kutoka kwa nyungu na ukande kwa dakika 3; Ongeza rangi.</b></p>
---	--

**Mchezo wa Kuigiza** - Tumia vipawa vya watoto wako vya kucheza ili mcheze hadithi yoyote ya Biblia. Watoto wabertilishane kucheza sehemu kuu.

**Daraja la Mchezo** - Tena ukitumia mchezo wa kuigiza, wacha watoto wafanye vile wangefanya wakikabiliwa na maswali ama wakiwa katika hali mbali mbali. Uliza, ‘Je, ungefanya nini kama...’ Hakikisha umewapa mwongozo wa kujadili mambo haya.

**Mwanaserere** - Kulingana na tamaduni, unaweza kutengeneza mwanaserere wa mkono kwa kutumia sokisi ama kitambara kikukuu. Ifanya ‘Yenye tabia ya Upuzi’ (isiwe sawa na binadamu ama mnyama. Tengeneza macho, pua, na mdomo kwa kutumia kifungo, uzi au kitambaa. Tumia huyu mwanaserere wakati mwingine kukusaidia kutoka hadithi ama kupeana kitendo. Waeleze watoto kwamba huu si mwujiza. Wakati mwingine waruhusu wanafunzi watumie huyu mwanaserere ili waelewe zaidi.

## **JINSI YA KUOMBA NA WALE WANAOATAFUTA USO WA MUNGU**

(Tafadhali badili kama inahitajika)

- a. Tambua umuhimu wa muda huo, ipatie umakini kamili na uwe mwangalifu kwa uongozi wa Roho Mtakatifu
- b. Piga magoti, kaa au simama karibu na mtu ambaye unakusudia kumsaidia.
- c. Kwa kimya omnia mwongozo wa Mungu na, bila kukatiza maombi yake, waombee pia. Yeye ndiye anayepaswa kuomba - wewe uko tu kusaidia kama Roho Mtakatifu anavyoongoza.
- d. Sikiliza sala ya mtafuta ili kubaini ikiwa wanahitaji msaada.
- e. Wakati mtafuta amemaliza kuomba, tafuta ikiwa ana uhakika kwamba maombi yake yalijibowi. Si lazima ujue ombi ni juu ya nini labda iwe anataka kuzungumza juu yake.
- f. Kama mwenye anatafuta maombi ataendelea kuomba bila kufika mwisho, au bila kuwa wazi:
  - i. Muulize kwa uangalifu ikiwa unaweza kusaidia. Mara ruhusa ikipewa,
  - ii. Tafuta ni kwa nini alikuja kuomba.
  - iii. Muongoze kwa ufupi na Maandiko husika.
  - iv. Pamoja ombeni kwa hitaji maalum na mtumaini Mungu na ombi.
  - v. Wakati mmemaliza kuomba, tafuta ikiwa ana uhakika kwamba maombi yake yalijibowi. Kama sivyo, wahimiza kwa muda mfupi waendelee kumwamini Mungu na kutembea katika nuru kama vile Mungu anamwongoza. Mkumbushe kwamba ni kwa imani tu kwa Mungu wanaweza kupata ushindi na, mara tu kazi imekamilika, Roho Mtakatifu atashuhudia pamoja na roho zao. Kunaweza kuwa hakuna udhihirisho wa mwili lakini uhakikisho wa Roho Mtakatifu utakuwapo kila wakati.
- g. Kumbuka kumpa mchungaji majina ya wale wote wanaotafuta maombi na matokeo ya maombi yao.

# **UTANGULIZI – KITENGO CHA I**

## **YESU ANAANZA HUDUMA YAKE**

---

**Marejeo ya Kibiblia:** Luka 2:42-52; Mathayo 3:1-17; 4:18-22; Marko 3:13-19; Yohana 1:35-51

**Mstari wa Kumbukumbu ya Kitengo:** *Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu* (Luka 2:52)

### **Malengo la Kitengo**

#### **Kitengo hiki kitasaidia Watoto:**

- kujuu hatua za kwanza za huduma ya Yesu
- kukua katika ujuzi wao juu ya Mungu
- tazama mtazamo wake mtiifu baada ya ubatizo wake
- jifunze njia maalum ambayo Yesu alitumia kuchagua wanafunzi Wake

#### **Kitengo cha Masomo:**

**Somo la 1: Yesu Ajifunza**

**Kutii Somo la 2: Yesu**

**Abatizwa Somo la 3: Yesu**

**Ajaribiwa**

**Somo la 4: Yesu Anawachagua Wanafunzi Wake**

#### **Kwa nini watoto wanahitaji kufundishwa kwa kitengo hiki:**

Watoto wanapaswa kujuu kwamba Yesu Kristo ni mhusika wa kweli wa hadithi ya kweli; si hadithi ya ndoto bandia.

Masomo haya yatawasaidia watoto kumjua Yesu kutoka umri wake wa miaka 12. Kupitia kwa maneno haya ya Kibiblia watoto wataanza kujifahamisha:

- na kijana mdogo, Yesu, ambaye aliita umakini wa watu kwa hekima Yake
- na njia ambayo Yesu aliiitikia na Maandiko kwa kila jaribu la Ibilisi
- na njia maalum ambayo Yesu aliwachagua wanafunzi wake. Yesu hakuchagua watu mtajiri wala mashuhuri, lakini wanaume wepesi na hata wakorofi.

**SOMO LA****01****YESU AJIFUNZA KUTII**

Maandiko: Luka 2:41-52

**Lengo la Somo**

Kuwafundisha watoto kwamba Yesu alimtii Baba Mungu, na kwamba wanaweza pia kufanya hivyo.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu” (Luka 2:52)

**Jitayarishe Kufundisha**

Tunapoona watoto wanakimbia na kucheza – tunaonakana kufanya makosa ya kufikira kwamba watoto hawajakomaa kiroho na hawawezi kufikiria kwa uzito. Watoto wana uwezo mkubwa wa kuelewa asili ya kiroho ya ulimwengu wetu, wakati mwagine hata wazi zaidi kuliko sisi watu wazima. Tunaweza kuifunza mambo ya thamani kuhusu ukuaji wa kiroho tunapowaona watoto wetu wakiyatoa maisha yao madogo katika Mikono ya Mungu yenye nguvu.

Vivyo hivyo akili na moyo wa Yesu ulikuwa kama mtoto, akili za udadisi na mioyo laini ya watoto inahitaji kujazwa na ukweli wa Mungu. Miaka hii ya kwanza itaamua mwelekeo amba watoto wako watafuata katika siku zijazo. Kama walimu ni nafasi kuu na jukumu kiasi gani tunayo kusaidia mwelekeo amba watoto wetu watafuata.

- Andaa mapema mafunzo yoyote ambayo utatumia kwa somo hili. Tengeneza nakala za Shughuli Ukarasa 1A kwa watoto wako.
- Kumbuka kurekodi mahudhurio, kuchukua sadaka, kukaribisha wageni na kukusanya habari za familia zao kuwasiliana nao wakati wa wiki.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Kamata umakini wa wanafunzi wako: Kabla ya darasa, andaa sanduku (begi au begi la kusafiri) na uliweke mbele ya darasa mahali pazuri kuonyesha wazo la kusafiri.

Waulize watoto: “Fikiria juu ya safari zozote ulizochukua. Je, ulichukua nini ya kwenda nayo kwenye safari yako? Safari hiyo ilidumu kwa muda gani? Umeona nini njiani? Ulienda wapi? Je! Kuna ye yeyote kati yenu aliywahi kupotea kwa kujitenga na wazazi wako mjini? Ulijisikiaje? Je, wazazi wako walihizije? Je, wazazi wako walikutafuta? Je, uliwatafuta wazazi wako? Je, walifanya nini walipokupata?”

Acha watoto wasimulie uzoefu wao.

Je! Unafikiri Yesu alipotea kamwe?”

“Acha tusikiliza hadithi nzuri juu ya safari Yesu alifanya na familia yake:

**Yesu Ajifunza Kutii**

Katika hadithi ya Luka 2:41-52 tunampata Mariamu, Yusufu, na Yesu wa miaka 12 wakianza matembezi marefu kwenda Yerusalem kwa sherehe maalum iliyoitwa Sikukuu ya Pasaka. Baada ya siku chache sherehe zilimalizika na kila mtu akaanza kurudi nyumbani kwake. Wakati wakitembea, Yusufu na Mariamu waligundua kuwa hawangeweza kumpata mtoto wao. Hakuna mtu mwagine aliywemwona Yesu pia. Yusufu na Mariamu waliamua kurudi Yerusalem kumtafuta Yesu. Hatimaye walimpata Yesu ameketi pamoja na walimu wa Sheria hekaluni. Kila mtu alishangazwa na akili na majibu ya Yesu. (Mwalimu – Fikiria njia za ubunifu za kuwasaidia watoto taswira ya tukio la Yesu wa miaka 12 akiwa ameketi na waalimu wa Sheria.)

Kama wazazi Yusufu na Mariamu walionyesha wasiwasii wao wakati walipompata mtoto wao. Mariamu aliuliza, “Yesu, kwa nini hukurudi na sisi? Wakati hatukukupata tulikuwa na wasiwasii na

tukakutafuta kila mahali!"

Yesu alishangaa. "Kwani kunitafuta?" aliwaambia. "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" (Luka 2:49) Yusufu na Mariamu hawangeweza kuelewa kile Yesu alikuwa anasema.

Kwa ombi lao Yesu aliwafuata wazazi wake wa duniani kurudi Nazareti ambapo aliishi kwa utiifu wao, huku akiendelea kuimarisu uhusiano Wake na Baba yake wa Mbinguni. "Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." (Luka 2:52) inatukumbusha kwamba Yesu alikua kama mtoto – kimwili, kiakili, na pia alikua "akimpendeza Mungu na wanadamu." Tunajua kwa uhakika kwamba kwa umri wa miaka 12 Yesu alielewa umuhimu wa uhusiano wake na Mungu. Masomo aliyoyasoma kama kijana yangemsaidia Yesu baadaye kutumaini katika Yule aliyemtuma kutimiza utume wake wa kuwa Mwokozi wa ulimwengu.

## Zoezi

### Tuchukue Safari!

- Wachukue watoto kwenye matembezi ya kuzunguka kanisa.
- Baada ya kufika mahali karibu na watoto wakae na wasikilize. Yesu na familia yake walienda katika safari, kutoka Nazareti kwenda Yerusalem. Safari yetu ilichukua dakika chache tu, lakini iliwichukua siku kadhaa.
- Wakati unashika Biblia, elezea tena hadithi ya Luka 2:41-52, lakini kwa maneno yako mwenywewe.
- Baada ya kukamilisha hadithi rudini pamoja na watoto mahali pao pa mafundisho.

(Hapo awali ulikuwa umeuliza mtoto kwa siri acae mahali ambapo ulielezea hadithi wakati wengine wote walirudi sehemu ya kufundisha pamoja na wewe.)

- Wakati darasa linearudi uliza, "Je, tuko hapa sisi sote?" Angalia chumbani na uhesabu ni watoto wangapi wako dasanani. Jifanye unashangaa mtu anapotea. "Je, nani anayekosa? Aa, \_\_\_\_\_ hayupo. Lazima turudi tumtafute."
- Kama kikundi nenda kumtafuta mtoto aliyepotea na umrudishe pamoja nawe. "\_\_\_\_\_ alikaa nyuma na hakurudi na sisi. Fikiria vile wazazi wa Yesu walihisi wakati waligundua kuwa Yesu hakuwa pamoja nao. Je, Yesu aliwaambia nini wakati walimpata ndani ya hekalu? ("Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu") Hata kama mtoto, Yesu alitaka kuwa na uhusiano mzuri na Mungu, Baba yake wa Mbinguni. Kama Yesu, tunawezaje kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu? (...kwa kusoma Biblia zetu, kwa kumuomba Mungu, kwa kusikiliza kile wazazi, wachungaji, na walimu wanasema kuhusu Mungu, na kuwatii.)
- Wape watoto nakala zao za Shughuli Ukurasa 1A. Andika au chora kitu tunaweza kufanya kuwa karibu na Mungu. Eleza picha na ukweli wowote uliojifunza.

## Kukariri

"Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." (Luka 2:52) Utahitaji mpira au kitu ambacho kinaweza kutupwa. Gawanya darasa katika timu mbili. Wakiwa wamesimama au wameketi, timu moja ikiwa imeangalia ingine, mpe mpira mtoto wa kwanza wa moja ya timu moja. Mtoto huyo atasema neno la kwanza la mstari (kwa mfano: "Na"). Basi lazima atupe mpira kwa mtoto wa kwanza wa timu pinzani, anaposema neno la pili ("Yesu"). Mpira utaendelea kutoka kwa mtoto hadi mtoto, kwa muundo wa zigizaga, hadi kile mtu aseme neno la mstari. Wanapomaliza kusema, pamoja na kumbukumbu, anza upya. Kwa kuirudia, watoto watajifunza aya ya kumbukumbu.

## Kufunga

Omba pamoja na watoto. Muombe Bwana awasaidie kuwa watiifu na wawe karibu na Mungu, kama vile ilivyokuwa na Yesu. Kama kuna watoto amba wanaweza kuwa hawakumtii Mungu na/au wazazi wao, panga madhabahu ya muda wa maombi. Unaweza kupeana kadi zilizo na majina ya watoto wanaohitaji kuombewa. Watie moyo waombee kila mmoja na wawaeleze wazazi wao, ndugu na dada zao, na marafiki hadithi ya leo ya Biblia. Katika hali hiyo, wengi watapata kumjua Yesu na jinsi alikuwa mtifupi kwa wazazi Wake. Waalike watoto warudi Jumapili ijayo.


## Zoezi la 1

### **YESU AJIFUNZA KUTII**


**Maandiko:** Luka 2:41-52

**Lengo la Somo:** Kuwafundisha watoto kwamba Yesu alimtii Mungu ambaye ni Babake, na wanaweza pia kufanya hivyo.


**Mstari wa Kumbukumbu:** “Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.” (Luka 2:52)



1



2



3

**Je, Nawezaje Kumtii Mungu?**

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na waelewe kwamba ubatizo wake unaonyesha kuwa alikuja kutuokoa kutoka kwa dhambi.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu” (Luka 2:52)

**Jitayarishe Kufundisha**

Ingawa watoto ni wadogo, ni muhimu sana kudhibitisha kuendelea kwao kwa kiroho. Ingawa wanampenda na kumtumikia Mungu, hawawezi kutoa ushuhuda kama wazazi wao au watu wengine wazima kanisani. Wajibu wa maendeleo yao ya kiroho hutoka kwa kutazama urafiki kati ya wazee walio karibu nao na Mungu. Wacha tujaribu kurekebisha maoni ya mtoto juu ya Mungu, na kuwapa watoto fursa ya uzoefu na kusimulia juu ya upendo na neema ya Mungu.

- Tayarisha mapema vifaa vyovoyote vya mafundisho ambayo utatumia kwa somo hili
- Kumbuka kurekodi mahudhurio, kuchukua sadaka, kukaribisha wageni na kukusanya habari za familia zao, kuwasiliana nao wakati wa wiki

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Wanyakuaji wa Umakini: Kabla ya darasa – Andika kile herufi ya neno “U-B-A-T-I-Z-O” kwenye ubao tofauti (unaweza kuweka miviringo ya mkanda wa kuficha nyuma barua ili kuzibandika au weka shimo na uzifunge kwa ukuta ukitumia uzi). Ndani ya darasa - In class – changanya herufi na uwape watoto. Sema: Pangeni hizi herufi ili kutengeneza neno lililo na maana maalum. Kama unayo herufi inayoambatana na ufunguo ninaoenda kuwapa, ining’inez juu:

- |   |           |
|---|-----------|
| +Herufi ya kwanza ni herufi ya ishirini na moja ya alfabeti.          | (U)       |
| +Herufi ya pili ni herufi ya pili bado ya alfabeti.                   | (B)       |
| +Herufi ya tatu ni herufi ya kwanza ya alfabeti.                      | (A)       |
| +Herufi ya nne ni herufi ya ishirini ya alfabeti.                     | (T)       |
| + Herufi ya tano ni vokali iliyo na nukta.                            | (I)       |
| + Herufi ya sita ni herufi ya ishirini na sita ya alfabeti.           | (Z)       |
| + Herufi ya mwisho ni herufi ya kumi na tano ya alfabeti.             | (O)       |
| * Waulize watoto: Je, ni neno gani ambalo tunalitamka na herufi hizi? | (Ubatizo) |

Sema: Ubatizo ulikuwa na ni njia ya kuonyesha kuwa umetubu dhambi zako. Unaonyesha pia unataka kuishi kwa Mungu. Wakati Yohana Mbatizaji alihubiri, aliwaambia watu kwamba walihitaji kutubu na kubatizwa.

“Je, umebatizwa?”

Hebu tusikilize sasa hadithi ya kusimua kuhusu mtu aliyebatizwa.

(Mwalimu, ili kufanya hadithi ifurahishe tumia kikaragosi kuwalisha Alberto.)

Habari, jina langu ni Alberto. Nitawaeleza kuhusu mtu wa ajabu ambaye jina lake ni Yohana. Watu wengine walitueleza kwamba Yohana alkuwa akisema na watu kando ya Mto Yordani. Mama yangu pamoja nami tuliamua kuenda kujionea.

Yohana alivaa mavazi yaliyotengenezwa kwa singa za ngamia. Mtu alisema alikuwa asali na nzige. Eti! Yohana aliwaambia watu, “Tubuni-acheni dhambi zenu na mumwombe Mungu awasamehe.”

Watu waliingia ndani ya maji na Yohana kwa upole akawasukuma ndani ya maji. Mama aliniambia hii ilitwa ‘ubatizo’ na ndio maana watu walimwita ‘Yohana Mbatizaji’.

Tulikuwa tumeketi juu ya mwamba tukitazama wakati kikundi cha Mafarisayo pia kilikuja kumwona Yohana. Mama aliniambia Mafarisayo walikuwa viongozi wetu wa dini muhimu zaidi. Yohana pia aliwaona Mafarisayo wanakuja; hao kundi la nyoka!

Yohana Mbatizaji alisema mambo ya kigeni; aliongea juu ya mtu mwingine ambaye atakuja, mtu mwenye nguvu! Yohana alisema kwamba hata yeye alikuwa hastahili kufungua kamba kwenye viatu vya mtu huyu. Je! Yohana angeweza kuzungumza juu ya nani? Ghafla mtu huyu mpole sana alitembea hadi kwa Yohana mtoni. Yohana alifurahi sana kumwona. Mtu alinong'ona, “Huyo ni Yesu! Anataka kubatizwa!” Yohana alimwambia Yesu, ‘Ninahitaji kubatizwa na wewe, unawezaje kuja kwangu kubatizwa?’

Yesu alisitisiza kwamba Yohana ambatize na kwa hivyo Yohana alimwongoza Yesu kuingia mtoni. Yohana kwa upole alimsukuma Yesu ndani ya maji. Wakati Yesu alikuja jambo la kufurahisha zaidi lilitokea; anga ikafunguliwa na Roho wa Mungu akashuka juu ya Yesu kama njija nzuri. Tulisikia sauti kuu kutoka mbinguni ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa; Nimefurahishwa sana naye.’ Hatungeamini yale tulikuwa tunesikia au kuyaona. Tulienda nyumbani tukiwa tumeshangaa na kila kitu kilichotendeka siku hiyo!

## Zoezi

- Je, Yohana alimwambia nini Yesu? (Nahitaji kubatizwa nawe.)
- Je, nini kilitokea Yesu alipotoka ndani ya maji? (Roho Mtakatifu alishuka juu ya Yesu kama njija na sauti ya Mungu ikasikika.)
- Je, unafikiri ni kwa nini ubatizo wa Yesu ulikuwa muhimu? (Kwa sababu alionyesha kwamba aliwapenda wenyewe dhambi na kwamba alikuwa amekuja kuwasaidia.)
- Je, tunamshukuru Yesu kwa njia gani kwa kuwa Mwokozi wetu? (Kwa kumpenda Mungu, kwa kufanya yale anayotaka sisi tufanye, kumpokea Yesu kama Mwokozi.)

## Kukariri

“Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.” (Luka 2:52)

Utahitaji seti 2 za kadi zilizo na maandishi ya mstari (kwa mfano “Na”). Ficha kadi katika maeneo tofauti wakati watoto hawaoni kwa mfano “Yesu” nyuma ya mlango na kadi ingine “Yesu” kwa dirisha. Gawa darasa katika timu mbili. Watoto watalitafuta neno la mstari na kisha walipange kwa mpangilio kutoka kwa mstari wa kwanza hadi ya mwisho pamoja na kumbukumbu. Timu ya kwanza kupata na kupanga kadi zote za mstari watasoma na kusoma juu ya mstari huo. Watoto watajifunza mstari wa kumbukumbu.

## Kufunga

Omba pamoja na watoto. Muombe Bwana awasaidie kuonyesha shukrani kwa Yesu kwa kuwa Mwokozi wetu. Kama kuna watoto ambaa wanaweza kutaka kumkubali Yesu, panga muda wa maombi ya madhabahu. Peana kadi zilizo na majina ya watoto wanaotaka kuombea. Wahimize waombeane na waeleze hadithi ya Biblia kwa wazazi woa, ndugu na dada zao, na marafiki. Katika hali hiyo, wengi watajifunza kumjua Yesu na vile alikuja kutuokoa kutoka kwa dhambi. Waalike watoto warudi Jumapili ijayo.

## **Zoezi la 2**


# **YESU ABATIZWA**

**Maandiko:** Mathayo 3:1-17

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Alikuja kutokoa kutoka kwa dhambi.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.” (Luka 2:52)

**“Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.’”**  
**(Mathayo 3:17)**



## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Yesu alikuwa aamue kumtii Mungu au Shetani. Nasi pia hatuna budi kufanya uamuzi huo.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu” (Luka 2:52)

## Jitayarishe Kufundisha

Watoto wanastahili kujua kwamba maaazi mengine ni mabaya. Uamuzi wa kumuasi Mungu siku zote ni makosa. Mungu habadiliki. Mungu akisema kitu ni kibaya kitakuwa kibaya kila wakati. Shetani anaweza kujaribu kutushawishi tumtii Mungu. Mungu anatujua na anatupenda. Tunapaswa kujisikia vizuri kumwomba Mungu atusaidie wakati wowote tunapajaribiwa.

Mfululizo huu wa masomo juu ya maisha ya Yesu yatawaelekeza watoto kwa Yesu. Yeye ni mfano wetu wa utiifu na kujitoa kwa Muumba wetu.

- Tayarisha mapema vifaa vyovoyote vya mafundisho ambayo utatumia kwa somo hili
- Kumbuka kurekodi mahudhurio, kuchukua sadaka, kukaribisha wageni na kukusanya habari za familia zao, kuwasiliana nao wakati wa wiki

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Wanyakuaji wa Umakini: Kabla ya darasa – Andika kile herufi ya neno “M-A-J-A-R-I-B-U” juu ya kadi tofauti. Ziweke kadi kwenye ubao katika utaratibu wao lakini uzipindue ili mtu asiweze kuziona. Andika ufanuzi wake juu ya kadi ingine. Ndani ya Darasa sema: “Leo tutajifunza neno mpya. Nitauliza baadhi ya maswali, yejote atakayeji vizuri anaweza kupindua kadi zake.”

- Waulize watoto: *Je, unapaswa kuwatii wazazi wako? Je, ni sawa kudanganya? Je, ni vizuri kunywa kinywaji ambacho si chako? Je, ni vizuri kumpiga ndugu au dada yako? Je, ni vizuri kuiba kazi ha mwenzio darasani au wakati wa mtihani?*

Je, ni nani anayeweza kusema neno ni gani? “Majaribu”

Je, majaribu ni nini? “Majaribu ni tamaa ya kufanya jambo la kumuasia Mungu.”

Sema: Sisi wote tunakutana na majaribu. Mara nyingi, tunapaswa kuchagua kati ya mema na mabaya. Hadithi ya leo inazungumzia mtu aliyekutana na majaribu; Yesu. Wacha tuone kama alifanya uamuzi mzuri:

Mpe kila mtoto karatasi na penseli:

- kunja karatasi mara mbili
- fungua karatasi na ulikunje katikati kwa mwelekeo mwingine. (Kwa hivyo karatasi hiyo itagawanywa katika sehemu nne sawa.)
- andika namba 1 hadi 4 kwenye sehemu

Unapoelea hadithi ya leo, sitisha kidogo katika kila mwisho wa eneo kwa watoto kuchora picha rahisi inayohusiana na eneo hilo.

**Jaribio Ngumu kwa Yesu (Mathayo 4:1-11)**

**Eneo la 1**

Baada ya Yohana kumbatiza Yesu Roho wa Mungu alimwongoza Yesu nyikani. Katika kuijandaa kwa kazi ambayo Mungu alikuwa amempangia Yesu afanye, Yesu alitaka kujua ilivyofanana kujaribiwa

kumuasi Baba yake wa Mbinguni. Kwa siku 40 mchana na usiku Yesu hakula chochote. Ibilisi alimwambia, “Ikiwa ndiwe mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate.” Yesu alikuwa na njaa, lakini alimwambia ibilisi, “Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

(WAKATI WA KUCHORA)

### Eneo la 2

Ibilisi alimpeleka Yesu hadi mji wa Yerusalem. Shetani alimweka juu ya kinara cha hekalu na akamjaribu tena, akimwambia, “Ukiwa ndiwe mwana wa Mungu jitupe chini. Neno la Mungu linasema kwamba malaika watakuchukua ikiwa utaanguka.” Yesu alimjibu kwa maneno ya Kumbukumbu la Torati 6:16: “Imeandikwa pia, ‘Usimjaribu Bwana Mungu wako.’”

(WAKATI WA KUCHORA)

### Eneo la 3

Ibilisi alimpeleka Yesu juu ya mlima mrefu. Kutoka hapo yesu angeona umbali mrefu sana. Ibilisi akasema, “Haya yote mitakupa, ukianguka kunisujudia.” Yesu alimjibu, “Nenda zako Shetani, kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako na umwabudu yeye peke yake.”

(WAKATI WA KUCHORA)

### Eneo la 4

Ibilisi aliondoka nao malaika wakaja kumlinda Yesu. Alishinda majaribio hayo makuu kwa ushindi mkuu. Kila wakati ibilisi alimjaribu Yesu, alifanya chaguo la kumtii Mungu!

(WAKATI WA KUCHORA)

“Je, kuna mtu yejote anayeweza kutaka kuelezea hadithi mara tena, tuonyeshe michoro yenu?”

## Zoezi

### Mchezo wa Majaribu

Andika Maneno ya Utiifu kutoka kwa Amri Kumi za Mungu kwenye kadi.

Mfano: *Hatutadanganya. Hatutaua. Tutaikumbuka siku ya Sabato tuitakase. Tutawaheshimu baba na mama yetu. Hatutaiba.*

Gawa darasa katika vikundi viwili.

Timu A itachukua kadi na kusoma Maneno ya Utiifu juu ya kadi.

Timu B inafikiria juu ya vitu ambavyo vinawenza kujaribu Timu A kufanya yale walisema watafanya au hawatafanya.

Timu A inafikiria njia za kupigana na majaribu.

Zungusha ni kikundi kipi ambacho ni Timu A.

## Kukariri

“Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.” Waambie watoto wasikilize kwa makini na wahesabu idadi ya maneno katika mstari wa leo wa kumbukumbu.

Soma mstari wa maandiko pole pole kusisitiza kila neno la kipekee.

Soma mstari mara ya pili ili wote waangalie tena neno lao. Sikiliza watoto tofauti wakipeana maneno yao ya kufikiria. Kama utapata majibu kadha tofauti rudia hatua yote.

-inafurahisha, zoezi linalorudiwa rudiwa ili kuwasaidia wote wakariri mstari wa Biblia.

## Kufunga

Waulize watoto kama wako na hitaji la maombi. Ombea mahitaji hayo na kisha uwaombee wanafunzi wako, ukimwomba Mungu awasaidie kushinda majaribu kama vile Yesu alivyoshinda. Watie moyo wahudhurie darasa linalofuata na wawaeleze watu hadithi ya leo..


## Zoezi la 3

### **YESU AJARIBIWA**

**Maandiko:** Mathayo 4:1-11

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujuu kwamba Yesu alikuwa aamue kumtii Mungu au Shetani. Nasi pia hatuna budi kufanya uamuza huo.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu” (Luka 2:52)



- 1. \_\_\_\_\_ ni chochote kinachotufanya tutake kumuasi Mungu. Inatusababisha kufikiria kwamba kumuasi Mungu ni sawa na vizuri kabisa.**
- 2. \_\_\_\_\_ ni jina maalum la Yesu. Wakati tunafahamu Yesu, tunamfahamu Mungu ni nani na anavyofanana.**
- 3. \_\_\_\_\_ ni furaha tunakuwa nayo wakati Mungu anatusamehe dhambi zetu na kutupanaisha kwake. Tunaweza kuwa na amani hata wakati mambo mabaya yanatendeka kwetu.**
- 4. \_\_\_\_\_ ni jina lingine maalum la Yesu. Jina hili linathihirisha kwamba Yesu “alichaguliwa na Mungu”. Mungu alimchagua Yesu kuwa Mwokozi wetu.**

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Yesu alikuwa aamue kumtii Mungu au Shetani. Nasi pia hatuna budi kufanya uamuzi huo.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu” (Luka 2:52)

**Jitayarishe Kufundisha**

Tunaamini watoto hawawezi kumfanyia Yesu mengi kwa sababu ni wadogo sana. Kuna njia nyingi ambazo watoto wanaweza kuwa wasaidizi wa Yesu. Somo hili litawasaidia watoto kuanza kuelewa kile kinachomaanisha kuwa mfuasi wa Yesu na kufikiria njia ambazo wanaweza kusaidia kwa kazi ya Mungu leo.

- Tayarisha mapema vifaa vyovyyote vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili
- Kumbuka kurekodi mahudhurio, kuchukua sadaka, kukaribisha wageni na kukusanya habari za familia zao, kuwasiliana nao wakati wa wiki,
- Pitia tena masomo matatu ya hapo awali na uwaambie wanafunzi watoe mifano ya vile wamekuwa waaminifu kwa Mungu.

Nyakua Umakini wa Watoto:

**Mbele ya darasa:** Kwenye karatasi nzito/kadibodi chora picha ya bahari, pwani na boti. Fikiria juu ya mifano katika historia ambayo Mungu alitumia watoto kuwaongoza wazazi wao kwa Kristo. Waeleez watoto wako mfano wowote ambaao unajua au mwulize mchungaji wako atembelee darasa lako na aeleze hadithi jinsi watoto wamesaidia kuwaleta watu kwa Yesu. Hadithi hizi zitawahimiza watoto wako.

**Uliza:** Je, tunapewa lini maagizo? (shuleni, kufua, ununuza, kitu kinapowekwa pamoja, n.k.) Hebu tuone jinsi unavyoweza kusikiliza vyema na kufuata maagizo:

**SIMON ANASEMA**

**Sema:** Watoto, fuata maagizo yangu wakati tu nitasema SIMONI ANASEMA!

“SIMON ANASEMA ruka ruka juu na chini.” Wote, pamoja nawe, ruka ruka juu na chini.

“SIMON ANASEMA piga mikono.” Wote, pamoja nawe, piga mikono.

“SIMON ANASEMA kanyaga miguu.” Wote, pamoja nawe, kanyaga miguu.

- endelea kurudia maagizo tofauti, ukienda haraka na haraka

**Sema:** “Sugua tumbo lako.” (Wakati huu Simon Anasema.) Wewe sugua tumbo lako. Mtoto yeoyote anasugua tumbo lake aondolewe – kwa sababu wakati huu hukusema SIMON ANASEMA.

**Uliza:** Je, unapaswa kusema nini ili kushinda mchezo huu: (Sikiliza maagizo na ufanye tu kile Simon anasema.) Ni muhimu sana kufuata maagizo.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Tengeneza takwimu za Yesu, Petro, na wanafunzi wengine, na watoto wengine. Tepe takwimu katika maeneo yanayofaa kwenye msingi wa bahari/pwani uliyotengeneza.

Hadithi ya leo inatueleza kuhusu baadhi ya watu ambaao walisikiliza na kufuata maagizo:

Siku moja alipokuwa akitembea kwenye pwani ya Bahari ya Galilaya Yesu alijaona baadhi ya wavuvi wa samaki. Waliitiwa Simon Petro na ndugu yake, Andrea. Walikuwa pembeni mwa maji,

wakitupa nyavu zao kuvua samaki. Yesu aliwaita. "Nifuateni na nitawafanya kuwa wavuvi wa watu." Petro na Andrea walitazama, wakatazama nyavu zao, wakafuata maagizo ya Yesu, na kuondoka mara moja kumfuata Yeye. Walipokuwa wakitembea pamoja na Yesu kwenye pwani, waliwaona baadhi ya marafiki wao wawili, Yakobo na Yohana, wamekaa kwenye mashua yao ya uvuvi, wakitengeneza nyavu zao.

Yesu aliwatazama na kuwaambia, "Nifuateni na mjivunze kuwavua watu." Kwa upesi, Yakobo na Yohana walismama, wakafuata maagizo ya Yesu, wakatoka kwenye mashua, na kumfuata Yesu. Baada ya siku chache Yesu aliamua kuondoka Galilaya. Alimpata Filipo ambaye alikuwa anatoka mji huo huo amba Petro na Andrea walitoka. Yesu pia alimwita Filipo amfuate. Filipo kisha akampata rafiki yake Nathanieli, "Lazima uje ukutane na mtu. Jina lake ni Yesu wa Nazareti. Yeye ni Mwokozi aliyahidiwa, ambaye Musa na manabii waliandika juu yake."

"Je, ulisema ametoka Nazareti?" Nathanieli aliuliza. "Je! Kitu chochote kizuri kinaweza kutoka Nazareti?" "Njoo uone," Filipo alijibu.

Nathanieli alikwenda na Filipo.

Yesu alipowaona wanakuja, alisema, "Hapa kuna Mwisraeli ambaye ndani yake hamna uongo!" Nathanieli alishangaa sana, "Unaniju kutoka wapi?"

"Nilikuona wakati ulikuwa chini ya mtini, hata kabla Filipo hajakuita," Yesu alijibu.

Nathanieli alishangaa sana. Alijua kwamba Yesu hakuwa mtu wa kawaida. "Rabi, wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme wa Israeli!" Alishangaa.

Yesu alimtzama. "Je, unaamini tu kwa sababu nilikwambia nilikuona chini ya mti? Utayaona maajabu zaidi ya haya."

Yesu na wafuasi wake walisafiri kupidia mko huo. Siku moja Yesu alipanda mlima. Aliwaalika marafiki hawa kwenda naye na akasema, "Mtakuwa wanafunzi wangu. Nataka ukae nami na ujifunze kufuata maagizo yangu."

Majina ya wanafunzi 12 yalikuwa Simoni Petro, Andrea, Yakobo, Yohana, Filipo, Batholomayo, Tomaso, Mathayo, Yakobo mwana wa Alfayo, Tadayo, Simoni Mkananayo, na Yuda Iskarioti.

**Imba:** Kulikuwa na wanafunzi 12

*Kulikuwa na wanafunzi kumi na mbili Yesu aliwaita wamsaidie:*

*Simoni Petro, Andrea, Yakobo, nduguye Yohana,*

*Filipo, Tomaso, Mathayo, Yakobo mwana wa Alfayo,*

*Tadayo, Simoni, na Yuda, Batholomayo.*

*Ametuita sisi pia. Ametuita sisi, pia.*

*Sisi ni wanafunzi wake; Mimi ni moja na wewe pia!*

*Ametuita sisi pia. Ametuita sisi, pia.*

*Sisi ni wanafunzi wake; Mimi ni moja na wewe pia!*

**Sema:** Hawa 12 walikuwa wasaidizi maalum wa Yesu. Walisafiri na Yesu na kumsaidia katika huduma yake hapa duniani. Walii twa "wanafunzi". Leo Yesu bado anahitaji wasaidizi (wanafunzi) wamfuate, wajifunze kutoka kwake, wamtii, na kumtumikia. Tunaweza pia kuwa wanafunzi wa Yesu!

### Peleka Zoeizi Nyumbani

**Uliza:** Watoto, je, mko tayari kufanya ahadi hii: \_\_\_\_\_ ahadi za kutii na kufanya kazi ya Mungu. (jina la mtoto)

Kama ni hivyo, basi unachukuliwa kama mwanafunzi wa Yesu. Chora na ukate sura yako mwenyewe, na jina lako liko mbele yake (sawa na saizi uliyotengeneza mapema ya Yesu na wanafunzi wake).

### Kukariri

"Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." (Luka 2:52)

Waambie watoto warudie mstari wa kukariri wanapotembea pamoja kuelekea baharini/pwani. Weka picha pamoja na majina yao kwenye historian a Yesu na Wanafunzi wake.

### Kufunga

Tena, fanya mwaliko wa kumfuata Yesu. Kama watoto wako tayari kuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu waulize waweke picha zao karibu na ile ya wanafunzi waliomfuata Yesu.

## Zoezi la 4

### **YESU AWACHAGUA WANAFUNZI WAKE**

**Maandiko:** Mathayo 4:18-22; Marko 3:13-19; Yohana 1:35-51

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Yesu alikuwa afanye uamuzi kati ya kumtii Mungu au Shetani. Tunapaswa pia kufanya uamuzi huo.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akmpendeza Mungu na wanadamu.” (Luka 2:52)

- 1. Tazama maneno yaliyo katika SANDUKU LA MANENO**
- 2. Yatafute maneno katika sehemu ya maneno. Yanaweza kuwa usawa au wima**
- 3. Kamilisha nafasi katika mstari wa Biblia. Kisha kariri Mathayo 4:19 na rafiki.**

Benki ya  
Neno  
Watu  
njoo  
tuma  
samaki  
mimi  
nenda

F	C	M	O	T	Y	U	P	S	E	O	G	F
R	M	O	Q	P	E	O	W	A	T	U	M	N
W	J	I	C	S	B	R	E	M	Y	T	X	Z
N	K	E	M	N	E	N	D	A	P	R	R	W
E	M	A	Q	I	S	D	I	K	D	E	J	I
P	N	P	K	C	H	F	S	I	H	E	S	P
T	U	M	A	B	I	O	P	H	H	R	E	E

“ ———, fuata ———, Yesu alisema ,

‘na nita —— ku ——— tu ——— .’”

**Mathayo 4:19**

# **UTANGULIZI – KITENGO CHA II**

## **YESU AFANYA TOFAUTI**

---

**Marejeo ya Kibiblia:** Marko 1:40-44; 2:13-16; 14:66-72; Yohana 21:1-29

**Mstari wa Kumbukumbu wa Kitengo:** “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyä; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya!” (2 Wakorintho 5:17)

### **Lengo la Kitengo**

#### **Kitengo hiki kitatusaidia:**

- Kuelewa kwamba tunapomkubali Yesu hatutakuwa kama tulivyokuwa mbeleni
- Kumruhusu Kristo atuongoze ili tusitende dhambi
- Kujuu kwamba sisi sasa ni wafuasi wa Mungu mwenye nguvu na wa upendo.
- Kuamini kwamba Bwana anaweza kubadilisha hata yule mtu mwenye dhambi nyingi na muovu zaidi.

### **Masomo ya Kitengo**

**Somo la 5: Yesu Amponya Mtu wa Ukoma**

**Somo la 6: Yesu Ambadilisha Mathayo**

**Somo la 7: Yesu Anawapenda Watoto**

**Somo la 8: Yesu Amsamehe Petro**

Inaweza kuwa vigumu kwa watoto kuelewa neno “dhambi.”

Lakini, watoto wanajifunza kujuu wakati mtu anatenda mambo mazuri au mabaya.

Kupitia kitengo hiki tutazwez kuona faida zinazotokana na kutotenda dhambi. Tutatambua kwamba Yesu anaweza kutusaidia tusitende dhambi.

Kabla tumkubali Kristo ndani ya mioyo yetu tulikuwa chini ya utawala wa ibilizi (ufalme wa giza) na tulifurahia kutenda dhambi; kama vile kudanganya, kuiba, kusema maneno mabaya, kuchukua, n.k.

Kwa vile sasa sisi ni watoto wa Mungu (Ufalme wa Nuru) hatutaki tena kutenda dhambi.

Tuweza kuelewa kwamba Mungu wakati Mungu anatupatia moyo mpya, uliosamehewa tunakuwa tofauti.

## Lengo la Somo

Kuwasaidia wanafunzi kujua kwamba Yesu anawapenda watu wanaokataliwa. Anashughulikia mahitaji yetu.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyä; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya!” (2 Wakorintho 5:17)

## Jitayarishe Kufundisha

Watoto hutazama tabia nyumbani, shulenii, kanisani, na kuanza kuzikumbatia katika matendo yao na nia. Hadithi ya Yesu akimponya mtu wa ukoma ni somo la upana ambalo litawasaidia wanafunzi wako kuelewa huruma na kuwaongoza wengine katika kuwajali wasiojiweza.

- Tayarisha vifaa utakavyotumia kwa somo hili
- Kumbuka kurekodi mahudhurio, kuchukua sadaka, kukaribisha wageni na kukusanya habari za familia zao, kuwasiliana nao wakati wa wiki,
- Pitia tena masomo matatu ya hapo awali na uwaambie wanafunzi watoe mifano ya vile wamekuwa waaminifu kwa Mungu.

Mbele ya darasa: andaa kukatwa kutoka kwa majarida na magazeti ya watu "tofauti": watoto na watu wazima wagonjwa kitandani, kwenye viti vyä magurudumu, watoto walio na glasi za macho au na fimbo ya mwongozo, mtu yeoyote ambaye anaelezea wazo la "uhitaji maalum."

Ndani ya darasa: Ning'iniza au bandika picha na uulize: Je, unaona nini ndani ya picha? Je, ungehisi vipi kama ingelikuwa ni wewe, umeketi kwenye kiti cha magurudumu au umelala kitandani? Je! Yesu anampenda mtu huyo? Je, Yesu anaweza kumponya yule akichagua kufanya hivyo? Sisitiza nguvu ya Mungu ya uponyaji. Zungumzia jinsi inavyoweza kuwa na huzuni kwa watu hao wakati tunawaepuka au kuwadhihaki. Sema: Acha tumuombe Bwana atusaidie kuwa wenye huruma; kuwaeleza watu hao kwamba Yesu ni Mungu wa upendo na kwamba wanapendwa na yeye.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

**Mbele ya Darasa:** kunja kila mraba wa sanduku katikati na kwa laini yenyé doti, chora umbo la moyo.

**Ndani ya darasa:** waulize wanafunzi wakate moyo kutoka kwa kila mraba. Kisha mtoto ataunganisha moyo kwa fimbo. Baada ya kumaliza na ufundi, waulize: Je, moyo unawakilisha nini? (Upendo) Tutatumia moyo kuonyesha somo la leo. Utainua moyo wako kila wakati unaposikia kwamba Yesu alionyesha upendo wake kwa mtu.

**Yesu Amponya mtu mwenye Ukoma**

“Najisi, najisi!” mtu mgonjwa na mwenye huzuni aliyesema maneno haya kwa sauti kila siku. Siku zote alikuwa amekaa barabarani akiangalia watu yenyé furaha na afya wakipita. Viongozi wa mji walikuwa na sheria iliyohitaji kwamba mwenye ukoma alitakakana kusema kwa sauti “najisi” ili mtu yeoyote asimkaribie na kushikwa na ugonjwa wake. Mtu aliyeambukizwa hakuruhusiwa kuingia kwenye majengo au kuwa karibu na watu wengine. Mavazi yake yalikuwa yameraruka na chafu. Ilikuwa vigumu sana kwake kupata chakula! Na vidonda, mwili mzima, vilikuwa vichungu na vibaya. Watu walimbonyezee vidole na kumkimbia. Mtu huyo alihisi upweke mwangi. Kila siku jambo lilelile lilitokea. Asubuhi moja akisema kwa sauti, “najisi, najisi!” kuwaonya watu wasimkaribie, mwenye ukoma alimwona mtu ambaye hakuwahi kumuona hapo awali. “Je, yawezekana?” Alifikiria kwa

shauku. "Je, yawezekana yule ni Yesu nimesikia juu yake, yule anayesema kwamba anaweza kuyaponya magonjwa? Ninakufa na ukoma huu mbaya, na labda mtu huyo anaweza kunisaidia.

Mtu huyo alimwendea Yesu akiomba kwa magoti, "Ikiwa ni mapenzi yako kunisafisha, unaweza kuifanya." Yesu alimwangalia yule mgonjwa ambaye alikuwa amepiga magoti mbele yake. Alimpenda na mara moja akamsaidia. Yesu akanyosha mkono wake na kumgusa mtu huyo, "Nataka... uwe safi." Mtu huyo aliinuka akiwa mzima! Hakuwa mgonjwa tena! Hakujua afikirie nini! Ndoto yake ilitimia! Ndio, iliwezekana! Hakuwa ndoto tena. Kile watu walisema kilikuwa cha kweli. Yeyote aliywendea Yesu alipokea uponyaji, msamaha, rehema na tumaini. "Aa asante Yesu!" yule mtu akashangaa. Kuangalia mikono na miguu yake, ambayo ilikuwa imefunikwa na vidonda wakati uliopita, sasa zilikuwa safi na laini. Ngozi yake ilikuwa mpya. Mtu huyo akasema kwa furaha, "Ninashukuru sana na nimefurahi. Lazima niende haraka nikawaambie watu wote kile kimenitendekea!" Lakini Yesu alimwambia, "Tazama, usimwambie mtu yeyote chochote. Bali nenda, ukajiwakilishe kwa kuhani na utoe dhabihu ya kusafishwa kwako ili kuonyesha kwamba umepona." Mtu mwenye furaha alijibu, "Asante, asante, nitafanya hivyo mara moja. Nina furaha!" Kisha akapotelea katikati ya umati, akiwaeleza watu yale Yesu alikuwa amemtendea. Ilikuwa siku nzuri kwa mtu huyo. Yesu alimpenda, hata na ugonjwa mbaya.

## Zoezi

Wape watoto karatasi za kupanga rangi zilizo na taswira mbili za kabla na baada ya Yesu kumponya mtu mwenye ukoma. Ruhusu watoto waangalie taswira mbili na uwosomee maagizo. Wacha walinganishe picha na wazungumzie tofauti kati ya taswira mbili. Hakikisha kwamba kila mtoto anaewela muktadha wa kabla na baada ya Yesu kumponya mtu mwenye ukoma.

**Uliza:** Je, mtu huyo alikuwa katika hali gani alipomwomba Yesu amsaidie? (Alikuwa na ugonjwa wa ukoma). Je, Yesu alifanya nini? (Alimponya)

**Sema:** Yesu alimponya, ndio maana alikuwa mtu mpya. Mstari wetu wa kumbukumbu unazungumza juu ya kiumbe kipyta. Mtu mwenye ukoma alipata baraka ambayo Kristo alimletea. Wape watoto muda wa kupaka picha rangi.

**Imba** nyimbo za sifa: Andaa mapema nyimbo mbili za sifa zenye furaha na zinazofaa ambazo watoto wanawenza kuimba wakati wa kuchorea.

**Sema:** Je! Unaweza kuwazia jinsi yule mwenye ukoma alihisi wakati Yesu alipomponya? Bila shaka alielewa vile Yesu alimpenda. Yesu anakupenda na anapenda kila mtu, hajjalishi tunaonekanaje au matatizo tulio nayo. Wacha tuimbe sifa kwa Bwana kwa furaha na tushukuru kwa upendo wake.

## Kukariri

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyta; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya!" (2 Wakorintho 5:17)

*Alituchakuga kufanya kazi yake:*



“....na sauti ikasikika kutoka hilo wingu: ‘Huyu ni Mwanangu mpPENDWA, ninayependezwa naye. Msikilizeni’” (Mathayo 17:5)

**Tunaweza  
kuwaombea watu  
walio wagonjwa**



# **UTANGULIZI – KITENGO CHA 4**

## **MPANGO WA WOKOVU**

---

**Marejeleo ya Kibiblia:** Luka 22:47-53; 63-71; Luka 23; 24:1-12, 36-53; Marko 16:15-16, 19-20

**Mstari wa Kumbukumbu wa Kitengo:** “Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisisi sote ni mashahidi wa tukio hilo.” (Matendo ya Mitume 2:32)

**Malengo ya Kitengo:**

**Kitengo hiki kitawasaidia watoto:**

- kujua kwamba Kristo alilipia adhabu ya dhambi zetu kwa kufa msalabani
- kuelewa jinis Yesu alifufuka kutoka kwa wafu
- kukubali kwa imani na shukrani kwamba Yesu ni Mwokozi wetu

**Masomo ya Kitengo:**

**Somo la 13: Yesu Alikufa kwa Ajili Yetu**

**Somo la 14: Yesu Alifufuliwa**

**Somo la 15: Yesu ni Mwokozi Wetu**

Watoto hawawezi kuelewa au hata kufikiria juu ya mtu kufa msalabani; si tamaduni ya ulimwengu tunayoishi. Unapoonyesha picha za kifo cha Yesu msalabani, eleza kwamba Yesu alikufa kwa njia hii ili kulipia adhabu ya dhambi zetu, nakwa hivyo unabii wa Agano la Kale wa kifo cha Yesu msalabani ulitimia.

Kifo cha Yesu, ambacho kilitokea zaidi ya miaka 2,000 iliyopita, kilituwezesha sisi waumini wote kwenda mbinguni. Mbinguni ni mahali patakatifu, bila dhambi yoyote. Wanadamu wote wametenda dhami na kwa hivyo, tukiwa bila Kristo, hatuwezi kuruhusia kuingia katika mbingu takatifu ya Mungu.

Dhambi hizo zinaweza kufutwa - kana kwamba hayajawahi kutokea, ikiwa adhabu imelipwa kwa dhambi ambazo tumefanya. Yesu anatupenda hivyo hivyo. Hakutaka sisi kupokea adhabu dhambi yetu ilistahili hivyo Yesu alichukua adhabu yetu mwenyewe; Alikufa msalabani.

Tunachotakiwa kufanya ni kumshukuru Yesu na kutoa maisha yetu kwake. Tumwambie Yesu tunasikitika sana kwa ajili ya dhambi zetu na kwamba hatutaki kuzitenda tena. Tumwambie Yesu kwamba tunataka kuishi pamoja Naye, hapa duniani, na mbinguni milele!

Hivi ndivyo Yesu alituokoa kutoka kwa dhambi zetu. Hii ndio maana tunamwita Yesu Mwokozi wetu.

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kujua kwa nini Yesu alikuja katika ulimwengu huu. Alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisi sote ni mashahidi wa tukio hilo.” (Matendo ya Mitume 2:32)

## Jitayarishe Kufundisha

Watoto wengine wanaweza kuhisi kupendwa na watu wazima walio karibu nao. Na waelewe kwamba Yesu aliwapenda sana hata alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zao. Waloweke watoto katika ukweli wa upendo wa Mungu. Mungu akusaidie kuwasiliana upendo wake bila masharti kwa kila mtoto. Somo hili litakupa nafasi ya kuwasaidia watoto kuelewa wazi zaidi kwamba Mungu ni upendo. Omnia kwamba watoto wamjibu yule anayewapenda zaidi; YESU.

**Kuanza Zoezi:** (T-A-F-U-T-A maneno ya Biblia)

**Kabla ya Darasa:** Andika herufi T-A-F-U-T-A.

**Sema:** Nitawapa dalili juu ya maneno yaliyo ndani ya Biblia na herufi ambayo jibu linaanza nayo. Je, unaweza kufikiria?

Kwa mfano:

T – Uasi kwa Mungu (DHAMBI)

A – Je, Yesu alikufa kwa ajil ya dhambi za nani?? (ZA WATU WOTE) F

– Je, nani anaweza kuokolewa? (WOTE)

U – Wakati mtu anainuliwa kutoka kwa wafu (KUFUFULIWA) T

– Yesu ali \_\_\_\_\_ msalabani (SULUBIWA)

A – Tukimuomba Yesu atusamehe, tutaenda huko siku moja (MBINGUNI)

Uliza: Je, ni maneno mangapi mapya ambayo umejifunza katika mchezo huu? Je, umesikia maneno hayo mbeleni? Je, yanamaanisha nini? Hadithi yetu ya Biblia leo ni juu ya maneno haya.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Yesu Alikufa Kwa Ajili Yetu

Wanaume wenyi silaha na marungu na mapanga walitokea ghafla. Aliyeongoza alikuwa Yuda, mmoja wa wanafunzi wa Yesu. Yuda kwa haraka alimwendea Yesu na akampa salamu za kawaida, za urafiki, na za heshima: busu kwenye shavu.

Kwa kusikitisha, Yesu alimwangalia mwanafunzi wake, “*Yuda, unamsaliti Mwana wa Adamu kupitia kwa busu?*”

Ghafla Petro alichukua silaha yake na kukata sikio la mtumishi wa kuhani mkuu.

“*Yatosha!*” Yesu alichukua sikio la yule mtu chini na akamponya.

Yesu aligeukia umati, “*Je! Ninaongoza uasi ambao umekuja na mapanga na marungu. Kila siku nilikuwa pamoja nanyi katika hekalu na hukuniweka mkono.*”

“*Twendeni!*” walipiga kelele walinzi wa hekalu. Kwa vurugu, walimchukua Yesu. Wanafunzi walikimbia kuokoa maisha yao. Usiku huo walinzi wa hekalu walimpiga Yesu kwa mjeledi mkali wa chuma. Walimfunika macho, wakacheka, wakamtukana, na kumwambia Yesu, “*Ewe, nabii! Tuambie ni nani aliyekupiga.*”

Wakampeleka Yesu mbele ya Pilato na alianza kumshtaki kwa uhalifu wote. “*Anasababisha shida katika nchi yetu,*” walisema. “...*Anakataza kutoa heshima kwa Kaisari, akisema kwamba Yeye ndiye Kristo, Mfalme.*” Pilato akamwuliza Yesu, “*Je, wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?*”

“*Umesema,*” Yesu alijibu.

Pilato alimwuliza maswali mengine kisha akageukia umati wa watu wenyenye hasira, “*Mtu huyu hajafanya kosa lolote. Nitampeleka Yesu kwa Herode. Anatawala mahali pa kuzaliwa kwa Yesu. Aamue kile atakachofanya na Yesu.*”

Yesu alipelekwa kwa Mfalme Herode. “*Fanya miujiza,*” Herode alimwambia Yesu. Yesu hakusema lolote. Kwa kumfanyia Yesu mzaha Herode alimvisha mavazi ya kifamle na wakamrudisha Yesu kwa Pilato.

Pilato aliwaeleza viongozi wa dini, “*Mtu huyu hastahili kifo kwa hivyo nitamweka huru baada ya kumuadhibu.*” Kila mwaka Pilato alimweka huru mhalifu; alitumaini Yesu angelikuwa huyo mhalifu. Lakini wote wakapiga kele pamoja: “*Tufungulie Baraba!*” (Baraba alikuwa mtu mbaya aliye kuwa gerezani kwa kusababisha maandamano.) Pilato aliwazungumzia tena akitaka kumweka Yesu huru; lakini walipiga kele zaidi wakisema, “*Msulubishe! Msulubishe!*”

“SAWA!” Pilato alisema. “*Mchukueni Yesu. Atapigwa na hatimaye mnaweza kufanya lolote mnalotaka na yeye. Nitamweka Baraba huru kama mlivyoomba.*”

Askari walimchukua Yesu, wakaweka msalaba mzito wa mba mgononi mwake, na kumpeleka mahali ambapo wahalifu wana sulubiwa. Yesu alikuwa mdhaifu sana na alijeruhwa hata asiweze kubeba msalaba wake. “*Wewe!*” askari walimwita mtu aliyesimama karibu. “*Beba ule msalaba hadi Golgotha.*”

Hatimaye walifika kwenye mlima wa kusulubiwa. Askari walipigilia mikono na miguu ya Yesu msalabani kisha wakatundika ishara iliyosema: “*HUYU NI MFALME WA WAYAHUDI*” Wezi wawili walisulubiwa wakati huo; mmoja kila upande wa Yesu. Yesu aliangalia umati, viongozi wa dini, askari, watu na akaomba akisema, “*Baba wasamehe kwa kuwa hawajui walitendalo.*”

Mmoja wa wezi alimfanyia Yesu mzaha akisema, “*Jiokoe mwenyewe, utuokoe nasi pia.*”

Mhalifu mwininge alisema, “*Wewe humwogopi Mungu, kwa vile wewe na mimi tunaenda kufa? Tunasekeka kwa sababu tunapokea adhabu ya matendo yetu mabaya; mtu huyu hakufanya chochote kibaya. Unikumbuke utakapoingia katika Ufalme Wako.*”

Kwa upendo Yesu alijibu, “*Nakwambia kwa haki, leo utakuwa pamoja nami peponi.*” Ilikuwa yapata saa tisa mchana Yesu alilia kwa sauti kubwa akisema, “*Baba, mikononi mwaka naiweka roho yangu.*” Kisha akufa. “*Hakika huyu alikuwa mtu mwema,*” Jemedari wa Rumi alisema kwa mshangao mkubwa.

Yusufu wa Arimathaya alienda kwa Pilato “*Tafadhali niruhusu nichukue mwili wa Yesu nikauzika.*”

“*Mchukue,*” Pilato alijibu.

Yusufu aliushusha mwili wa Yesu kutoka kwa msalaba na kuupeleka kaburini katika bustani. Kwa kujazwa na uchungu, Yusufu alikwenda nyumbani kuandaa manukato yaliyonukia vizuri ili kuyaweka kwa mwili wa Yesu. Rafiki yake alikuwa amekufa! Ilikuwa siku ya huzuni katika historia!

## Zoezi

Tazama Ukurasa wa Zozeli wa Somo la 13. Andika hatua za ABC ambazo mtu anafaa kuchukua ili kukubali msamaha wa dhambi zetu: 1) Kiri kwamba sisi ni wenyenye dhambi 2) Amini katika imani kwamba Yesu alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu 3) Mtangaze Yesu kama mwokozi, na uwaeleze wengine kwamba Yesu anasemehe dhambi zetu.

## Kukariri

“Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisisi sote ni mashahidi wa tukio hilo.” (Matendo ya Mitume 2:32) Andika mstari wa kukariri kwenye karatasi kubwa. Kata kila neno ili ziwe kando, kama vipande vyta fumbo kuweka pamoja. Soma aya ya kumbukumbu mara kadhaa. Changanya vipande vyta maneno. Ruhusu kila mtoto achukue neno.

Uliza: Je, ni nani aliye na kipande kilicho na neno, “Yesu”? Mtoto huyo aseme mstari na kuweka neno lao juu ya meza. Uliza: Ni nani aliye na kipande kilicho na neno “mashahidi”? Mtoto aseme mstari na aweke neno lao juu ya meza. Ukiendelea kila mtoto anastahili kuweka kipande chao cha kartani juu ya meza mahli sawa hadi mstari wote ukusanyiwe.

## Kufunga

Labda wengine wetu wanositikika kwa kumuasi Mungu na wanetaka kumuomba Yesu leo kuwa Mwokozi wao? Fungeni macho.

Imba ‘*Yote kwa Yesu.*’

Sema: Ikiwa unataka kumpokea Yesu kama Mwokozi wako inua mkono wako.

Ikiwa mtu ye yote anainua mkono wake muulize mmoja wa wasaidizi wako atunze watoto wengine. Nena na omnia na wale walioitikia. Ruhusu Mungu akuongoze katika kazi hii.

Wahimizie watoto waeleze hadithi ya Biblia kwa familia yao.


## Zoezi la 13

### **YESU ALIKUFA KWA AJILI YETU**

**Maandiko:** Luka 22:47-53, 63-71; Luka 23

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwa nini Yesu alikuja Ulimwenguni. Alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisi sote ni mashahidi wa tukio hilo.” (Matendo ya Mitume 2:32)



*Yesu anaweza kuwa Mwokozi wako*



Yesu alikuja msalabani kwa ajili ya watu wote. Alikuwa kwa ajili yako. Je, umemwomba Yesu akusamehe dhambi zako na kuwa Mwokozi wake. Hivi ndivyo unavyofanya.

KUBALI

AMINI

KIRI

kwamba umetenda dhambi,  
(umefanya makosa, umemuasi Mungu).  
Mwambie Mungu yale umetenda,  
sikitika kwa ajili yake na uwe tayari kuacha.  
**(Warumi 3:23; 1 Yohana 1:9)**

kwamba Mungu anakupenda. Alimtuma  
Mwanawe, Yesu, akuokoe kutoka kwa  
dhambi zako. Muombe Mungu akusamehe  
na kisha upokee msamaha wake.  
**(Yohana 3:16; Matendo ya Mitume 16:31)**

Yesu kama Mwokozi Wako.  
Waeleze wengine yale Mungu amekutendea.  
Mpende Mungu na umfuate Yesu.

**(Yohana 1:12; Warumi 10:13)**

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Yesu alikufa, akazikwa na Mungu akamfufua. Tunamsherehekeea wakati wa Pasaka.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisi sote ni mashahidi wa tukio hilo.” (Matendo ya Mitume 2:32)

**Jitayarishe Kufundisha**

Je, ni nini huja kwa akili na mawazo ya watoto wakati wa Pasaka? Je, ni ukweli na kufurahisha kiasi gani ambao tunaweza kufanya ufufuo kwa watoto ambao akili zao zimeelekezwa kwenye sherehe? Hatuna jibu nzuri. Watoto hawatuonyeshi mara moja wakati ukweli wa kiroho unakuja kwao. Mara nyingi walimu hawaelewi ishara wanazotutumia.

Kama waalimu hatuna jukumu la kuwashawishi watoto wa ukweli wa Biblia; hiyo ni kazi ya Roho Mtakatifu. Lengo letu ni kuwasilisha ukweli kwa uaminifu na kwa njia bora zaidi, basi amini kwamba Roho atawasaidia kuitumia.

“Unawafundisha” wanafunzi wako kwa kuangazia maisha yako na kile unachosema kwa maneno yako. Kwa njia ile ile ambayo unazungumza juu ya ufufuo, utawasilisha ukweli wa uwazi huu kwao. Ikiwa unapokea au hupokei dalili yoyote kutoka kwa watoto, wafundishe somo hili kwa ujasiri. Kwa wakati wake Mungu atafanya ukweli wa ufufuo kuwa wazi kwa watoto.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Yesu Alifufuliwa!**

“Siamini!” Maria Magdalena aliwaambia marafiki wake. “Ni kama ndoto.”

“Najua,” mwengine alisma. “Je, ni kwa nini walimwua Yesu katika njia hiyo mbaya?”

Ilikuwa Jumapili asubuhi. Maria Magdalena, Mariamu mama wa Yakobo, na wanawake wengine waliompenda Yesu walienda kaburini. Walitaka kukamilisha maelezo yote maalum ambayo watu walitekeleza kwa mpenda wao aliyekufa. Wanawake walibeba mitungi iliyoja manukato na marashi nyingi. Wangeweka manukato katika mikunjo ya shuka iliyo funika mwili wa Yesu. Wakati wanawake walitembea, walisemezana. “Je, tutaingaje ndani ya kaburi la Yesu?” mmoja wao aliuliza. “Hilo ni swali nzuri sana” mwengine alijibu.

“Wako sawa!” wa tatu alisema. “Viongozi wa hekaly waliweka jiwe kubwa kwenye lango la kaburi na kuliweka mhuri. Na sasa walinzi walilinda. Labda ni kwa sababu walinzi hao hao pengine watatusaidia kuliondoa jiwe.”

“Tazama!” mwanamke mmoja alilia. “Jiwe limeondolewa. Kaburi liko wazi!” Haraka, mwanamke alingia kaburini. Mwili wa Yesu haukuwepo!

“Mwili wa Yesu uko wapi?” waliulizana. “Ni nini kilitendeka? Je, ni nani anayeweza kuwa ameuchukua?” Wakati huo, wanawake waliwaona watu wawili wakisimama karibu nao. Lakini hawa hawakuwa watu wa kawaida. Mavazi yao yaling’ a kama umeme. Walikuwa malaika.

Wanawake walipiga magoti, wakiwa na uoga.

“Kwa nini wanatafuta walio hai kati ya wafu? Malaika waliuliza. “Yuko hapa, amefufuka. Hamkumbuki yale Yesu alisema kabla hajafa? Aliwaambia atasulubiwa na maadui wake, lakini siku ya tatu atafufuliwa.”

Malaika alipozungumza wanawake walianza kumkumbuka Yesu. Kwa shauku, walikimbilia mahali

ambapo wanafunzi wa Yesu walikuwa. "Jiwe lilikuwa limeondolea, kaburi la Yesu lilikuwa tupu!" walisema kwa furaha.

"Malaika wawili walitwambia kwamba Yesu yu hai, kama tu vile alivyokuwa ametueleza!"

"Hiyo haina maana!" wanafunzi walisema. Walikuwa wamemwona Yesu akifa kwa uchungu msalabani. Walimna Yusufu Mwaramathiya akiweka mwili wa Yesu kaburini. Hawakukumbuka maneno ya Yesu juu ya kufufuka kwake. Hawakuwaamini wanawake.

Petro alitaka ku{jonea mwanyewe. Alikimbia kaburini. Aliinama, akatazama kaburi lililokuwa tupu, na kuona shuka zilizokuwa bure ambazo zilikuwa zimetumika kufunga mwili wa Yesu. Petro aliondoka mahali hapo na kurudi mahali wanafunzi wengine walikuwa. "Je, nini kilitendeka?" alijiuliza. "Je, yawezekana kwamba Yesu yu hai?"

**Uliza:** Ni muujiza gani amba Mungu alifanya asubuhi ya Pasaka? (Alimfanya Yesu aishi tena.) Je, ni nani aliyeamini Habari Njema ya kwamba Yesu alikuwa amefufuka? (Mwanzioni hakuna aliyeamini, baadaye wanawake waliamini.) Je, unafikiri ni kwa nini hadithi ya ufufuo ni muhimu zaidi kwa Ukristo?

Sema: Hadithi ya leo ni hadithi nzuri sana katika Biblia nzima. Ukristo ni dini ya pekee ambayo kiongozi wake, Yesu, alifufuka kutoka kwa wafu na leo anaishi mbinguni. Kwa vile Yesu alifufuliwa sisi Wakrist tunajua kwamba nguvu za Mungu ni kuu zaidi ya nguvu zingine. Wakristo wanajua kwamba wakati tunakufa tutaishi tena na tutakuwa pamoja na Mungu na Yesu mbinguni. Hii ni Habari Njema ya Ufufuo!

## Zoezi

### Tunakumbuka Kaburi Lililo Tupu (igizo)

Waigizaji: wanawake 3, Petro, askari watatu au wanne, malaika wawili, wanafunzi kadhaa.

Andaa mapema mazungumzo mafupi kati ya wahusika ili kuigiza siku ya ufufuo. Tumia ubunifu wako kubuni kaburi na jiwe limeondolewa.

### Mshawishi Petro

Sema: Wacha tujifanye kwamba tunakutana na Petro wakati anarudi kutoka kwenye kaburi tupu. Petro amechanganyikiwa na yale ameyaona. Je, tutamwambia nini Petro ili kumsaidia ajue na kuamini katika habari njema kwamba Yesu yu hai? Je, tutamshawishije?

Chagua mtotoacheze jukumu la Petro na darasa lote,kwa shauku, mpe habari njema na ujaribu kumshawishi kwamba ni ya kweli. Peter atalamika na kusema kwamba anachoambiwa ni cha uongo. Mwishowe mtoto anawenza kuonekana ambaye anacheza Yesu, wote wamevaa mavazi meupe, amba humsalimu Petro na wale wote waliokusanyika.

## Kukariri

"Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisi sote ni mashahidi wa tukio hilo." (Matendo ya Mitume 2:32)

Andika mstari wa kumbukumbu na maneno yakiwa yamechanganywa. Kwa mfano: "Mungu, sisi sote ni mashahidi, Yesu..." Kisha waambie watoto waende mmoja baada ya mwingine waandike kwenye ubao mstari na maneno katika utaratibu sawa.

## Kufunga

Hakikisha watoto waelewa maana ya ukweli ya ufufo. Mshukuru Mungu kwa ufufuo wa Yesu. Wafundishe mazungumzo haya kama salamu ya Pasaka au Ufufuo:

Mwalimu: Bwana amefufuka!

Watoto: Hakika amefufuka!

Mwambie kila mtoto aseme kwaheri kwa wenzao kwa salamu hizo.


## **Zoezi la 14**

# **YESU ALIFUFULIWA!**

**Maandiko:** Luka 24:1-12

**Lengo la Somo:** Waaide wanafunzi kujua kwamba Yesu alikufa, akazikwa na Mungu akamfufua. Tunamsherehekea wakati wa Pasaka.

**Memory Verse:** “Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisi sote ni mashahidi wa tukio hilo.”  
(Matendo ya Mitume 2:32)



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi wajue kwamba wanafunzi wa Yesu walimwona akirudi mbinguni baada ya Mungu kumfufua kutoka kwa wafu.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisisote ni mashahidi wa tukio hilo.” (Matendo ya Mitume 2:32)

**Jitayarische Kufundisha**

- Andaa mapema vifaa vyovyyote vya mafundisho ambavyo utahitaji kwa somo hili.
- Kumbuka kurekodi mahudhurio, kuchukua sadaka, kukaribisha wageni na kukusanya habari za familia zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Wanafunzi walikusanyika pamoja katika chumba. Injili ya Yohana inatueleza kwamba walikuwa mahali ambapo milango ilikuwa imefungwa (Yohana 20:19)  
Je, Yesu ni nani?

**Hadithi ya Biblia****Yesu Yu hai!**

Mara tu wawili wa wafuasi wa Yesu kutoka Emau walikimbia chumbani na kusema kwa mshangao, “Yesu yu hai! Ametembea nasi hadi Emau, lakini hatukujua alikuwa nani. Tulimwalika kula chakula cha jioni na sisi. Tulimwomba aombe na alipoanza kuomba, mwishowe tulimtambua. Yesu yu hai!” Baadhi ya wanafunzi katika chumba hicho waliitikia, “Hiyo haiwezekani. Yesu alikufa. Tulimwona kwa macho yetu akifa. Watu hawafufuki baada ya kufa kwa siku tatu!” wengine walisema. “Lakini ni kweli,” Watu hao wawili walisisitiza.

Walipokuwa wakizungumza Yesu aliwatokea. “Amani na iwe nanyi,” alisema.

“Ni roho!” mtu alisema. Kila mtu alitetemeka kwa uoga.

“Kwa nini una wasiwasi na kwanini mashaka huja akilini mwako?” Yesu aliuliza. “Tazama mikon na miguu yangu. Ni mimi; niguse uone.”

Sasa wanafunzi walilazimika kuamini Habari Njema. Hakuwa jini. Alikuwa Yesu na hakika alikuwa amefufuka!

Siku moja Yesu aliwaongoza wote mahali maalum kwenye Mlima wa Mizeituni. Akiinua mikono yake, Yesu aliomba baraka za Baba. Alipokuwa akinena Yesu alianza kupaa mbinguni. In a few moments He disappeared. The disciples never saw Jesus again on this earth.

Je, walikuwa na huzuni? Labda kidogo; katika njia hiyo jambo hilo hutendeka kwetu wakati mtu tunayempenda anaondoka. Lakini wanafunzi pia walikuwa wamejawa na furaha. Yesu yu hai!

Punde tu Yesu angemtuma Roho Mtakatifu kuwa nao wakati wote. Lililokua muhimu zaidi ni kwamba wanafunzi walikuwa na kazi ya kufanya. Wanafunzi walipaswa kumwambia kila mtu kwamba Yesu yu hai na na kwamba angewasamehe dhambi zao zote ikiwa wangemwomba.

**Zoezi**

Wagawanye watoto katika vikundi viwili; kundi A na Kundi B  
Kutoka kwa Luka 24:1-12 From Luke 24:1-12 waulize maswali yafuatayo kwa mpangilio mbadala:  
A – Je, ni nini kilijaza mawazo ya wanafunzi waliposikia kwamba Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu? (hofu, mshtuko)  
B - Je! Wanafunzi walikuwa na huzuni kwa sababu Yesu alikuwa amekufa? (Ndio)  
A – Je, wanafunzi walikuwa na huzuni kwa sababu mwili wa Yesu ulikuwa umeibiwa? (Ndio)  
B – Je, ni kweli kwamba wanawake waliamini Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu lakini wanafunzi hawakuamini? (Ndio)  
A – Je, ni uongo kwamba hakuna mtu aliyeamini Yesu alikuwa amefufuka? (Ndio)  
B – Je, ni wanawake wangali ambao walienda kaburini? (hatujui)  
A – Je, kulikuwa na jiwe kubwa ambalo lilifunika kaburi? (ndio)  
B – Je, ni watu wangapi waliokuwa pale katika mavazi yaliyong’aa” (wawili)  
A – Je, wanawake walienda kaburini saa tisa mchana? (hapana, asubuhi mapema)  
B – Baadaye, ni nani walikimbia kaburnini kutazama? (Petro)  
Timu itakayojibu maswali mengi ndiyo itashinda.

### Kukariri

“*Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisis sote ni mashahidi wa tukio hilo.*” (Matendo ya Mitume 2:32)

Andika mstari huu juu ya kadi ndogo zilizokatwa; kila neno kwenye kadi yake. Changanya kadi na usambaze moja kwa kila mtoto kwa watoto 14 (weka pamoja na kumbukumbu). Haya! TWENDE! Tazama jinsi watoto wanavyowenza kujipanga kwa usahihi wenyewe.

### Kufunga

Omba pamoja na watoto watumaini na kuamini kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Yesu YU HAI! Ombea watu walio wagonjwa au mtu ye yeyote aliye na tatizo nyumbani. Ombea kila mmoja. Watie watoto moyo waeleze hadithi ya leo ya Biblia kwa wazazi wao, ndugu/dada, na marafiki.

## Zoezi la 15

### YESU YU HAI!

**Maandiko:** Luka 24:36-53

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi wajue kwamba wanafunzi wa Yesu walimwona akirudi mbinguni baada ya Mungu kumfufua kutoka kwa wafu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisis sote ni mashahidi wa tukio hilo.” (Matendo ya Mitume 2:32)

Chapisha ukurasa huu. Kata picha ya Yesu aliyefufuka.  
Weka picha iwe imesimama mbele ya wanafunzi hapo chini.



**“Basi Mungu alimfufua huyo Yesu na sisis sote ni mashahidi wa tukio hilo.”**  
**(Matendo ya Mitume 2:32)**

Onyesha picha hii ili wote waone.

# **UTANGULIZI – KITENGO CHA 5**

## **SHERIA KUMI MUHIMU ZAIDI**

---

**Marejeleo ya Kibiblia:** Kutoka 19:1-20, 21, 24:12-18, 32:1-33:6, 34:1-14; 1 Samweli 17:12-20, 22:1-4, 24; Mathayo 5:21-22, 43-45; 1 Wafalme 21:1-29; 2 Wafalme 5:13-27.

### **Mstari wa Kumbukumbu wa Kitengo:**

*Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)*

### **Malengo ya Kitengo**

#### **Kitengo hiki kitawasaidia watoto**

- Kujuu sheria ambazo Mungu alituachia ili tuishi maisha ya hekima
- Kulinda mawazo yao
- Kuheshimu na kuwapenda wazazi wao
- Kujuu kwamba udanganying huleta matokeo mabaya
- Kuelewa kwamba ni lazima Mungu awe katika nafasi ya kwanza kila wakati

#### **Masomo ya Kitengo**

**Somo la 16: Sheria za Kuishi na Hekima**

**Somo la 17: Ni lazima Mungu awe katika Nafasi ya Kwanza**

**Somo la 18: Kuwaheshimu Wazazi Wetu**

**Somo la 19: Linda Mawazo Yako**

**Somo la 20: Kuiba na kudanya Huleta Matokeo Mabaya**

**Somo la 21: Ulafi ni Hatari**

Kila mtoto mdogo anahitaji kushika kwamba Biblia ni kitabu cha kufuata. Si hadithi tu inayozungumza juu ya Mungu aliyeishi miaka elfu iliyopita na kuacha tu kitabu kikubwa na kigumu kuelewa.

Wasaidie watoto kuona kwamba Amri 10 si sheria za kuzuia uhuru wetu na hata furaha yetu. Sheria za Mungu ni za kutusaidia kuepuka mateso na kutusaidia kuishi kwa amani na utulivu.

Gharama ambayo wale wanakiuka amri za Mungu wanastahili kulipa ni kutenganishwa milele na Mungu.

## Lengo la Somo

Kuwasaidia wanafunzi kutambua umuhimu wa kutii Amri kumi za Mungu.

## Mstari wa Kumbukumbu

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

## Jitayarisha Kufundisha

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kulitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Wazazi wanazo sheria za kutii. Kwa sheria hizi Kwa sheria hizi tutaishi salama zaidi na kujifunza zaidi juu ya maisha. Mungu ana sheria 10 muhimu ambazo anatarajia sisi tutii kwa sababu zinatusaidia kujua jinsi anavyotaka watu wake waishi. Hadithi ya leo ya Biblia ni juu ya sheria hizi 10 muhimu – Amri Kumi.

**Amri Kumi za Bwana (Kutoka 20:1-17)**

Waisraeli waliona mlima mbele yao; ilikuwa kubwa! Wamesafiri miezi tatu yote. “Wekeni kambi hapa,” Musa alisema. “Tunakaa kwa muda.”

Wakati watu walipiga kambi chini ya mlima, Musa alizungumza na Mungu mlimani. Mungu aliwakumbusha watu jinsi alivyowaongoza wote. Musa alirudi kwenye kambi na akawaambia kile Mungu alikuwa amemwambia. Watu wakajibu, “Tutafanya kila kitu ambacho Yehova ametueleza.” Musa alirudi mlimani na akamwambia Mungu, “Watu wameahidi kutii.”

Mungu alisema, “Waeleze wajiandae. Leo na kesho waoge na wavae mavazi yao. Siku ya tatu nitarudi kusema na nanyi. Watu watasikia na watajua kwamba wanaweza kukuamini wewe kama kiongozi wao kwa sababu nimekuchagua. Hakikisha wanakaa mbali na mlima kwa sababu ni takatifu. Hawawezi kuugusa.

Musa na watu walimtii Mungu na kijiandaa. Siku ya tatu, kulikuwa na radi na umeme juu ya mlima. Kulikuwa na wingu zito, moshi, moto, na kelele kubwa. Mungu alikuwepo na watu waliogopa! Kila mtu kambini alitetemeka. Musa aliwatoa watu kwenye kambi ili wakutane na Mungu na wakasimama chini ya mlima. Musa alipanda mlimani kukutana na Mungu. Watu walipokuwa wakisubiri Mungu alinena na Musa.

Mungu alimpa Musa sheria kumi muhimu sana za watu kutimiza. Tunaita sheria hizi Amri Kumi ambazo Mungu angeonyesha watu wake vile wanaweza kuishi.

Amri za kwanza nne zinaonyesha watu jinsi ya kumtukuza na kumheshimu Mungu:

“Msiwe na miungu ingine mbele yangu.” Watu wa Mungu hawapendi au kuabudu mtu mwengine ila Yeye. Watakiwa kumweka Mungu mbele.

“Usijifanyie sanamu ya miungu wala kuiabudu.” Mungu aliwaambia watu wake wasitengeze picha au sanamu za kuabudu.

“Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako.” Watu wa Mungu walitakiwa kutumia jina la Mungu kwa njia tu iliyoonyesha upendo na heshima Kwake.

“Ikumbukeni siku ya Sabato na kuitakasa.” Siku ya Sabato ni siku maalum ya Bwana. Watu walitaiwa kumweka Mungu mbele, kutumia siku hiyo na kupumzika.

Amri kumi zifuatazo ziliwangundisha jinisi ya kuwatendea wengine:

“Waheshimu baba yako na mama yako.” Mungu aliwataka watu ku waheshimu na kuwati wazazi wao.

“Usiue watu wengine.”

“Usizini.” Watu wa Mungu wanastahili kutunza ahadi zao za ndoa. Kwa hivyo, mwanamke aliyeolewa hafai kuwa na uhusiano na mtu mwingine. Katika hali hiyo, mwanaume ailiyeoa asiwe na uhusiano na mwanamke ambaye si mke wake.

“Usiibe.”

“Usimshuhudie jirani yako uongo.”

“Usiitamani nyumba ya jirani yako.” Yesu hakuwataka watu wake kutamani vitu ambavyo vilikuwa vya watu wengine.

Amri Kumi zingewasaidia Waisraeli kuishi kama watu maalum wa Mungu. Hizi ni njia kumi nzuri za kumpenda na kumtii Mungu.

### Zoezi

Je, sheria ni za nini?

Waulize watoto kujiunga nawe kwa kuketi au kusimama kwa mviringo.

Peana jiwe ndogo kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Unaposema “Amri Kumi”, mtoto aliye na jiwe mkononi mwake ataacha kulipitisha na kueleza sheria iliyo nyumbani kwao.

Uliza: Kwa nini unafikiria baba yako (au mama, au wazai wako, kulingana na vile hali inavyoweza kuwa) wanafanya sheria hiyo?

Endelea na mchezo ukiruhusu kila mtoto achukue nafasi akishika jiwe na kuzungumza juu ya sheria nyumbani mwao..

### Kukariri

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

Waambie watoto washike vipande vya karatasi vilivyo na maneno yaliyo na mstari wa kumbukumbu. Wainue karatasi ili kila mtu aweza kuyaona. Rudia hadi kila mtu aweza kusema mstari wa kumbukumbu bila kuangalia.

### Kufunga

Waombee watoto watii amri kumi, hasa zile wanazungumza nazo.

## **Zoezi la 16**

### **SHERIA ZA KUISHI NA HEKIMA**

**Maandiko:** Kutoka 20:1-17

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kutambua umuhimu wa kutii Amri Kumi.

**Mstari wa Kumbukumbu:** Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifluta amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)



- I – Mweke Mungu Mbele
- II – Mpende Mungu Peke Yake
- III – Usilitumie Jina la Mungu Vibaya
- IV – Ikumbuke Siku ya Sabato na Kuitakasa
- V – Waheshimu Wazazi Wako
- VI – Usiue
- VII – Usizini
- VIII – Usiibe
- IX – Usidanganye
- X – Usitamani Kitu Kisicho Chako

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kama kuna vitu katika maisha yao ambavyo ni muhimu kuliko Mungu? Ni lazima Mungu awe katika nafasi ya kwanza!

**Mstari wa Kumbukumbu**

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

**Jitayarisha Kufundisha**

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kulitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Kutoka 20:1-6 – Utamchagua Mungu au ndama dhahabu?**

“Tutafanya yote Bwana ametuamrisha. Tutamtii.” ilikuwa ahadi watu walifanya kwa Mungu baada ya Yeye kusema nao kupitia Musa. Walisahau ahadi hiyo kwa haraka sana.

Mungu alimwambia Musa, “Nenda mlimani ukutane nami hapo. Nitakupa mawe yaliyo na sheria iliyoadikwa juu yake.” Mungu alikuwa anawapa watu Amri Kumi kwa sababu aliwapenda. Alijua kwamba wakitii sheria zake, watakuwa watakatifu, watakuwa na furaha, na watamtukuzwa kwa tabia zao.

Musa alisema na watu, “Kwa kukosa kwangu ndugu yangu Haruni na wasaidizi wake watasimamia kila kitu. Mkiwa na shida, mpelekee.”

Musa alipanda mlimani kukutana na Mungu na kubaki pale kwa siku arobaini usiku na mchana. Mungu alimpa Musa mawe ambayo alikuwa ameandika Amri Kumi. Mungu pia alimpa maagizo ingine muhimu.

Katika kambi, mwanzo kila kitu kilionekana sawa. Watu walianza kuwa na wasiwasi baada ya muda. Walipotazama mlimani kile waliona ni moshi na moto. Mwishowe, watu walimwendea Haruni na kumwambia, “Tafadhali tufanyieni miungu ambayo itakuwa pamoja nasi na kutuongoza. Musa alituondo Misri lakini sasa hatujui kilichomtendeka.”

Haruni alichoka na kulia sana na malalamiko mengi. Kazi yake ilikuwa kufundisha watu kumwabudu Mungu wa pekee wa kweli, & yeye tu. Sasa hakuwa na ujasiri wa kutii. “Nileteeni vipuli vyenu vya dhahabu.” aliwaambia Waisraeli.

Harun aliyeusha dhahabu yao na kuifanya kwa umbo la ndama mzuri, “Israeli, mungu wenu aliyeaondoa Misri ndio huyu.”

Waisraeli walipenda ndama huyo wa dhahabu anayeng'aa. Walipoitazama walihisi kana kwamba Mungu mwenyewe yuko pamoja nao na sio mbali juu ya kilele cha mlima. Haruni pia alijenga madhabahu ya ndama wa dhahabu.

Haruni aliwaambia, “Kesho tutakuwa na sherehe kubwa na tutamuabudu Mungu.”

Siku iliyofuata mji ulichoma sadaka kwa heshima ya ndama wa dhahabu. Waliiabudu kana kwamba ilikuwa Mungu na wakaanza kusherekeea. Walikula, wakakunywa, walicheza na kuimba. Wasahau kumtii Bwana na kuanza kuasi. Mungu alijua kile walichokuwa wakifanya. Alikasirika! Mungu aliwapenda watu sana lakini walikuwa wanaharibu mipango yote mizuri alikuwa nayo kwao.

Mungu alisema na Musa, "Watu hawa ni wagumu na hawaiiitii mimi. Nitawaangamiza kabisa." "Hapana Mungu wangu, tafadhali usifanye hivyo!" Musa aliomba. Uliwaondoa watu hawa kutoka Misri na ukiwaharibu sasa Wamisri watasema kwamba wewe ni mwovu. Tafadhali wasamehe watu." Mungu alimjibu, "Sawa, Sitawaharibu kabisa."

Musa akashuka haraka kutoka mlimani. Wakati huu Musa alikuwa tayari amesikia michafuko. Aliona ndama wa dhahabu ambayo watu waliabudu na akajawa na hasira. Musa alirusha mawe chini na ndama wa dhahabu ndani ya moto. "Yule aliye upande wa Mungu, ajiunge pamoja nami!" Musa alilia.

Watu wengine walimkaribia Musa.

Siku iliyofuata Musa aliwaambia watu, "Mmetenda dhambi kubwa sana na nitarudi mlimani mahali Mungu yuko. Pengine nitaweza kumshawishi awasamehe maovu yenu."

Watu waliskitika kile walichokitenda; walilia, wakachukua nguo zao nzuri na vito vya kujitia kuonyesha jinsi walivyohisi vibaya. Mungu aliwasamehe watu ingawa alilazimika pia awaadhibu kwa dhambi zao. Mungu alimwambia Musa arudi mlimani na Mungu mwenyewe aliandika Amri Kumi katika mawe mengine mawili. Mungu alifanya kitu cha ajabu: Mungu alikuja karibu na Musa ili Musa aweze kumuona Mungu, hata angalau kidogo tu.

"Mimi ni Yehova," Mungu alimwambia Musa. "Mimi ni Mungu wa mtakatifu mwenye huruma, mwelesi wa hasira na mwangi wa rehema na kweli ... anayesamehe dhambi."

Mungu alifanya ahadi na Musa: "Nitafanya maajabu ambayo haijafanywa duniani kote, lakini wewe na watu lazima mnitii. Msiiinamie miungu ingine bali mimi peke yangu!"

### Zoezi

Andaa kadi mbili na neno moja kwa kila kadi:

- Kadi zingine za mstari wa kumbukumbu
- Kadi zingine za amri ya 1 na ya 2

Tengeneza timu mbili. Gawa kazi hizo kwa kila kikundi.

Kwa kusaidiana, timu mbili zitakusanya mstari wa Biblia au amri kwa kuweka kila neno katika sehemu yake sawa. Kundi litakalokamilisha kwanza litashinda.

Pindua kadi zikiangalia chini juu ya meza, rudia mstari wa kumbukumbu na amri kama kundi. Vikundi vinaweza kubalishana kadi ili watoto wote wajifunze mstari na amri mbili.

### Kukariri

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

Wambie watoto waandike mstari kwenye kipande cha karatasi. Bandika karatasi hizo kwenye ukuta kwa kila mtu kuona.

### Kufunga

Omba na watoto, ukimwuliza Mungu awasaidie wakati wa wiki, wakimpa nafasi ya kwanza katika shughuli zao zote na kila mahali.

## Zoezi la 17

### **NI LAZIMA MUNGU AWE KATIKA NAFASI YA KWANZA**

**Maandiko:** Kutoka 20:1-6

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kama kuna mambo katika maisha yetu yaliyo muhimu kuliko Mungu? Ni lazima Mungu awe katika nafasi ya kwanza!

**Mstari wa Kumbukumbu:** Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkiziflata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

#### **Njia 10 za Kumweka Mungu Mbele:**

1. Sema na Mungu Kila Siku.
2. Muombe Yesu awe Mwokozi Wako.
3. Mwambie Mungu unapenda
4. Tii Amri 10 za Mungu na ufanye mambo ambayo unajua Mungu anataka ufanye
5. Msifu Mungu mahali popote uko
6. Mtolee Mungu Sadaka zako
7. Waonyeshe wengine upendo
8. Jifunze kile Biblia inasema
9. Kuwa tayari kufanya lile Mungu anakuomba ufanye, Hata kama linaonekana ngumu kulifanya
10. Wazungumzie marafiki wako juu ya Mungu na Kanisa

#### **Njia 10 za Kumweka Mungu Mbele:**

1. Sema na Mungu Kila Siku.
2. Muombe Yesu awe Mwokozi Wako.
3. Mwambie Mungu unapenda
4. Tii Amri 10 za Mungu na ufanye mambo ambayo unajua Mungu anataka ufanye
5. Msifu Mungu mahali popote uko
6. Mtolee Mungu Sadaka zako
7. Waonyeshe wengine upendo
8. Jifunze kile Biblia inasema
9. Kuwa tayari kufanya lile Mungu anakuomba ufanye, Hata kama linaonekana ngumu kulifanya
10. Wazungumzie marafiki wako juu ya Mungu na Kanisa

Tumia penseli za rangi kuandika sentensi zifuatazo upande wote wa karatasi nzito. Rembesha karatasi katika njia yako bora na uitumie kama usaidizi wa kurasa za Biblia. Ibebe nawe Jumapili ijayo kanisani.

## Lengo la Somo

Kuwasaidia wanafunzi kuwa na motisha ya mfano wa Daudi wa utiifu kwa wazazi, kuwa tayari kuwashemtu wazazi wao, kuwatendea vile Mungu alivyoamuru.

## Mstari wa Kumbukumbu

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifua amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

## Jitayariske Kufundisha

Neno “tukuza” linahusisha kuthamini, kuheshimu, kusikiliza, kuwa na haja na, na kuwatii wazazo wetu. Waonyeshe watoto maana ya kuwatukuza na kuwashemtu wazazi kwa kuwa mfano mwema kutoka kwa maisha yako. Waeleze juu mafundisho ambayo umeokea kutoka kwa wazazi wako na ueleze jinis umewaheshimu.

Watoto watajifunza sio tu kutoka kwa maneno yako bali kupitia kwa mfano wako.

Kuna watoto amba wazazi wao hawawezi kustahili kuheshimiwa. Baadhi ya watoto wako wanaweza kuwa walikuwa wahanga wa kunyanyaswa na wazazi wao. Omba hasa kwa ajili ya watoto wao. Ikiwa unashuku kuwa wanateseka, zungumza na mchungaji wako.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kulitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.

Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

## Utiifu 1 Samweli 17: 12-20

Ndugu zake Daudi watatu walikuwa askari katika jeshi la Mfalme Sauli akipigana juu ya Jeshi la Wafiliki. Wafiliki walikuwa na nguvu sana, maadui wabaya; mambo yalikuwa hayaendi vizuri kwa jeshi la Sauli. Adui alikuwa na askari ambaye alikuwa jitu lililoitwa Goliati. Hakuna aliyweweza kumpinga Goliati. Kwa siku arobaini majeshi hayo mawili walibaki mahali walikuwa na wala hawakupigana. Wakati huo hakukuwa na redio wala televisheni za watu kutafuta kilichokuwa kinafatendeka vitani. Njia peke yake ya kuja kama askari walikuwa salama ilikuwa ni kwenda mahali jeshi lilikuwa ili kuwaona. Mara nyingi viongozi wa jeshi hawakuwa na chakula cha kutosha cha kuwapa askari, hivyo familia walilazimika kuleta chakula.

Daudi, mwanawe Yese mdogo, alikuwa mchungani wa kondoo wa babake karibu na Bethlehemu. Yese alimtuma Daudi aende pamoja naye. Daudi alipowasili babake alimwambia, “Wapelekee ndugu zako nafaka hii iliyochoomba pamoja na hii mikate kumi. Peleka kwenye kambi mara moja. Peleka vipande hivi viwili vya jibini vya kitengo chao. Uangalie kama ndugu zako wako salama na utuletee neno kutoka kwao.”

“Ndio, baba,” Daudi alijibu. “Nitaenda asubuhi mapema.” Siku iliyofuata, Daudi alitii kila kitu ambacho babake alimwambia afanye. Alimtafuta mtu achukue nafasi yake ya kuchunga kondoo alipokuwa ameenda. Kisha Daudi alipeleka chakula na akaenda katika kambi ya jeshi la Sauli. Wakati Daudi aliwapata ndugu zake, aliwapa chakula na akawauliza jinsi walivyoendelea. Ni wakati huu wa

matembezi haya ambayo Daudi alimwua Goliati. Baadaye Daudi alirudi nyumbani na habari njema kwa babake.

Miaka nyingi ilipita na Daudi alikua. Wakati huo wote alimtii Mungu na wazazi wake. Mungu alipendezwa sana na Daudi.

### Zoezi

Tengeneza seti 2 za kadi 10. Andika juu ya kila mmoja wao Amri 10. Changanya kila seti ya kadi na uziweke chini.

Gawanya wanafunzi katika timu mbili na ipe kila timu seti yao ya kadi 10 za Amri. Kuwa na mbio ili uone ni timu gani inaweza:

- kuweka kadi zao kwa mpangilio sahihi (kulingana na Kutoka 20)
- Weka kadi katika utaratibu wa ABC

### Kukariri

*Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)*

Andika mstari wa kumbukumbu, lakini acha nafasi tupu za maneno mengine.

Acha watoto wajaze nafasi zilizo wazi wakati wanasoma aya hiyo kwa sauti.

Rudia mstari pamoja nao hadi waweze kusema kwa sauti bila msaada

### Kufunga

Wakusanye watoto pamoja ili kuomba.

Si rahisi kila wakati kuwashemimu na kuwatii wazazi, lakini Mungu anaweza kutusaidia kila wakati. Kama umeamua kuwashemimu wazazi wako zaidi, muombe Bwana akusaidie kutimiza ahadi yako. Ni vizuri kuwashemimu wazazi wetu!


## Zoezi la 18

### KUWAHESHIMU WAZAZI WETU

**Maandiko:** Kutoka 20:12; 1 Samweli 17:12-20, 22:1-4

**Lengo la Somo:** Kuwasaidia wanafunzi kuwa na motisha ya mfano wa Daudi wa utiifu kwa wazazi, kuwa tayari kuwasheshimu wazazi wao, kuwatendea vile Mungu alivyoamuru.

**Mstari wa Kumbukumbu:** Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifua amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)



Chora picha ya familia yako. Iweke kwenye fremu ili tupu hapo juu.  
Mfano uko hapa chini.



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa jinsi ilivyo muhimu kusamehe.

**Mstari wa Kumbukumbu**

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

**Jitayariske Kufundisha**

Watoto wanahitaji msaada katika kujua jinsi wanastahili kukabiliana na hisia kama hasira. Watoto wa vita wanakutana na mambo kwa mtando yanayoweza kuwafanya wasiwe na hisia. Mungu wetu mwenye upendo anatuamuru tuheshimu maisha ya wanadamu wenzetu; "Usiue." Tunastahili hata kutafuta wema wa maadui zetu. Kadiri ulimwengu wetu unavyozidi kuwa na vita hili si jambo rahisi kuwafundisha watoto. Naomba tuchague njia ya Mungu ya upendo kuelekea wale ambao wametukosea.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

- Andaa mapema vifaa vyaa mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili. Wakaribishe wageni na ukusanye ujumbe wao wa mawasiliano wiki hii.

**Yalinde Mawazo Yako - "Daudi Aliamua Kupenda"**

Mfalme Sauli alivaa silaha zake na kuanda upanga wake. Alikuwa amerudi tu baada ya kuwafukuza Wafilisti lakini hakuwa anaenda kupumzika. Mfalme Sauli alikuwa tu amepokea ujumbe, "Daudi yuko nyikani!"

Sauli aliwaza: "Hii ni nafasi yangu. Naweza mtafuta Daudi nimwue."

Mungu alikuwa amemchagua Sauli kuwa mfalme wa Israeli wa kwanza. Mwanzo Sauli alikuwa mfalme mzuri, lakini alianza kumuasi Mungu. Kwa sababu hiyo alilazimika kuchagua mfalme, yule angemtii.

Mungu aliamua kuwa mfalme atakayekuwa wa Israeli angekuwa Daudi kwa sababu alimpenda na kumtii Mungu. Watu pia walimpenda Daudi na hiyo ilimfanya Mfalme Sauli kuwa na hasira., "Namchukia Daudi. Anajaribu kuchukua ufalme wangu."

Hiyo haikuwa ukweli lakini Sauli alipoendelea kufikiria juu ya Daudi na chuki, ndivyo alishawishiwa ya kwamba Daudi alikuwa adui yake. Saul alianza kutafuata njia ya kumwua Daudi. Sauli aliita jeshi lake na wakaenda pamoja kumtafuta Daudi. Daudi alikuwa amejificha pangoni aliposikia kelele. Kulikuwa na mtu mwingine kwenye pango! Daudi na watu wake walitazama .... Mfalme Sauli alikuwa ndani!

Marafiki wa Daudi walimwambia, "Hii nafasi yako ya kumwua Sauli. Yeye ni mtu mbaya, anamuasi Mungu na anajaribu pia kukuua. Mungu alimleta Sauli hapa ili uweze kumwua."

(Soma sentensi ifuatayo pole pole na kwa kuigiza.)

Kwa uangalifu sana Daudi aliteleza kwenda kwa Sauli, akatoa kisu chake nje, akanyosha mkono wake kuelekea kwa mfalme, na kukata . . . ukingo mmoja wa joho lake. David alinyata kurudi mahali watu wake walikuwa. Sauli hakusikia wala kuhisi kitu!

Daudi alihisi vibaya; alikuwa ameonyesha kutomheshimu mfalme, "Singeanya hivyo. Mungu alimchagua awe mfalme wa Israeli. Sitamwumiza Mfalme Sauli!"

Baada ya dakika chache Sauli aliondoka ndani ya pango kuendelea kumtafuta Daudi. Daudi alingojea hadi wakati Sauli alikuwa mbali kidogo na kisha akaondoka pangoni. "Sauli," Daudi aliita kwa sauti! Mfalme aliangalia nyuma, kwa mshangao. Sauli hangeamini kwamba Daudi alikuwa karibu hivyo!

Daudi aliinama mbele yake na kusema, "Kwa nini unawasikilisa wale wanaokwamba kwamba ninataka kukuumiza?" Daudi alimwonyesha Sauli kipanda cha vazi na kupiga kelele, "Tazama – Ningechukua uhai wako! Watu wangu waliniomba nifanye hivyo. Sitajaribu kukuumiza; mfalme aliyezaguliwa na Mungu. Kwa nini unajaribu kuniua?"

Sauli aliona vazi; lilitoka kwa viazi lake la kifalme! Kwa mshangao Sauli alifikiria, "Daudi angeondoa uhai wangu na nilitaka kumwua." Mfalme Sauli alihuzunika juu ya mawazo yake maovu kwa Daudi na kusudi lake la kumwua. Mwishowe Sauli alisema, "Wewe ni mtu mwema kuniliko. Siku moja utakuwa mfalme na wakati utakuwa, niahidi hutaua familia yangu. Niache niishi."

"Naaidhi!" Daudi alijibu na kurudi katika sehemu yake ya maficho katika pango. Sauli angebadilisha mawazo yake na kujaribu kumwua tena. Lakini aliamini kwamba Mungu atamsaidia na Mungu alipoona inafaa atamruhusu awe mfalme. Mpaka siku hiyo ilipofika, Daudi angetimiza amri ya Mungu na kukoosa kumwua Sauli.

### Zoezi

*Nitakusomea hali nyingi.* Ikiwa ninakuelekeza, rudi nyuma na useme, "Nitamtii Mungu na kufanya jambo sahihi." Kisha useme ni nini ungefanya katika kila hali:

- Rafiki yako wa karibu alikudhihaki kwa sababu unapenda kulala na mdoli wako.
- Rafiki anayeketi karibu na wewe aliandika katika kitabu chako.
- Kijana mkubwa alikusimamisha katika lango la shule na kuchukua penseli zako

Yesu alisema kwamba tunapaswa kuwapenda maadui zetu na kuwaombea wale wanatutesa. Mungu anataka watu wake wachague upendo badala ya uovu.

### Kukariri

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

Gawa mstari katika maneno kadhaa, kwa mfano: "Mtii Bwana", "Mungu wako", "Fuatensi amri yake," n.k. Andika neno kwa kila kadi, weka uso za kadi zikiwa zimeangalia chini juu ya meza, uzichanganye vizuri. Chukua kadi na uunde sentensi ikiwa na neno lililoandikwa kwenye kadi.

Kwa mfano: kadi inasema "Mtii Bwana," na mtoto anakamilisha: "Mtii Bwana Mungu wako na uwe mkarimu kwa dada yako.")

Kila mtoto anayechagua kadi akamilishe sentensi. Weka kila kadi iliyotumika uso wake ukingalia juu kwenye meza, ukikusanya mistari.

### Kufunga

Chora uso uliyokasirika na uso unaotabasamu:

1. Angalia uso wenye hasira na ufikirie mtu aliyekufanya jambo baya. Ombo kimya kwa mtu huyo. Ombo Mungu akusaidie kuwasamehe.
2. Angalia use wenye tabasamu na ufikirie jinsi utafurahia wakati unamwona huyo mtu tena. Baada ya kusamehe na kumwonyesha mtu huyo upendo hakutakuwa na hasira tena. Urafiki wenu utaendelea.
3. Ombo, ukimwomba Mungu atusaidie kuwapenda na kuwasamehe wale ambao wametutendea vibaya.

## Zoezi la 19



### LINDA MAWAZO YAKO

**Maandiko:** Kutoka 20:13; 1 Samweli 24; Mathayo 5:21-22, 43-45

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa jinsi ilivyo muhimu kusamehe.

**Mstari wa Kumbukumbu:** Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

#### Mviringo wa Kufikiria na Kutenda



Tazama hizi picha mbili hapa juu. Jadili ni picha gani inayowakilisha mawazo yako. Omba.

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba kuiba na kudanganya ni dhambi mbaya. Mungu anaweza kutusamehe tukitubu.

## Mstari wa Kumbukumbu

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

## Jitayarisha Kufundisha

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kulitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

**Kuiba na Kudanganya Kunaleta Matokeo Mabaya 2 Wafalme 5:13-27**

Naamani alikuwa mtu muhimu sana ambaye alimfanyia mfalme kazi. Aliishi mbali na Israeli na alikuwa na mtumishi aliyemfanyia kazi na alimjua Mungu wa kweli. Naamani alikuwa mgonjwa sana na ugonjwa mbaya ulioathiri ngozi yake na kusababisha vidonda katika mwili wake wote ambao ultiwa ukoma. Naamani alipata matibabu lakini hakuna hata moja iliyomsaidia. Aliathirika zaidi! Siku moja mtumishi alizungumza na mke wa Naamani akasema, “Elisha, nabii wa Mungu anaweza kumsaidia mume wako. Yeye yuko Israeli. Anaweza kwenda kumuona!”

Naamani alienda Israeli na kumtembelea Elisha. Nabii alijua mkuu wake anafaa kufanya nini ili aponywe na Mungu. Naamani alifanya kile nabii alimwambia na ukoma ukaangamia. Ngozi yake ilionekana mpya; vidonda vyota viliondoka! Alikuwa na furaha sana! “Asante, asante,” alimwambia Elisha. “Sasa ninajua kwamba hakuna Mungu katika ulimwengu wote kama Mungu wa Israeli. Tafadhalii kubali zawadi hii kama shukrani.”

“Hapana,” Elisha alijibu. “Mungu alikuponya, si mimi. Sitazikubalia zawadi!”

“Nenda kwa amani,” Elisha alimwambia Naamani.

Gehazi, mtumishi wa Elisha, alikuwa anasikiliza “Siwezi kuamini kwamba Elisha hakukubali chochote kutoka kwa Naamani huyu wa Kilikia! Alikuwa na mavazi mazuri na zawazi za fedha. Elisha angekubali kitu!” alifikiria.

Mtumishi aliendelea kufikiria. Mwishowe aliamua la kufanya. “Nitamfuata Namaani na nimwulize zawadi na nijiwekee mwenyewe.” Gehazi alianza kukimbia.

Kwa umbali Naamani alimwona akikaribia na kugeuka kumtafuata mtumishi wa Elisha. Naamani aliuliza, “Je, kila kitu kiko sawa?”

“Ndio, kila kitu kiko sawa,” Gehazi alisema. “Lakini Elisha ana ujumbe wako. Kuna watu wawili ambao wana ujumbe wako. Kuna watu wawili wadogo ambao wanahitaji msaada wako. Anauliza unipatie zawadi za fedha na mavazi yao.”

“Sawa!” Naamani alisema. “Nitakupa zawadi za Elisha.”

Gehazi alichukua zawadi kutoka kwa Naamani na kumrudishia Elisha.

“Ulikuwa wapi, Gehazi?” Elisha alimwuliza.

“Unamaanisha nini?” alijibu. “Sikuenda mahali popote. Elisha alitikisa kichwa kwa huzuni na kusema,”Ninajua ulichokifanya Gehazi! Ulidanganya na ukaiba. Umetenda dhambi pia mbele za Mungu. Ulivunja amri zake.” Gehazi aliinamisha kichwa kwa aibu. Elisha alikuwa amegundua kile alichokuwa amefanya. “Sasa utaadhibiwa kwa dhambi yako! Elisha alisema. “Wewe na watoto wako mtakuwa na ukoma, katika hali ile ambayo Naamani alikuwa nayo kabla hajapona.” Na hivyo ikatendeka. Kwa huzuni, Gehazi alilazimika kujifunza matokeo mabaya ya kuvunja amri ya Mungu.

### Zoezi

“Je, ulisikia nini?” Rejelea:  
Watoto wote waketi kwa mviringo.  
Ili kurejelea hadithi, uliza maswali ili kuona kile watoto walisikia:  
Kwa mfano, unaweza kusema: “Nilisikia kwamba kulikuwa na mtu muhimu, ya kwamba alikuwa mwanajeshi.”  
Uliza mtoto wa 1 wa mkono wako wa kushoto: “Je, ulisikia nini?”  
Mtoto wa 1 anaweza kujibu “Jina lake ni Naamani.”  
Mtoto wa 1 atamwuliza mtoto wa 2: “Je, ulisikia nini?  
Mtoto wa 2 anaweza kusema: “Naamani alikuwa na mtumishi.”  
Mtoto wa 2 atauliza wa mtoto wa 3:: “Je, ulisikia nini?”  
Na katika njia hii, wataendelea kueleza hadithi ya Biblia.

### Kukariri

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)  
Andika mstari huu hapo juu kwenye kadi ndogo, kila neno kwenye kadi yake. Zichanganye kadi. Chagua namba inayofanana ya watoto kama vile kadi. Watoto wasimame kwa mshororo. Peana kadi moja kwa kila mtoto. Waambie watoto wajaribu kufikiria mpangilio wao sawa na waseme mstari kwa sauti kama vile unafaa kusemwa.

### Kufunga

Ikiwa sisi ni watoto au watu wazima, Mungu ana uwezo wa kutusamehe na kutuzuia tuisianguke. Omiba pamoja na watoto na Mungu awasaidie waepuke kusema uwongo. Tunapaswa kusema ukweli kila wakati!

## Zoezi la 20

### KUIBA NA KUDANGANYA HULETA MATOKEO MABAYA

**Maandiko:** 2 Wafalme 5:13-27

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba kuiba na kudanganya ni dhambi mbaya. Mungu anaweza kutusamehe tukitubu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

Je, Gehazi alifanya nini?



- Alimwambia Naamani  
aabudu sanamu
- Alimdanganya Naamani
- Alimwambia Naamani kwamba  
Elisha alitaka kumuona



- Alinunua mavazi
- Alimmunulia Elisha  
zawadi
- Alichukua pesa na  
mavazi ambayo  
hayakuwa yake.



- Alimdanganya Elisha.
- Alimwomba Elisha  
pesa.
- Alimwambia Elisha  
alikuwa mgonjwa.

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi waelewa hatari za ulafi na kushukuru kwa kile Mungu ameturuhusu kuwa nacho.

## Mstari wa Kumbukumbu

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

## Jitayarisha Kufundisha

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kulitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

**Ulafi ni hatari 1 Wafalme 21:1-29**

Mfalme Ahabu alitaka shamba la mizabibu, “Shamba nzuri sana la mizabibu! Tazama ile mizabibu, nguzo nzuri mno! Zinaonekana kuwa na ladha! Shamba hili linaweza kuwa nzuri kwa mboga zangu!” Ahabu alipozidi kulitazama shamba la mizabibu, ndipo alilitamani. “Shamba lile lazima liwe langu. Mimi ni mfalme, ni lazima niwe na shamba nzuri zaidi,” alijiambia. Kisha akaenda kumuona Nabothi, mmiliki wa shamba.

“Habari Nabothi,” Ahabu alisema. “Naomba kusema na wewe.”

“Kuna nini?” Nabothi aliuliza.

Ahabu alijibu, “nalipenda shamba lako la mizabibu. Hakika, nalipenda, hivyo nalitaka. Unaweza kuwa na linguine ukilitaka. Nitakuacha uchague lile unalotaka.”

“Hapana asante,” Nabothi alisema. “Shamba lile la mizabibu ni la familia kwa muda mrefu na nitaliweka kwa ajili ya watoto wangu.”

Jambo hili lilimkasirisha Mfalme Ahabu sana na uso wake ulifunika na hasira. “Unafikiria mimi, Nabothi?” ni nani?” mfalme alimkemea. “Mimi ni mfalme na nalitaka shamba hili la mizabibu!”

Mfalme alirudi katika jumba lake la kifalme na kujifungia chumbani mwake. Aliingia kitandani, hakuamka, hakula wala kunywa, na alikuwa bado na hasira. Ahabu aliendelea kufikiria zaidi juu ya shamba nzuri la mizabibu, “Ni nzuri sana! Lazima liwe langu. Mimi ni mfalme.”

Mfalme alilalamika sana hadi Malkia Yezabeli alichoka kumsikiliza. Siku moja aliamua kusema naye, “Kwa nini usile? Je, tatizo lako ni nini? Kwa nini unanung’unika na kulalamika?”

“Nina hasira na huzuni,” mfalme alisema. “Nalitaka shamba la Nabothi la Mizabibu na hataki kunipa. Nilijitoa kumlipa na akasema hatakubali. Anawezaje kuwa mchoyo?”

Yezabeli alifura alipomsikia mfalme, “Wewe si mfalme wa Israeli? Amka, kula, na ufurahi; nitakuchukulia shamba la Nabothi,” malkia alisema..

Malkia Yezabeli alifanya mpango wa hatari sana. Alifanya kuwa Mfalme Ahabu. Aliandika barua na kuzifunga na pete ya kifalme. Kila mtu aliamini kwamba Ahabu alikuwa ameziadika. Mfalme hakuwa na wasiwasi kwa kile mke wake alikuwa anakifanya. Jambo lilikuwa muhimu kwake ni kupata shamba la mizabibu kutoka kwa Nabothi kwa gharama yoyote.

“Andaa chakula maalum na umwalike Nabothi,” malkia aliamuru. “Mpe kitu maalum, kisha useme mgeni alisema maneno mabaya juu ya Mungu na kisha umwue.”

Viongozi walimwalika Nabothi kwa chakula maalum. “Kaa hapa,” walimwambia Nabothi. “Tuna hiki kiti maalum kwako.”

Nabothi aliketi. Kisha watu wawili waovu walimwelekezea Nabothi kidole na kusema kwa sauti, “Alinena maovu kwa Mungu!”

Kila mtu alikubali kwamba Nabothi afe. Walimwua na kutuma ujumbe kwa Malkia Yezebeli. “Walimpiga Nabothi kwa mawe na akafa.”

Yezebeli alifurahi sana. Kwa haraka alienda kumwambia mfalme kwamba Nabothi alikuwa amekufa mfalme alienda na furaha kwa shamba la mizabibu. Ahabu alisugua mikono yake kama mtoto mwenye furaha na toy anayoipenda. “Mashamba haya ya mizabibu yote ni yangu sasa!” Alichukua mchanga kidogo na kuacha uteremke pole pole katikati ya vidole vyake, akihisi utamu wa ushindi.

Wakati Ahabu alikuwa anasherehekea Mungu alinena na Eliya, nabii wake, “Mfalme Ahabu amemwua Nabothi na anachukua mali yake. Nenda mahali yuko.”

Eliya alimpata mfalme mwenye furaha katika shamba lake mpya la mizabibu. “Mungu amekasirika na wewe,” Elijah alisema. “Umetenda dhambi, ulivunja amri yake! Umemwasi Mungu! Mungu atachukua kila kitu na utakufa!”

Papo hapo Mfalme Ahabu aligundua maovu yake na alihuzunika sana. “Imekuaje nikafanya jambo mbaya kama hili?” alilia.

Ahabu alijua alikuwa ametenda dhambi. Alijua amefanya jambo mbaya. Akilia na kuomboleza, alitubu, akavaa mavazi yaliyoraruka, na kumuomba Mungu amsamehe.

Mungu alijua kwamba Ahabu alisikitika kwa hivyo alimsamehe, lakini alimwambia Ahabu kwamba watoto wake hawatukuwa wafalme. Ahabu alifahamu kwamba alikuwa amevunja sheria ya Mungu bila kulipa matokeo. Alifahamu umuhimu wa kumtii Mungu.

## Kukariri

Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)

Waulize watoto warudie mstari mara kadhaa.

Kwa mviringo waambie watoto wapitishe mpira mdogo na soksi mzee, au makaratasi yaliyofungwa pamoja katika muundo wa mpira.

Imba wimbo. Muziki utakapokwisha mtoto anayeshika mpira mkononi mwake na aeme mstari wa kumbukumbu.

Endelea mara kadhaa, ukiwasaidia watoto kukariri mstari wa kitengo hiki.

## Kufunga

Macho yetu yakiwa yamefunga, ongoza katika ombi la kushukuru. Kila mtu anaweza kusema maneno mafupi kama: “Nakushukuru Bwana kwa mama yangu.” “Nakushukuru Bwana kwa baba yangu.” (Endelea kutoa shukrani kwa mambo yote ambayo Mungu anatupa: afya, familia, ndugu na dada, kazi, shule, vifaa vya kucheza, marafiki, waalumu, wachungaji, miti, maua, wanyama, n.k.)

Funga kwa maombi ya watoto kuwa na furaha na shukrani, badala ya kutaka vitu vile wengine wako navyo. Shukuru Mungu kwamba watoto wanajifunza Amri Kumi. Muomba Mungu atusaidie kukumbu maagizo ambayo ametuachia tufuate Amri Kumi. Muombe Mungu atusaidie kuwa na furaha badala ya walalamishi wa ulafi.

## Zoezi la 21

### ULAFI NI HATARI

**Maandiko:** 1 Wafalme 21:1-29

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi waelewa hatari za ulafi na kushukuru kwa kile Mungu ameturuhusu kuwa nacho.

**Mstari wa Kumbukumbu:** Kwa hivyo mtatii sauti ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu mkizifuata amri zake na masharti yake ambayo ninawaamuru. (Kumbukumbu la Torati 27:10)



## **UTANGULIZI – KITENGO CHA 6**

### **MUNGU NI WA KIPEKEE NA MWENYE NGUVU**

---

**Marejeleo ya Kibiblia:** Hesabu 13:1-14:42, 27:12-23; Yoshua 1, 3-4, 6:14, 6-15

**Mstari wa Kukariri wa Kitengo:** “Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo”  
(Yoshua 1:9b)

#### **Malengo ya Kitengo**

##### **Kitengo hiki kitawasaidiwa watoto:**

- Kuacha uoga na kumtumainia Mungu
- Kuwa na ujasiri wa kukabiliana na hali ngumu
- Kutambua kwamba wanapomtii Mungu, anawasaidia

#### **Masomo ya Lengo**

**Somo la 22: Enenda Mbele Bila Uoga**

**Somo la 23: Enenda Mbele kwa Ujasiri**

**Somo la 24: Enenda Mbele kwa Utifuu**

**Somo la 25: Enenda Mbele Kwa Nguvu za Mungu**

**Somo la 26: Enenda Mbele kwa Ahadi za Mungu**

Mara nyingi tunakutana na hofu na kukosa ujasiri wa kumtii Mungu. Kuptia masomo haya tuweze kuelewa kamba Mungu yuko pamoja nasi kila mahali na katika kila hali. Mungu atatusaidia kushinda hofu zetu za ndani hata wakati tunahisi peke yetu au bila msaada.

Tuweze kuona kwamba kuwa karibu na Mungu kutatuletea furaha.

Tuweze kuona kwamba tunapomtii Mungu, atatulinda, na hata katika hali za kutisha.

Tuweze kujua kwamba Mungu ni rafiki ambaye yuko kando yetu kila wakati.

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba tunaweza kumtumainia na kumtii Mungu.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

**Jitayarishe Kufundisha**

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kilitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****MUNGU NI WA KIPEKEE NA MWENYE NGUVU Hesabu 13:1-14:42**

Siku moja Mungu alimwambia Musa, “Tuma watu waende wakaipeleleze nchi ya Kanaani ambayo ninawapa wana wa Israeli.”

Musa aliwaita viongozi 12, “Enendeni Kanani. Chunguzeni nchi na mtambue kama ni nzuri au mbaya. Angalieni vile miji inavyofanana na kama nchi ni nzuri ya kupanda chakula. Leteni baadhi ya tunda linalomea katika Kanaani.”

Watu 12 walienda Kanaani mara moja na kuchunguza nchi yote kwa siku 40. Huko waliona sehemu za nyika, mashamba ya nafaka, tunda la ladha, na mito iliyotiririka kwa haraka. Wapelelezi walichukua, tini, makomamanga, na kukata rundo kubwa la zabibu. Lilikuwa kubwa sana hata walilazimika kubeba watu wawili. Siku arobaini baadaye walirudi na ripoti kwa Musa.

Walipofika, walimwonyesha Musa, Haruni na watu wote tunda waliloleta. Kumi kati ya wapelelezi walianza kusema, “Kanaani ni nchi nzuri. Tazama tunda hili nzuri! Hata hivyo, wamiliki wa Kanaani ni wakubwa na wenye nguvu. Wanaishi katika miji iliyo na kuta zenyenye nguvu.

“Tusiogope kwa ajili ya hayo,” Kalebu alisema, mmoja wa wapelelezi. “Nafikiri tunaweza kwenda na kuchukua nchi. Tunaweza kuchukua!”

“Usiende!” wengine walisema kwa sauti. “Tunaweza kuwavamia wale watu kwa sababu si wakubwatu, ni majitu! Watatupiga kama nzige!”

Waisraeli walikuwa wanaanza kukasirika. “Je, tulikuja hapa kwa nini?” walilalamika. “Mungu ataacha watutue sisi wote. Maadui watawateka nyara wake na watoto wetu. Turudi Misri. Tumchague kiongozi aturudishe.”

Musa na Haruni walipiga magoti na nyuso zao chini. Watu walikuwa wakimvunja Mungu heshima kwa kusema mabaya mengi juu yake. Je! Mungu angefanya nini?

Yoshua na Kalebu walirarua mavazi yao kuonyesha jinsi walighadhabika, “Hatusemi hivyo! Nchi ni nzuri na lazima tumtegemee Mungu. Usiwatishe watu. Mungu yuko pamoja nasi. Tunaweza kuchukua nchi!”

Watu hawakutaka kuwasikiliza. Waliogopa na kukasirika hata wakataka kumwuo Musa, Yoshua, na Kalebu.

Ghafla Mungu akawatokea kama wingu angavu la nuru! Pia alikuwa na hasira. “Hadi lini watu hawa wataendelea bila kuamini?” Mungu alimwuliza Musa. “Nitawaangamiza na kuanzisha taifa jipyaa na

familia yako.”

Musa aliomba, “Hapana Mungu, Tafadhali usifanye hivyo! Ulituleta kutoka Misri na kila mtu katika Kanaani anajua hilo. Wewe ni mwema na mwenye kusamehe. Tafadhali wasamehe watu hawa ingawa wamefanya mabaya makubwa sana!”

Mungu alijibu, “Nitawasamehe, bali sitaruhusu mmoja wao kuingia Kanaani. Waliona miujiza ambayo nilifanya kati yao lakini hawanitumaini wali kunitii. Waambie watu ujumbe huu: ‘Wataishi jangwani kwa miaka mingine 40. Hii inawakilisha mwaka mmoja wa kila siku ambao wapelelezi walichunguza nchi. Ila Yoshua na Kalebu walionitumaini, kila mtu aliye na miaka 20 au zaidi atakufa. Watoto wao siku moja wataishi Kanaani, bali hao hawataiona.’”

Wakati Musa aliwaambia watu yale Mungu alimwambia wahuzunika sana.

“Tumetenda dhambi,” walisema. “Kwa hiyo sasa tutaenda kwenye nchi ambayo Mungu alituahidi.”

“Msifanye hivyo!” Musa alisema. “Mmechelewa kuingia Kanaani.”

Wapelelezi 10 ambao hawakumtumaini Mungu baadaye walikufa. Walilazimika kusubiri tena miaka ingine 40 lakini walijua kwamba Mungu angetimiza ahadi yake ya kuwafikisha katika nchi ya Kanaani.

Yoshua na Kalebu waliamini katika ahadi kwamba Mungu angewapa nyumbani mpya. Walimtumainia Mungu na walitaka kumtii. Mungu anataka tumtumainie, tumtii, na kila kitu anachotaka sisi tufanye.

### Zoezi

Tengeneza seti ya kadi ili na maneno “Tumaini” and “Kutii” kwa kila mtoto. Chora herufi kubwa ya maneno mawili, ili waweze kupaka rangi, au kurembesha. Leta rangi, wino, brashi, kalamu za wino, mbegu, maharagwe, mahindi, mchele, gundi, makaratasi madogo ya kubandika yaliyo na picha za matunda, n.k. Waambie watoto warembeshe maneno kama wanavyopenda. Wanapoendelea kufanya kazi, chukua nafasi ya kuwauliza maswali juu ya somo na ueleza maana ya maneno hayo.

### Kukariri

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

Baada ya kurudia mstari wa kumbukumbu mara kadhaa uiandike bila utaratibu. Waambie watoto waandike kifungu katika utaratibu sawa.

### Kufunga

Kumwamini na kutii Mungu sio rahisi kila wakati. Mungu atatusaidia kama tu vile alivyowasaidia Yoshua na Kalebu. Sema sababu zozote za kumshukuru Mungu na mahitaji yoyote ya maombi. Ombea mahitaji. Muombe Bwana awasaidie watoto kujifunza kumtumaini na kumtii Mungu kama vile Yoshua na Kalebu walivyofanya.

## **Zoezi la 22**

### **ENENDA MBELE BILA UOGA**

**Maandiko:** Hesabu 13:1 – 14:42

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba tunaweza kumtumainia na kumtii Mungu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

Katika fumbo iliyo hapo chini tafuta maneno yaliyo upande wa kulia:



Je, unaweza kumtumainia nani? \_ \_ \_

Je, Unaweza kumtii Mungu? \_ \_

Je, ni nani anayetusaidia wakati tunahitaji  
ujasiri?

— — —

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba kama tu vile Mungu alivyompa Yoshua ujasiri wa kuwa kiongozi wa watu, atawapa pia ujasiri wa kufanya kile anachowaomba kufanya.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

**Jitayarishe Kufundisha**

- Andaa mapema vifaa vyaa mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kulitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Enenda Mbele kwa Ujasiri Hesabu 27:12-23**

Musa alikuwa amezeeeka sana. Alijua kwamba wakati wa kifo chake ulikuwa unakaribia na alikuwa na wasiwasi na watu wa Israeli. Walikuwa wakitangatanga jangwani kwa miaka 40. Punde wangkuwa wanaingia katika nchi mpya ambayo Mungu alikuwa amewaaahidi muda mrefu uliopita. Musa alimwambia Mungu, “Watu hawa ni kama kondoo. Wanamhitaji mtu awaongoze au wataendelea kutangatanga.”

Mungu alimjibu, “Yoshua ndiye mtu sawa wa kazi hii. Ananitumainia, na ananitii. Atakuwa kiongozi wa hekima. Mwambie Yoshua aende pamoja nawe na kuhani, na kusimama mbele ya watu. Mwekee mikono na uwaonyeshe watu kwamba unamweka Yoshua kuwa kiongozi wao.”

“Mungu nitafanya utakaloniambia,” Musa alisema.

Musa aliwakusanya watu wote pamoja. Pamoja na Eliezari kuhani, walismama mbele ya watu wote. Musa alimwekea Yoshua mikono na kumtaja kama kiongozi mpya wa watu.

Punde Musa alikuwa. Muda haukupita, Mungu alinena na Yoshua. “Yoshua ni lazima uwaongoza hawa watu kupitia Mto Yordani kwenda nchi mpya inayoitwa Kanaani. Nitatimiza ahadi niliyofanya na Musa ya kwamba nitawapa watu hawa Nchi ya Ahadi. Nitakuwa pamoja nawe. Ninakuamuru uwe hodari na mjasiri. Usiogope wala kuhofu kwa kuwa mimi, Yehova Mungu wako, nitakuwa pamoja na wewe popote uendapo.”

Yoshua alipeana maagizo kwa watu wajiandae kuvuka Yordani na kwenda nchi mpya. Je, watu hawa wangetii? Kwa miaka nyingi Musa alikuwa kiongozi!

Watu wote walikubali kumtii Yoshua kama vile walivyomtii Musa! Walitumaini na kuamini kwamba Mungu alikuwa na Yoshua kama tu vile alivyokuwa na Musa. Kwa shauku watu walisubiri maagizo ya Yoshua yaliyofuata. Punde tu wataingia katika nchi yao mpya.

**Zoezi**

Kabla ya darasa kutengeneza au kukopa vifaa vyaa kupigia ambavyo watoto wanaweza kutumia. Darasani pitisha vyombo. Cheza mandhari ya muziki na dansi ya kutosha. Waambie watoto

wazunguke darasa wakiambatana na muziki pamoja na vyombo, wakipiga mikono na binja. Wanapokuwa wakitembea, simamisha muziki mara kadhaa. Unaposimamisha, sema:

Mwalimu: - Ni nani anayetupatia ujasiri?

Wanafunzi: - Mungu!

Mwalimu: - Je, ni nani tunayestahili kumtumainia?

Wanafunzi: - Mungu!

Mwalimu: - Je, ni nani tunayestahili kumtii?

Wanafunzi: - Mungu!

Endelea kucheza, mkitembea, na kutangaza vile muda unavyowaruhusu.

### Kukariri

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b) Chora nyayo 11 kwenye kipande cha karatasi. Tengeneza nakala kwa kila mtoto.

Andika maneno ya Yoshua 1:9, neno moja kwa kila nyayo. Kata nyayo. Fanya zoezi la kuyaweka maneno katika utaratibu ili mstari uwe umekusanywa vyema. Changanya nyayo zote na uziweke pamoja mbele yao. Unapopeana ishara waambie waanze kuyaagiza hadi mstari utakakapokusanywa vizuri. Mtoto wa kwanza atakayepata ataongoza kikundi kusema mstari. Ifanye mara kadhaa.

### Kufunga

Tamatisha darasa kwa kuombea mahitaji yao (kwa ujasiri wa kukabiliana na hali ngumu) na mahitaji mengine watoto wako nayo. Muombe Mungu awasaidie kukumbuka kuomba wakati wanahitaji ujasiri.

## **Zoezi la 23**

### **ENENDA MBELE KWA UJASIRI**

**Maandiko:** Hesabu 27:12-23

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba kama tu vile Mungu alivyompa Yoshua ujasiri kuwa kiongozi wa watu, atatupatia pia na sisi ujasiri wa kufanya kile anachotaka wafanye

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

# **Yeye Ni Nani?**

Je, ni nani aliyejikuwa kiongozi wa watu wa Mungu katika historia? Weka herufi katika nafasi hizi hapa chini:

---

Yoshua alimtumainia Mungu. Mungu alimpa Yoshua ujasiri wa kufanya kile alichomwambia afanye.



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba  
Mungu atatuheshimu tukitii maagizo yake.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe  
popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

**Jitayarische Kufundisha**

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kulitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni. Kukusanya habari zao na usisahau kuwatemebelea au kuwapigia wakati wa wiki
- Chapisha Ukurasa wa Zoezi wa somo la 24. Bandika kwenye kipande kizito cha karatasi. Kata herufi. Kusanya mawe madogo 12. Fuatilia hadithi ya Biblia ambayo utasimulia.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Waagize watoto kama ifuatavyo:

- Chukua hatua 6 za mtoto
- rudi hatua 2 nyuma
- nenda hatua 3 upande wako wa kulia
- nenda hatua 4 za kuteleza upande wako wa kushoto
- ukisimama sehemu, zunguka kwa mviringo
- ruka ruka mara 7

Je, maagizo yalikuwa magumu kufuata?

Je, watu hupeana mwelekeo kwa nini?

Je, ni kwa nini inakuwa muhimu kufuata maagizo?

Je, ni nini kinaweze kutokea ukikosa kufuata maagizo unayopewa?

Kufuata maagizo ni jambo muhimu sana. Katika hadithi yetu ya Biblia leo tutatmbua jinsi ilivyo muhimu kufuata maagizo ambayo Mungu anatupatia.

**Yoshua 3-4**

Mungu alinena na Yoshua, “Waeleze makuhani wasimame katikati ya mto. Waeleze watu kamwe wasiguse safina; lazima ziwekwe mbali.”

Makuhani na watu walimtii Mungu na Yoshua. Wakati huo wa mwaka kingo za Mto Yordani zilikuwa zinatiririka na maji. Maji yalikuwa ya kina kirefu sana. Lazima makuhani wawe walijiuliza, “Kwa nini Mungu anatuambia tufanye kitu ambacho kinaweza kuwa hatari sana?” Lakini waliamua kumtumainia Mungu na kumtii.

(Tafuta sura kubwa ya mto. Funika nchi kavu na kipande kidogo cha mto.)

Makuhani waliweka miguu yao ndani ya maji. Mto uliacha kutiririka!

(Ondoaa kipande kidogo cha mto.)

Vito vya mto vilikuwa vikavu! Ni ajabu sana! Watu walitazama kwa mshangao na waliweza kuona jinsi maji yaliacha kutiririka wakati makuhani walimtii Mungu na kuingia ndani ya maji. Hawa watu walisikia hadithi jinsi Mungu alifungua njia kavu katikati ya Bahari ya Shamu wakati walikuwa wanaondoka Misri, lakini walikuwa hawajaona na macho yao. Sasa walikuwa wanaona nguvu za Mungu kwa vitendo!

Watu wa Israeli walivuka mto kwenye nchi kavu. Lakini makuhani walibaki katikati ya mto.

Baada ya kuvuka Yoshua aliendelea kutii kila agizo alilopewa na Mungu.

Mungu alimwambia Yoshua, “Chagua watu 12. Waambie wachukue mawe 12 kutoka katikati ya mto karibu na sehemu ambayo makuhani wamesimama. Waambie watu wayapeleke mawe kwenye sehemu tutakayolala usiku wa leo.”

Watu walibeba mawe kwa mabega yao kutoka katikati ya mto hadi nchi yao mpya ya Kanaani. Kulikuwa na jiwe moja kwa kila kabila 12 za Israeli.

Mungu alimwambia Yoshua, “Waeleze makuhani watoke ndani ya mto.” Makuhani walitii.

Mara tu kuhani wa mwisho alitoka ndani ya maji, maji yalianza kutiririka tena.

(Weka vipande vidogo vya mto kwenye nchi kavu tena.)

Watu walipoona yale Mungu alikuwa ametenda walimheshimu Yoshua kama kiongozi wao, “Mungu yuko pamoja na Yoshua, kama tu alivyokuwa na Musa.

Yoshua aliwaongoza watu kwenye sehemu ambayo wangelala usiku. Yoshua alitumia mawe 12 kujenga madhabahu hapo.

(Weka mawe 12 madogo juu ya meza.)

Yoshua alisema, “Siku moja watoto wetu watatuuliza maswali. Watatuuliza, ‘Je mawe haya yako hapa kwa nini?’ Waeleze kwamba Mungu alitusaidia kuvuka mto kwenye nchi kavu. Wambie wanaweza kumtumainia na kumtii Mungu.”

Siku hiyo Waisraeli walijifunza kwamba nguvu za Mungu ni kuu na zenyengetu zaidi kuliko za mtu mwingine au chochote tunachoweza kufikiria. Mungu anaweza kufanya mambo yote. Anatumia nguvu zake kulinda ulimwengu na watu. Hata kama hatuelewi mipango yake tunaweza kumtumainia. Yoshua na Waisraeli walimtumainia na kumtii Mungu. Tunaweza kufanya hivyo.

## Kukariri

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b) Zunguka darasani, kama Yoshua na Israeli, ukirudia mstari wa kumbukumbu mara tena.

## Kufunga

Kuwa na wakati wa maombi. Kila mtu amshukuru Mungu kwa kumsaidia.

Muombe Mungu atusaidie kumtii na kumtumainia.

## **Zoezi la 24**


### **ENENDA MBELE KWA UTIIFU**

**Maandiko:** Yoshua 3:4

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu atatuheshimu tukitii maagizo yao.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)


Kata na ukunje picha ya mto isimame.



Tumia kipande hiki cha mto kufunika nchi kavu:



Kata na ukunje picha za makuhani na watu ili waweze kusimama na kutembea ndani ya mto.



Ondoa kipande kidogo cha mto kuonyesha wakati Mungu alisimamisha maji.

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu anaweza kufanya mambo yasiyowezekana wakati tunamtumainia na kumtii.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo”  
(Yoshua 1:9b)

**Jitayarische Kufundisha**

Wakaribishe wanafunzi kwa upendo. Hakikisha kwamba darasa liko safi wakati wanawasili. Kabla ya kuanza kichwa cha leo rejlea kwa ufupi masomo tatu yaliyopita na uwaalize wanafunzi kutoa mifano ya vile wamekuwa waaminifu kwa Mungu.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Enenda Mbele kwa Nguvu za Mungu –Yoshua 6**

Siku hizo zilifurahisha sana kwa Waisraeli! Walikuwa tayari katika nyumba yao mpya; Kanaani. Waisraeli walikuwa wamesubiri muda mrefu lakini Mungu alitimiza ahadi yake ili kuwaleta katika nchi hiyo. Mungu alikuwa amemleta Yoshua na Waisraeli salama kuvuka Mto Yordani na sasa walikuwa tayari kushinda miji.

Karibu na jiji kubwa la Yeriko. Ilikuwa na kuta za juu na zenyе nguvu na milango mikubwa. Mungu alinena na Yoshua na kumpa mpango wa kushinda mji, “Fanya ninachokukwambia na mji utakuwa wenu.”

Yoshua alisikiliza kwa umakini kwa kila maagizo ya Mungu, “Kwanza zunguka Yeriko mara moja kila siku kwa siku sita. Makuhani saba watabeba pembe za kondoo mbele ya sanduku.”

Hakika Yoshua alishangaa wakati alisikia kile Mungu alimwambia afanye. Hiyo haikuwa njia ya kawaida ya kupigana vita. Yoshua alimwamini na kumtumainia Mungu.

Mungu alimpa Yoshua maagizo zaidi, “Siku ya saba mtauzunguka mji mara saba. Makuhani watapuliza pembe. Wakati makuhani watapuliza pembe zao kwa muda mrefu watu of Israeli watapaza sauti! Kuta za Yeriko zitaanguka na jeshi litaweza kwenda moja kwa moja mbele na kuuangamiza mji.”

“Tutafanya yale umetueleza, Bwana,” Yoshua alisema. Aliwakusanya watu na kuwaeleza mpango wa Mungu.

“Je, tutafanya nini?” makuhani waliuliza.

Yoshua alijibu, “Chukua sanduku la agano na mzunguke mji mkiwa mmelibeba sanduku.”

“Na je, sisi?” makuhani wengine saba waliuliza.

“Mtazunguka mbele ya Sanduku la Agano na kuchenza tarumbeta” Yoshua alisema.

“Tuambie tunaweza kufanya nini pia,” askari waliongezea.

Yoshua aliuliza, “Watu wengine wataenda mbele ya makuhani. Wengine wataenda mbele ya sanduku. Wakati mnafanya haya yote msipaze sauti au kufanya lolote. Subirini hadi niwaambie. Nitakapowapa agizo – PAZA SAUTI!”

Waisraeli wote walimtumainia Mungu. Walikuwa tayari kutii. “Twende!” waliambiana.

On the first day the Israelites marched around the city once and then returned to the camp. The following days they continued marching.

Siku ya saba waliamka asubuhi mapema. Waliuzunguka mjia tena. Lakini siku hiyo hawakusimama baada ya kuuzunguka mara moja. Walizunguka mara mbili, kisha mara tatu. Hatua zao za miguu ziliendelea kuwa na sauti zaidi. Walizunguka mara ya nne, tano, na sita! Miguu yao ilisikika kama radi iliyotikisa nchi. Mwisho, Israeli ilizunguka Yeriko mara saba kwa mara ya mwisho. Makuhani walicheza tarumbeta kwa sauti na kwa muda.

Mara tu Yoshua alisema, “Pazen i sauti, kwa sababu Bwana amewapa mji!”

Wakati huo watu walipaza sauti! Boom ... boom, vunja, boooom! Kuta zilianza kutingizika. Vunja! Nchi ilikuwa inatingizika! Kisha ... vunja, boooom! Kuta za Yeriko zilivunjika na kuanguka chini!

Askari wa Israeli walivamia mji. Papo hapo walikuwa wamewashinda kabisa maadui zao. Usiku huo kulikuwa na furaha kubwa kambini!

Mungu anaweza kufanya yasiyowezekana wakati tunamtumaini na kumtii. Watu walimtumainia na kumtii Mungu. Alitumia nguvu zake kufanya yasiyowekekana. Kuta na miji ya Yeriko iliangamia!

### Zoezi

Mpe kila mtoto kipande cha udongo/matope au unga. Katika somo letu leo nguvu ya Mungu iliangamiza mji mkuu na kuta zake kubwa. Kuta hizo lazima ziwe zilitengenezwa na matofali ya nguvu. Leo tunaenda kujenga tofali ambalo litatusaidia kukumbuka hadithi hii.

Finyanga udongo kwa umbo la tofali nene la mstatili. Na penseli au kalamu chora herufi “Y” kwenye tofali. Herufi “Y” katika tofali itakukumbusha “Yoshua” na Yeriko.” Mungu alifanya jambo lilikuwa ngumu kwa Yoshua na Waisraeli. Atafanya pia yasiyowezekana leo tukimtumaini na kumtii.

### Kukariri

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b) Watoto wawili watasimama au waketi wakiangaliana.

Mtoto A atafanya changamoto yake: “Nafikiri naweza kusema mstari kwa kutazama tu maneno (9).”

Mtoto B atamta changamoto Mtoto A akisema: “Nafikiri naweza kusema mstari kwa kutazama tu maneno (8).”

Mtoto A atapinga: “Nafikiri naweza kusema mstari kwa kutazama tu maneno (6).”

Watoto waendelee kutia wengine changamoto hadi kila mtoto afikirie wanaweza kuusema kwa maneno hayo machache na watatia changamoto wapinzani wao kwa maneno: SEMA MSTARI!

Kwa nasibu andika idadi ya maneno ambayo mtoto wa mwisho alitaja. Ikiwa mtoto aliye na changamoto anasoma maandishi kwa usahihi mpe tuzo ndogo au makofi maalum. Cheza tena!

### Kufunga

Eleza mahitaji yao na sababu ya kushukuru.

Tunaweza kumtumaini na kumtii Mungu kwa sababu anajua yaliyo mema kwetu. Mshukuru Mungu kwa hekima na nguvu zake. Ombea mahitaji na shukrani za watoto. Mshukuru Mungu kwa kuwasaidia kumtumainia na Kumtii.

## Zoezi la 25

### ENENDA MBELE KWA NGUVU ZA MUNGU



**Maandiko:** Joshua 6

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu anaweza kufanya yasiyowezekana tukimtumaini na kumtii.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Joshua 1:9b)





Kata na ukunje picha za watu ili wasimame.



Kata kuta na uzisimamishe.

Wafanye watu wazunguke kuta mara 7. Kisha piga KELELE na ufanye kuta zianguke chini!!!!



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba  
Mungu Hutimiza Ahadi Zake.  
Mtumainie Mungu.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe  
popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

**Jitayarishe Kufundisha**

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na ujaribu kilitayarisha darasa kabla ya wanafunzi kuwasili.
- Kumbuka kukaribisha wageni kukusanya habari zao kuwasiliana nao wakati wa wiki

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Enenda mbele kwa nguvu za Mungu. Yoshua 14:6-15**

Baada ya Waisraeli kushinda mji wa Yeriko waliendelea hadi katika nchi ambayo Mungu alikuwa amewahahidi. Yoshua aliwaongoza watu katika vita vingi juu ya Wakanaani. Mungu aliwasaidia kushinda maadui wao na kujinyakulia mji.

Baada ya vita vingi Waisraeli walishinda karibu Kanaani yote. Sasa ni wakati wa kugawa nchi katika makabila ya watu wa Israeli. Mungu alikuwa amemweleza Musa jinsi ya kufanya. Sasa Yoshua alikuwa na kazi.

Siku moja Kalebu alimwendea Yoshua na kusema, “Yoshua, unakumbuka wakati, miaka nyingi iliyopita, wewe pamoja na mimi tulikuwa sehemu ya wapelelezi 12 ambaa Musa alituma kuchunguza nchi mpya?”

“Nakumbuka vizuri sana,” Yoshua alijibu.

“Vyema,” Kalebu aliendelea, “Nilikuwa na miaka 40 wakati huo. Niliporudi kutoka safarini niliwaeleza watu kwamba tunapaswa kumtii Mungu na kuingia nchi.”

“Ndio,” Yoshua alisema, “Nilikubaliana na kila kitu alichosema. Ulimwambia Musa kwamba nchi ilikuwa nzuri na kwamba Mungu angetusaidia kushinda watu walioishi huko. Ulituomba tumtumainie na kumtii Mungu.”

“Hiyo ni sawa,” Kalebu alisema. “Lakini unakumbuka kilichotendeka baadaye? Wapelelezi wengine walipeana ripoti mbaya sana ambapo watu waliogopa kumfuata Mungu.”

“Ndio, Nakumbuka vizuri sana,” Yoshua alisema. “Hiyo ndio sababu tulipoteza miaka 40 jangwani!”

Kalebu aliendelea, “Lakini nilimtii Mungu kwa moyo wangu wote na Mungu alinena na Musa. Mungu aliniahidhi kwamba sitakufa jangwani. Alisema kwamba wakati nchi mpya ilikuwa yetu nitapokea sehemu ya nchi ambayo nilitembea juu ya kama milki yangu.”

“Ni kweli,” Yoshua alikubali akifikiria. “Bwana alikuwa ameweka ahadi aliyoifanya miaka 45 iliyopita wakati tulitangatanga jangwani,” Kalebu alisema. “Sasa niko na miaka 85. Lakini nahisi kuwa na nguvu mbeleni. Niko tayari kupigana kwa ajili ya nchi ambayo Mungu aliahidi kutupatia. Ukinipa mlima huu ambaa Mungu aliniahidhi, nitaenda na kuwashinda watu wanaoishi huko. Mungu atanisaidia!”

Yoshua alijibu, “Nina furaha kukupa mji wa Hebron, ambaa ni sehemu ya nchi ya ahadi tuliyopewa

na Mungu. Umekuwa mwaminifu kunitii. Ninakupa baraka za Mungu.”

Kalebu hakupoteza muda. Alienda Hebron na kushinda maadui walioishi huko. Kutoka wakati huo Hebron ilikuwa ya Kalebu na familia yake. Mungu alitimiza ahadi yake kwa sababu Kalebu alimtumainia na akamti Mungu kwa uaminiful.

### Zoezi

Kalebu alikuwa amesubiri kwa miaka 45 kwa Mungu kutimiza ahadi yake ya kumpa nchi.

Je, unayo miaka mingapi? Andika majibu ya watoto kwenye ubao.

Je, utakuwa na miaka mingapi katika miaka 45? Fanya hesabu pamoja na watoto.

Babu na bibi yako lazima wawe na miaka (51, 52, 53). Kalebu alikuwa asubiri muda mrefu kupokea kile Mungu alikuwa ameahidi. Lakini Mungu alifanya. Mungu kila wakati hutimiza ahadi zake. Kwa ujasiri tumaini na kumtii.

### Hili ndilo somo la mwisho ya kitengo hiki.

Rejelea masomo yote katika kitengo hiki kwa maswali rahili ambayo umeandaa mapema. Wakumbushe watoto juu ya viongozi wa Israeli kwa Nchi ya Ahadi. Jinsi walivyotumaini Mungu na jinsi hakuwaacha.

### Kukariri

“Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

Kama inawezekana, nenda mahali palipo wazi. Waambie watoto wasimame katika mistari miwili.

Simama mbali kiasi kutoka kwa vikundi viwili.

Sema kwa sauti: NENDA!

Mtu wa kwanza wa kila laini akimbie mahali upo.

Watakapofika, watageuka na kutazama kundi.

Watapaza sauti kwa neno la kwanza la mstari.

Mtoto anayefuata kutoka kwa kundi atakimbia na watapaza sauti kwa neno linalofuata la mstari na kuendelea. Kama mtoto hajui neno warudi mwisho wa laini. Kundi litakalokamilisha kwanza watasema mstari wote kwa sauti wakitumia marejeleo ya Kibiblia na watakuwa washindi.

### Kufunga

Omiba pamoja na watoto. Muombe Bwana afanye kila mtu amtumainie Mungu kama Kalebu; mtu ambaye alijua jinsi ya kumtii na kumtumainia Mungu.

## Zoezi la 26


### ENENDA KWA AHADI ZA MUNGU

**Maandiko:** Yoshua 14:6-15

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu Hutimiza Ahadi Zake. Mtumainie Mungu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe popote uendapo” (Yoshua 1:9b)

Jaza mapengo ukitumia maneno yaliyo katika mviringo wa rangi.



— — — — — hutimiza  
— — — — — kwa wale  
**wanao** — — — — —  
**ndani Yake na kum** — — —

# **UTANGULIZI – KITENGO CHA 7**

## **TUNAMUIGA YESU**

**Marejeleo ya Kibiblia:** Luka 9:51-56, 12:13-21; Marko 12:38-44; Yohana 4:1-42

---

**Mstari wa Kukariri wa Kitengo:** “Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.”  
(Yohana 14:21a)

### **Malengo ya Kitengo**

#### **Kitengo hiki kitawasaidia watoto:**

- Kujifunza umuhimu wa kuiga thamani za Yesu
- Kuchagua kila wakati njia za amani na zisizo za vita
- Kujuua kwamba wao ni wa thamani, si kwa sababu ya kile walicho nacho, bali kwa sababu kuwa hao ni nani
- Kujuua kwamba hata watoto wanahitaji Mwokozi

### **Masomo ya Kitengo**

**Somo la 27: Tafuta Amani**

**Somo la 28: Tafuta Upendo**

**Somo la 29: Mtafute Mungu**

**Somo la 30: Tafuta Uzima**

Mifano inayostahili kuigwa haipo. Waonyeshe watoto Yesu.

Wafundishe watoto maadili muhimu kama amani, upendo, sehemu ya Mungu katika maisha yao, na umuhimu wa kuwa na Mungu miyoni mwao.

Watoto wanaathiriwa sana na maadili ya wenzao wa shule. Mitazamo na njia za maisha za watoto wengi hutoka katika nyumba zisizo za Kikristo. Masomo haya ni muhimu sana ya kuwasaidia watoto kumuiga Yesu.

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi waishi katika amani na watu wote.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

**Jitayarishe Kufundisha**

Vita havikuwa sehemu ya mpango wa Mungu kwa watoto wake. Yesu alifundisha kwamba Mungu anatarajia wafuasi wake kuchagua amani.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Tafuata Amani (Luka 9:51-56)**

Yesu alitumia muda mwangiakuwafundisha watu juu ya upendo wa Mungu. Aliwaagiza pia jinsi ya kuwatendea wengine. Yesu aliwasaidia watu na kuwaponya.

Siku moja akiwa anafundisha Galilaya Yesu alijua alikuwa aende Yerusalemkuwaeleza watu kwamba Mungu aliwapenda wote. Yesu alijua kifo chake msalabani na safari yake ya mbinguni ilikuwa inakaribia. Yesu aliwaambia wafuasi wake, “Ni wakati wangu wa kwenda Yerusalem.”

Kila mtu alianza kuandaa kile angehitaji kwa ajili ya safari. Mmoja wa wanafunzi alimwuliza Yesu ni njia gani ambayo watafuata.

“Njia ya haraka ni kupitia” Yesu alijibu. “Itatuchukua tu siku tatu tukienda katika njia hiyo.”

“Lakini Yesu,” alimwambia mwanafunzi mwagine, “Wasamaria wanawachukia Wayahudi. Tukipitia Samaria tutakuwa na shida.”

“Tunafuata hiyo njia,” Yesu alijibu. “Wasamaria na Wayahudi wote waliumbwa na Mungu. Anapenda kila mtu kwa usawa. Tukikaribia mji mtu mmoja anaweza kwenda mbele na kuzungumza na watu. Wanaweza kuwaambia kwamba hatutaumiza mtu ye yeyote; sisi ni watu wa amani.”

Walipokuwa wanaelekea Yerusalemu Yesu aliwafundisha. Alitaka wanafunzi wake kuelewa kwamba Mungu aliwataka waonyeshe upendo kwa kila mmoja, hata wale walio waovu au tofauti. Walitembea hadi jioni. Ulikuwa wakati wao wa kusimama, kula na kupumzika.

“Kuna mjii hapa,” Yesu alibonyeza na kidole chake. “Tafadhal nenda ukaulize kama tunaweza kulala huko na kama kuna chakula.”

Baadhi ya wanafunzi walienda vijijini. Mtu aliwazungumzia kwa sauti, “Ninyi si wa hapa; Ninyi ni Wayahudi. Tunawachukia Wayahudi!”

“Tazama, tunaenda Yerusalemu,” mmoja wa wafuasi wa Yesu alisema. “Kikundi chetu kiko nje ya mlango wa kijiji. Tunahitaji mahali pa kulala usiku huu. Tunaweza kukaa hapa?”

“Tunajua tayari kule mnaenda,” Msamaria mwagine alisema, “hiyo ndiyo inatufanya tunakuwa na hasira.”

“Mnaamini kwamba hatustahili kwenda Yerusalemu. Tunakoabudu Mungu haitoshi kwa Wayahudi!” Wayahudi walifkiria Wasamaria walikosa kwa sababu walimtolea Mungu sadaka za kuteketezwa juu ya mlima wa Samaria. Wayahudi walifkiria sehemu nzuri peke ya kutoa sadaka ya kuteketekewa ili ni ndani ya hekalu la Yerusalemu.

Wanafunzi waliwaacha wanaume waliokuwa na hasira pamoja na mji wao. Walirudi na kumweleza Yesu kile kilichotoeka.

“Hatuweza kukaa!” walisema. “Hawataki lolote na Wayahudi!”

Yakobo na Yohana waliskia kilichotokea na wasema kwa sauti, “Je! Hao Wasamaria wenyе kiburi wanafikiria wao ni akina nani?” Yakobo na Yohana walijulikana kama wana wa ngurumo kwa sababu walikasirika kwa urahisi. “Je, hao Wasamaria wapumbavu hawajui wewe ni nani?” walimwuliza Yesu. “Wewe una nguvu kuliko nabii Eliya! Najua tutaafanya nini. Omba moto chini kutoka mbinguni! Wacha mji wote uteketee; hiyo itawapa somo nzuri!”

Yesu alipumua na kutikisa kichwa. Wanafunzi hawa wawili walikuwa na mengi ya kujifunza juu ya upendo wa Mungu.

“Huwezi kuwachoma watu na nyumba zao kwa sababu tu ni mbaya,” Yesu alifafanua. “Hiyo ni makosa. Nahitaji watu wa kuelewa kuhusu upendo wa Mungu! Matendo mabaya hayatasaidia watu kuelewa upendo wa Mungu kwao!”

“Lakini tufanye nini?” Yakobo na Yohana waliuliza.

“Tutaenda sehemu ingine, mji mwengine,” Yesu alisema.

Siku hiyo Yesu alifundisha somo umuhimu kwa ‘wana wa ngurumo’. Yakobo na Yohana walijifunza kwamba Mungu anawataka watu waishi katika amani na majirani wao na waonyeshe upendo wao, hata wakati majirani hawako wakarimu.

Tunaweza kujifunza kutoka kwa Yesu. Tunaweza kuchauga amani na kuamua kugeuka wakati wengine wanataka kupigana na kubishana na sisi.

## Zoezi

### **Jinsi ya Kuishi kwa Amani**

Watoto wataonyesha ‘vidole vyao juu’ au ‘vidole vya chini’ kulingana na kama taswira ifuatayo ni ya kuishi na amani au la:

1. Yesu alimsikiliza Baba yake, Mungu.
2. Yesu alimtii Mungu na akaenda Yerusalem.
3. Yesu na wafuasi wake walinena juu ya upendo wa Mungu.
4. Yesu aliwatuma baadhi ya wafuasi wake kwenda Samaria.
5. Wasamaria waliwachukia Wayahudi.
6. Wasamaria hawakutaka kumkaribisha Yesu na rafiki zake.
7. Yesu na rafiki zake walienda mji mwengine.
8. Wanafunzi walitaka mto uwanguke kutoka mbinguni hadi kwa Wasamaria.
9. Yesu anawataka 1 watu wote kupenda kila mmoja na wasipigane.

## Kukariri

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

Kila mtoto aandike, kwa njia ya urembo, mstari wa leo wa kumbukumbu. Waupeleke nyumbani na kuuweka nyumbani kwao mahali utaonekana.

## Kufunga

Waombee watoto wawe wachukuzi wa amani kati ya marafiki zao, katika familia zao, na katika sehemu yoyote ambayo kuna hali ngumu. Muombe Bwana awaepushe na maovu.

Watie moyo warudi kwenye darasa litakalofuata.

## **Zoezi la 27**



### **TAFUTA AMANI**

**Maandiko:** Luka 9:51-56

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi waishi katika amani na watu wote.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

Tazama picha hizi hapa chini na ujibu maswali yanayofuata:



1. Je, ni nani hakumkaribisha Yesu?
2. Je, ni nani alitaka moto ushuke kutoka mbinguni?
3. Je, Yesu alifanya nini?
4. Je, Yesu na wanafunzi wake walikuwa wanaenda wapi?

**“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)**

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba tunapenda kwa sababu ya upendo wetu kwaMungu, na wala sio kuonekana na watu.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, ye ye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

**Jitayariske Kufundisha**

Watoto wanaishi katika ulimwengu ambao unawafundisha kujaribu kuwa bora katika kila kitu. Wanapokua wanajifunza kwamba mafanikio hayapimwi na yale wengine wanafikiria juu yao na kiasi cha pesa na milki waliyo nayo maishani.

Somo hili litakupatia nafasi ya kuwaonyesha watoto kwamba kuna njia tofauti na bora; njia ya Mungu ya upendo. Tunahitaji kujua kwamba ni maoni ya Mungu yaliyo muhimu. Anafurahia wakati tunamuonyesha upendo na pia tunapoonyesha wengine upendo.

Watoto wanapaswa kujua kwamba Mungu hajali ni pesa ngapi tunayo au ni ngapi tumepata. Mungu anajali jinsi mioyo yetu na uhusiano zetu ziko na ye ye na watu wengine.

Gundua njia za kuwaonyesha upendo kwa Mungu. Tunaweza kutoa ahadi ya kumpenda na kumheshimu Mungu kuliko vitu vyote.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Zawadi Kubwa ya Upendo (Marko 12:38-44)**

“Wanaamini kuwa wanavaa vizuri sana na mavazi yao ya bei ghali,” Yesu alisema. “Waliamini kwamba ilikuwa vyema kufanya kila mtu awatazame. Wanapenda kuvutia wakati wanakaa mbele wakati wa ibada. Wanangojea na kutafuta mahali pazuri kwenye hafla. Wanajaribu kuwaonyesha kwamba wanampenda Mungu na kwambwa wanamtii, bali ukweli ni tofauti. Wanaonyesha tu upendo kwao wenyewe. Maombi yao kwa sauti ya juu yanapaswa kusikiwa tu na wengine, bali si kwa Mungu kuwasikia.”

“Hiyo inasaidia,” mwanamke alisema. “Ikiwa nitamuomba Mungu bali nawaumiza watu, hiyo si kuwaonyesha ninawapenda.” Yesu aliketi chini. Karibu aliweza kuona chombo cha matoleo. Alitazama pembeni na kuona kwamba watu walikuwa wakipita na wanaweka sadaka zao. Tajiri, ambaye alionekana kuwa wa maana sana, alikuja kutoa sadaka yake. Alihakikisha kuwa watu wanamtambua. Akaweka kiasi kikubwa cha sarafu na akatazama huku na huku kwa kiburi kikubwa. Yesu aliendelea kuwaangalia watu wengine matajiri ambao walifanya vivyo hivyo, wakifanya onyesho kubwa. Walijisikia fahari sana. Bila shaka, hakuna mmoja wao aliyefikiria juu ya Mungu. Ndipo Yesu akaona mjane masikini sana aliyekaribia kimya. Mwanamke huyo hakuangalia mtu yeyote. Alitembea akiwa ameinamisha kichwa chake chini. Alionekana kuwa chakavu, na mavazi ya viraka na yaliyoraruka. Mume wake alikuwa amekufa. Alikuwa na sarafu mbili tu! Yesu alitabasamu alipomwona akikaribia na kumpa Mungu kila kitu alichokuwa nacho.

“Tazama,” Yesu aliwaambia watu waliokuwa naye “Mtazame mwanamke huyu aliyekimya.”

“Lakini hakuwa na chochote cha kumpa Mungu,” Mitume walisema.

Yesu aliwajibu, “Nataka ukumbuke ukweli huu muhimu: yule mama maskini alimpa Mungu zaidi ya wale matajiri wote waliota, kwa sababu alitoa yote aliyokuwa nayo. Walitoa kutoka kwa ziada yao,

kutoka kwa mabaki yao. Mwanamke huyu masikini aliweka kila kitu alichopaswa kuishi.” Mungu hataki tutoe watu wengine wafikiri sisi ni wazuri. Anataka tutoe kila tunachowenza kwa sababu tunampenda, na wala si kwa sababu inatufanya tuhisi kuwa muhimu. Mwishowe wafuasi wa Yesu walelewa aliyokuwa anawafundisha. Sasa walielewa kuwa Mungu anavutiwa na sisi kumpenda, kumpenda jirani yetu, na sio kwa kuonekana. Hili lilikuwa somo muhimu hekaluni. Leo tunaweza kujifunza kitu maalum sana. Lazima tutoe mazuri tunayo kwa sababu tunampenda Mungu, si kwa sababu tunataka wengine watuone na kufikiria sisi ni wazuri au watu wa muhimu. Hii ni fursa nzuri ya kuitipisha toleo ikiwa haukufanya mapema. Yesu alifundisha mambo muhimu sana. Hadithi yetu ya Biblia leo inatufundisha kwamba jambo muhimu si kiasi tunachompa Mungu; kilicho muhimu kwake ni kwa nini tunakitoa. Anatutaka tutoe mema yetu kwa sababu tunampenda.

### Zoezi

Nakili au chora mbele ya sarafu tofauti za pesa za nchi yako. Bandika kwenye karatasi kama kadi. Paka rangi/rangi ya dhahabu, fedha, au shaba. Nyuma ya sarafu andika moja ya maneno ya mstari wa kumbukumbu. Kabla ya watoto kuja katika Shule ya Jumapili, ficha sarafu katika darasa lote.

Waulize wanafunzi watafute sarafu 14, pamoja na marejeleo ya Kibiblia: “*Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.*” (*Yohana 14:21a*)

Watoto watakapopata sarafu wanafaa kukimbia na kuziweka juu ya meza kwa njia sawa ili kuunda mstari wa kumbukumbu.

### Kukariri

“*Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.*” (*Yohana 14:21a*)

Wape watoto kipande cha karatasi na uwaambie waandike mstari wa kumbukumbu. Urembeshe vizuri uvezavyo. Peleka nyumban na mfanye mazoezi ya kuukariri.

### Kufunga

Weka kikundi kwa mviringo. Waambie wamuombee mtu aliye upande wa kushoto. Kila mtu aombe mtoto aliye karibu naye. Walimu wanapaswa kuombea darasa lote wawe watoto wa upendo wanaotii Neno la Mungu. Walimu wanapaswa kuwaombea wale wote walio tayari kumpenda Mungu na jirani yao bila kuonekana na wengine. Wamshukuru Mungu kwa upendo watoto walionyesha wakati walitoa hifadhi zao za mapato na kununua chakula kwa ajili ya watu wahitaji.

## **Zoezi la 28**



### **TAFUTA UPENDO**

**Maandiko:** Marko 12:38-44

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba tunapenda kwa sababu ya upendo wetu kwa Mungu, si kwa sababu ya kuonekana na watu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

### **Zawadi ya Upendo**



Je, wewe unaonyeshaje upendo wako kwa Mungu?

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba haimpendezi Mungu tukiwa walafi na wachoyo. Tukimpata Mungu, atatusaidia kumpenda zaidi ya maombi ya dunia.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

## Jitayarishe Kufundisha

Vipindi nya watoto kwenye televisheni, vifaa ya kucheza, na baadhi ya michezo imeundwa kwamba watoto watumie muda wa kutosha navyo. Vipindi hivi, vifaa nya kucheza, na michezo huwavutia watoto. Watoto, hata wazazi, wanaamini kwamba wakati wako na hivi vitu, watakuwa na furaha kila wakati.

Yesu anatufundisha njia tofauti ya kutafuta kile tunachotaka. Anafundisha kwamba milki, watu, na vitu tunavyotaka kucheza navyo havielekezi kwa furaha. Furaha ya ukweli inapatikana kupitia tu kwa uhusiano wa karibu na Mungu. Watoto leo wanahitaji kusikia kwamba Bwana anayo mengi zaidi kwao kuliko mali; vipindi nya televisheni, vifaa nya kucheza, mchezo, n.k. Ana uzima wa milele akilini, na wanapaswa kufanya uamuzi. Watoto wanaweza kumchagua Mungu kwanza bila kujali wengine wanafanya nini au kusema nini.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

- Andaa mapema vifaa vyovyyote nya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili.
- Kumbuka kukaribisha wageni, chukua sadaka, wakaribishe wageni, na ukusanye habari za familia zao ili kuwasiliana nao wakati wa wiki
- Kabla ya kuanza kufundisha kichwa cha leo kwa ufupi rejelea masomo mawili yaliyopita. Waulize watoto jinsi walivyofanya wakati wa juma na ikiwa wana mahitaji yoyote ya maombi. Chagua zoezi litakalowasaidia watoto kuelewa somo.
- Nyakua usikilifu wa wanafunzi: “Tuseme mna televisheni nyumbani kwenu na wazazi wenu wanawaruhusu kutazama vipindi vyote nya watoto wakati wowote mnapenda. Mna pia vitu vingi nya kuchezea, na michezo. Je! mngejisikiaje?” (pata majibu kutoka kwa watoto)

## Mtafute Mungu

Katika hadithi ya Luka 12:13-21, tunampata kijana mdogo aliyetaka mengi zaidi:

Watu wengi walikusanyika karibu na Yesu, wakimsikiliza kwa makini. Mtu mmoja katika umati hakuwa na furaha. Mtu huyo alifikiria, “Pengine naweza kumpata Yesu amzungumzie ndugu yangu ili anipe sehemu ya urithi wake.” Mtu huyu alikuwa mdogo wa kaka wawili. Sheria ilisema kwamba kaka yake mkubwa angepokea urithi. Kijana huyo alikuwa na pesa lakini alihisi kuwa haitoshi; alitaka zaidi!

“Bwana,” alimwita Yesu. “Mwambie kaka yangu mkubwa anipe pesa za urithi. Sio haki kwamba anapaswa kuwa na zaidi yangu. Ninapaswa kuwa na zaidi!”

“Kijana,” Yesu alijibu. “Mimi si hakimu. Sio mimi kumfanya ndugu yako akupe pesa.” Kijana huyo hakuwa na furaha. Kisha Yesu alitazama umati na kuwaeleza hadithi.

Wakati mmoja, palikuwa na mkulima aliyekuwa tajiri

*Alikuwa amepanda nafaka nyingi katika shamba lake. Mwaka huu uzalishaji wake wa nafaka ulikuwa mzuri sana. Mavuno yalikuwa makubwa sana hivi kwamba mtu huyo hakuwa na mahali pa kuweka yote. ‘Nitafanya nini sasa?’ mkulima alijiuliza. “Sina ghalaa za kutosha kuhifadhi mavuno haya.”*

(Simamisha hadithi kuuliza maswali yafuatayo)

- Je ni nani aliyefanya mbegu ya nafaka kukua? (Mungu)
- Je, mkulima anapaswa kumwambia nini Mungu kwa kuvuna nafaka yenyeye afya? (Asante, Bwana,)
- Je, unafikiri mkulima angefanya nini na nafaka aliyovuna? (awasaidie wahitaji waliokosa chakula)
- Je, unafikiri mkulima alifanya nini na nafaka ambayo hangeweza kuhifadhi? (Jibu litakuwa tofauti)

*Biblia inatueleza mkulima aliharibu ghalaa yake ndogo na akajenga kubwa. Alikaa chini na kufikiria, “Maisha mazuri haya. Mimi ni mwenye nguvu na afya. Maisha yangu yatakuwa rahisi kwa miaka nyingi.”*

*Lakini Mungu alimwambia, “Wewe mpumbavu! Ulinisahau, ulisahau kunipenda, ulisahau kwamba kila kitu kinatoka kwangu.” Usiku huo yule mkulima alikuwa.*

- Je, alienda na nafaka? Je, angetumia mimea yake?

Yesu anatutaka tujifunze na kukumbuka kwamba haimpendezi Mungu tunapokuwa walafi na wachoyo. Tukimpata Mungu, atatusaidia kumpenda zaidi ya vitu vya dunia kama (televisheni, vitu vya kuchezea, pesa, na vingine vingi). Tunaweza kuamua kumweka Mungu katika nafasi yetu ya kwanza miyoni mwetu.

## Zoezi

Kuwa na pipi zinazotoshana na idadi ya watoto darasani. Ziweke mezani na uwaambie watoto wachukue moja moja. *Utaona kwamba watoto wengine watachukua zaidi ya moja na wengine watakosa.* Waeleze watoto walio na zaidi ya pipi moja washiriki na wale wamekosa. Waambie wasifungue pipi zao hadi kila mmoja awe amepata. *Itakuwa vigumu kwa watoto wengine kushiriki. Wakumbushe watoto kwamba hii ndiyo Yesu anatufundisha katika somo hili ‘Haimpendezi Mungu tunapokuwa walafi na wachoyo. Tukimpata Mungu, atatusaidia kumpenda zaidi ya vitu vya dunia.*

## Kukariri

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

Andika mstari wa kumbukumbu kwenye ubao au juu ya karatasi ya manila. Eleza maana ya mstari wa kumbukumbu kisha uwaambie watoto waurudie mara kadhaa. Sasa anza kufuta neno moja baada ya linguine (kama yako kwenye ubao) ukianzia neno la kwanza na uwaambie watoto warudie mstari wote hadi maneno yote yawe yamefutwa. Kama utatumia karatasi la manila, tafuta kitu cha kufunika maneno. Mwisho wake, baadhi ya watoto watakuwa wanasesma mstari wa kumbukumbu bila kuusoma kwenye ubao au karatasi la manila.

## Kufunga

Ombo na watoto. Yesu mpendwa tusaidie tusiwe walafi na wachoyo. Tusaidie ili tukuweke wewe wa kwawnza katika maisha yetu ili chochote kama televisheni, vitu vya kuchezea, michezo, riadha, au kitu kingine chochote kisichukue nafasi ya kwanza. Tujue kila wakati kumweka Mungu katika nafasi ya kwanza.


## **Zoezi la 29**

### **MTAFUTE MUNGU**

**Maandiko:** Luka 12:13-21

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba haimpendezi Mungu wakati tunakuwa walafina wachoyo. When we find Mungu He will help us love Him more than earthly things.

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye." (Yohana 14:21a)



**UNGANISHA NUKTA ILI UGUNDUE NANI  
HAKUMWEKA KATIKA NAFASI YA KWANZA....**

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi waelewe kwamba Wokovu ni wa kila mtu anayeamini ndani ya Yesu Kristo na kumpokea kama mwokozi.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, ye ye ndiyе anipendaye.” (Yohana 14:21a)

**Jitayarishe Kufundisha**

Wengi wetu tunawapenda watu ambao tunahisi starehe nao. Tunaona kufanana kati ya watu na pia tunaona utofauti. Mungu hajatuita tuchague watu wanaofanana na sisi au kukaa mbali na wale walio tofauti na sisi.

*Katika hali hiyo Yesu anatufundisha tuangalie zaidi ya wale tunahisi starehe nao. Anatutaka tupeane zawadi ya wokovu kwa wote wanaohitaji kumjua..*

- Wapokee watoto kwa upendo.
- Rejelea kwa ufupi masomo matatu yaliyopita na uwaambie watoto wazungumzie vile wamekuwa waaminifu kwa Mungu.
- Eleza maana ya maneno yafuatayo:
  - “**Wafuasi wa Yesu**” - watu wanaoamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, wanampenda na kumtii.
  - “**Uzima wa Milele**”-kuishi milele. Wakati tutakufa, wale ambao tumemkubali Yesu kama mwokozi wataishi naye mbinguni.
  - “**Maji ya Uzima**” – maji ya kiroho yanayopeana uzima wa milele.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

\* Jifanye hili lilitokea mahali: *Watoto walikuja kwenye darasa lao la shule ya Jumapili. Mtoto pia alikuja ambaye alikuwa amevaa vitambaa vivilvyochanwa na vichafu. Hakuwa na viatu vyovyote. Watoto wanakufa hawataki kukaa naye. Je! Ungehisije ikiwa ungekuwa mtoto huyo? Labda haujavaa kama mtoto huyo, lakini labda kuna kitu kinachokufanya uwe tofauti na watoto wengine. Pengine lugha yao ni tofauti na yako na wanasema hawataki uhusike nao. Je, ungehisiji viipi?*

Tunaenda kuona vile Yesu alihusika na watu ambao walikataliwa na kabilia yao (Wayahudi). Yesu na wanafunzi wake walikuja kutoka Yudea wakienda Galilaya. Yesu alisema wanapitia njia fupi zaidi, kupitia Samaria. *Wanafunzi wake hawakulipenda wazo hili - kwa sababu walijua Wayahudi na Wasamaria walichukia wao kwa wao.* Walifika kijiji katika Samaria ambapo walipata kisima. Yesu alikuwa amechoka na aliwaambia wanafunzi Wake waende kununua chakula katika mji wa karibu. Wanafunzi walipokuwa wakiondoka, mwanamke Msamaria alifika pale kisimani. Alibeba mtungi wake kuchukua maji. Yesu alimtazama na alijua kila kitu juu yake. *Mwanamke huyu alikataliwa na kila mtu katika eneo la nyumbani kwake kwa sababu ya mambo mabaya ambayo alikuwa akifanya.* Yesu alijua kuwa Mungu alimpenda na alihitaji mabadiliko katika maisha yake. Yesu alimuuliza yule

mwanamke Msamaria, “naomba maji ninywe?”

Mwanamke alishangaa! “Huyu ni Myahudi” alifikiria, “Wayahudi a Wasamaria, hasa wanawake hawanipendi.” “Je, mbona unaniomba kinywaji?”

Kwa sauti ya ukaribu Yesu alisema, “Ungelijua ni nani unasema naye, ungejua kwamba ninapeana zawadi kuu kutoka kwa Mungu. Ningekupatia” **maji ya uzima!**”

“kwa nini?” mwanamke alisema. “Je, ungewezaje kutoa maji kutoka kwa kisima?

Mwanamke hajua kwamba Yesu alikuwa anazungumzia **uzima wa milele**, wala si maji ya kawaida. Yesu alijibu, “yeyote anywaye kinywaji cha maji haya atakuwa na kiu tena bali yule anywae maji nitakayompa hatakuwa na kiu tena.

“Nahitaji hayo maji” Mwanamke alisema.

Yesu alijua kwamba mwanamke huyo alikuwa ameishi maisha ya dhambi lakini sawa, alihitaji upendo na msamaha wa Mungu. Maisha ya mwanamke huyo yalibadilishwa. Alitaka kujua zaidi kuhusu Mungu na aliwaalika watu zaidi kuja kumsikiliza Mwokozi.

Tunajifunza kwamba; *Wokovu ni wa kila mtu anayeamini katika Yesu Kristo na kumpokea kama Mwokozi wake.*

Mwaliko:

Wape nafasi watoto ambao hawajakubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi.

Tumia: - K, B, C.....

K – Kiri kwamba wewe ni mwenye dhambi (*sisi wote ni wenyе dhambi/tunafanya mambo mabaya na kutenganishwa na Mungu*) Lakini tukisema tunasikitika, Mungu anatusamehe.

A – Amini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, *Alimwaga damu yake kwa ajili yetu na ni yeye tu anayeondoa dhambi .....*

T – Mtangaze Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi. *Ili uwe na tumaini ya uzima wa milele.*

## Zoezi

Kuwa na rangi tano za kueneza za aidha karatasi, vitambaa, au shanga.

- Nyeusi inamaanisha **Dhambi** *ambazo sisi sote tumetenda*
- Nyekundu – **wokovu**, - *Yesu alikufa msalabani kwa ajili yetu wote.*
- Nyeupe – **Msamaha**- *wakati tunasema tunasikitika kwa Bwana, Anatusamehe,*
- Kijani kibichi – **kukua kwa kiroho** – *tunaendelea kukua katika kumjua Mungu kwa, kuomba, kusoma na kuitii Biblia, kwenda kanisani/Shule ya Jumapili na kuwaeleza wengine kuhusu Yesu Kristo.*
- Manjano – **Uzima wa milele** – *tunapookoka, tunamwishiа Bwana sasa na kisha nay eye mbinguni milele.*

Kila mtu atafute mwenzake. Badilishaneni kwa kila mmoja rangi za uinjilisti.

Nenda nyumbani na rangi ulizotumia leo kuwasaidia kuinjilisha marafiki wao. Hawana marafiki unaowapenda ambao unataka kushiriki rangi hizi na kwa sababu **wokovu ni wa kila mtu anayeamini Yesu Kristo na kumpokea kama mwokozi.**

## Kukariri

“Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)

Wasaidie watoto kukariri aya kwa kuirudia mara kadhaa. Chagua watoto waseme mstari kulingana na jinsi wamevalia (kwa mfano: *wasichana waliovaa nguo, wasichana katika sketi na blauzi, wavulana wakivaa kaptula, wavulana wakiwa wamevalia suruali, wale wenyе nywele fupi n.k.*)

## Kufunga

Omba na watoto: Asante Yesu kwa kutupenda sisi wote; bila kuwa na wa kupenda zaidi.

Yesu impendwa, tusaidie kuacha kuchagua watu tunaowapenda. Tupe ujasiri wa kushiriki ujumbe wako wa wokovu na kila mtu. Tusaidie kukumbuka kwamba wokovu ni wa kila mtu anayekuamini na kukupokea kama Mwokozi wake.


## Zoezi la 30

### TAFUTA UZIMA

**Maandiko:** Yohana 4:1-42

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Wokovu ni wa kila mtu anayeamini katika Yesu Kristo na kumpokea kama mwokozi wake.

**Memory Verse:** “Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.” (Yohana 14:21a)



# **UTANGULIZI – KITENGO CHA 8**

## **KANISA DUNIANI**

---

**Marejeleo ya Kibiblia:** Matendo ya Mitume 8:1-8:26-24, 10, 11:19-26, 13:1-12, 14:21-28

**Mstari wa Kumbukumbu wa Kitengo:** “Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonitura mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

### **Malengo ya Kitengo**

#### **Kitengo hiki ni cha kuwasaidia watoto:**

- Kujua kwamba Mungu alianzisha Kanisa kwa kusudi la kuwasilisha Habari Njema
- Kujua kwamba kazii kuu ya Kanisa ni kutangaza Injili
- Kujua kwamba hakuna kizuizi kinachowenza kusimamisha kukua kwa Kanisa ulimwenguni

### **Malengo ya Kitengo**

**Somo la 31: Habari Njema kwa Mtoashi**

**Somo la 32: Habari Njema kwa mtu wa Roma**

**Somo la 33: Habari Njema kwa Watu wa Antokia**

**Somo la 34: Habari Njema kwa Kila Mtu**

Kanisa la Yesu Kristo limeteswa na kushambuliwa kwa chuki nyingi. Pamoja na hayo yote, Kanisa halijaokoka tu, limeenea ulimwenguni kote. Mungu amewainua watu wa ujasiri na huruma ambao, hata kwa gharama ya maisha yao, wamemkiri Kristo na kutanganga Habari Njema. Watu hawa walitimiza agizo la Mungu; mkono wa Bwana ulikuwa pamoja nao. Nguvu za Mungu zilidhihirishwa kwa ishara, maajabu, na miujiza. Watu wengi walikuwa wafuasi wa Kristo. Ulimwengu umeharibika sana na dhambi inaonekana kutawala kila kitu. Bado, Kanisa la Yesu Kristo linabaki kuwa nyumba ya maadili ambapo tunaweza kupigana juu ya dhambi. Maisha yaliyopotea yanaweza kubadilishwa kuwa maisha mapya na safi.

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa inachomaanisha kuwa mmishenari na jisi injili ilianza kuenezwa.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonitura mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

**Jitayarishe Kufundisha**

Inampendeza Mungu tunapofikiria na kupenda watu ambaeo ni tofauti na sisi au ni kutoka tamaduni zingine. Wazo hili la Kikristo liliwekwa kwa matendo katika Kanisa la kwanza. Mbele ya Mungu watu wote wana thamani sawa na ni wazo Lake kwamba Wakristo wanapaswa kumfikia kila mtu na ujumbe wa mapenzi ya Mungu.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Maneno Muhimu**

- Habari Njema – injili .....kuwaeleza watu kwamba Yesu Kristo alikuba msabalani na akafufuka tena ili tuokolewe.
- Mmishenari .....Mmshenari ni mtu ambaye Mungu anatuma kueleza Habari Njema juu ya Yesu kwa watu kutoka tamaduni zingine.

“Je, kuna ye yote aliyepokea habari njema wiki hii?”

**Matendo ya Mitume 8:26-40**

Ilikuwa wakati mgumu kwa kanisa la Yerusalem. Wafuasi wa Yesu walikuwa wamefungwa kwa kueleza Habari Njema. Wengi walilazimika kukimbia kwa sababu maisha yao yalikuwa hatarini. Filipo alikuwa mmoja wa Wakristo hao na hivyo alikimbia kwenda Samaria. Filipo aliogopa kukaa Yerusalem, bali hakuogopa kuelezea watu juu ya Yesu. Filipo alihubiri, “Nina Habari Njema ya kuwaeleza.”

Watu walikusanyika kumsikiliza Filipo akiwaeleza watu hadithi nzuri ya vile Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za kila mtu ulimwenguni. Baada ya watu kuona miujiza ambayo Mungu alifanya kupidia Philip, wengi waliamua kumfuata Yesu. Kulikuwa na furaha kubwa katika mji huo.

Siku moja Mungu alimtuma malaika kwa Filipo ambaye alimwambia, “Nenda kusini kwenye njia ya jangwani. Ni njia inayotoka Yerusalem kuelekea Gaza.”

Filipo alimtii Mungu. Watu wengi walitembea kwenye barabara hiyo.

Alipokuwa njiani, Filipo akasikia kelele ya miguu ya farasi ikikaribia huku ikivuta gari lililombea afisa Mtoashi muhimu. Afisa wa Kushi alikuwa anasoma kutoka kitabu cha Isaya. Filipo alisikia afisa akisoma na akamwuliza, “Je unaelewa kile unachosoma?”

“Hapana, sielewi. Je, nitaelewaje? Nahitaji mtu wa kunielezea.” Afisa alimwalika Filipo apande kwenye gari na aketi naye.

Filipo aliemweleza afisa habari Njema ya Yesu kwa neema. Mtoashi alifurahia; kwa kujua kwamba Yesu alimpenda na kwamba alikuwa Mwokozi wake. Aliamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake. “Tazama!” Mtoashi alisema. “Kuna maji pale napenda kubatizwa.” Ubatizo ni njia ya kuonyesha kila

mtu kuwa Yesu amebadilisha maisha yako.) Filipo alimbatiza yule mtu.

Afisa Mtoashi alikuwa na furaha. Alimshukuru Mungu kwa kumtuma Filipo kwake. Afisa huyo alimshukuru Yesu kwa kuwa Mwokozi wake. Filipo aliendelea kusafiri kutoka mji hadi mji, akienda popote Mungu alimtuma kueleza Habari Njema ya Yesu.

### Zoezi

Wasaidie watoto waigize hadithi ya Filipo na Afisa Mtoashi.

### Kukariri

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonitura mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

Gawanya watoto katika vikundi viwili. Waambie watengeneza mistari miwili, wakisimama bega kwa bega na waliangalina na nafasi ya umbali wa theluji mbili (2/3)

Mstari wa A useme mstari wa kumbukumbu pamoja wakitembea kuelekea Mstari wa B.

Mstari wa B unapongeza kazi yao nzuri, “Vyema kabisa!” wakati mstari wa A unarudi nyumba katika sehemu yao ya mwanzo.

-rudia pamoja na Mstari wa B mkisema mstari wa kumbukumbu ....

### Kufunga

Bwana Yesu asante kwa kunikoa. Asante kwa watu wote umetuma kunieleza Habari Njema. Nisaidie ya kwamba nikutii kila wakati unaponitura kwenda kuelezea watu Habari Njema. Amina.


## Zoezi la 31

### **HABARI NJEMA KWA MTOASHI**

**Maandiko:** Matendo ya Mitume 8:1-8, 26-40

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa inachomaanisha kuwa mmishenari na jisi injili ilianza kuenezwa.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonituma mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi waelewe kwamba Mungu hana watu wa kupendelea. Anapenda kila mtu kwa usawa kwa kile pembe ya dunia. Mungu anataka watu wote wampokee kama mwokozi wao.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonituma mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

**Jitayarishe Kufundisha**

Watoto Wakristo wanahitaji kutambua kwamba Mungu anataka kila mtu ajue Habari Njema za Yesu Kristo. Wanahitaji kusikia kwamba Mungu anawapenda watu wote, haijalishi wanaishi wapi, wazazi wao ni nani, kabila lao au uraia wao, au iwe wanatoka katika nyumba za Kikristo au la. Bwana anawapenda watu wote na hana mapendeleo. Mungu anataka kile mtu ampokee kama mwokozi wao.

Mara tu watoto wamejifunza ukweli, watajifunza kuhusu umuhimu wa kuwafikia wengine na kuwaeleza kuhusu Yesu Kristo.

Kumbuka kuwaalika watoto wageni. Kusanya ujumbe wao wa mawasiliano wakati wa wiki.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Kuwa na picha za watu kutoka nchi na tamaduni tofauti. Waonyeshe watoto picha na uwaalize kile wanajua kuhusu sehemu hizo na tamaduni. Onyesha mambo mazuri juu ya kila tamaduni.

Waulize watoto ni wapi wangependa kutembea.

Katika hadithi ya leo tunajifunza kwamba Mungu anapenda watu wote kwa usawa, katika kile pembe ya dunia. Kwa sababu hiyo, tunaenda kuona jinsi Petro aliwasilisha Habari Njema kwa Kornelio.

Kornelio alikuwa mtu mzuri na muhimu katika jamii. Alikuwa jemadari (kamanda) wa jeshi la Kirumi. Aliamini Mungu mmoja wa kweli. Kornelio aliwasaidia wengine na alikuwa mtu wa maombi. Kornelio hakuwa Myahudi (watu wa Mungu waliochaguliwa). Siku moja mchana akiwa anaomba, Kornelio alikuwa na maono, Alimwona malaika. Kornelio alihangaika!

Malaika alimwambia. “*Kornelio, Mungu amependezwa na wewe. Mungu anataka ufhamu mengi kumhusu.*”

Kornelio alifurahi; hakika, alitaka kujua mengi juu ya Mungu.

“*Mtume mmoja wa watu wako katika mji wa Yopa*” malaika aliamuru. “*Huko utampata Petro ambaye atakueleza yote unayotaka kujua.*”

Papo hapo Kornelio aliwatumishi na askari kwenda Yopa. Walifika mjini wakati Petro alikuwa akiomba katika nyumba ya rafiki. Petro alipokuwa akiomba, yeze pia aliona maono. Aliona mbingu ikifunguka na kitu kama shuka kubwa ilishuka chini. Ilishushwa hadi kwenye nchi kwa pembe zake nne. Ndani yake kulikuwa na wanyama wa miguu minne ya nchi, wanyama watambaa, na ndege wa angani. Kisha akasikia sauti kutoka mbinguni ikitisema, “Amka Petro; kula na ule.” Petro alihangaika! Alijua kuwa Mungu alikuwa amewaambia watu wa KiWyahudi wasile wanyama wa aina hiyo kwa vile walikuwa wachafu.

“La Bwana, siwezi kula!” Petro alijibu. “Sijapata kula vyakula ambavyo ni najisi na vichafu.

Sauti ilinena tena, “*Usiseme vitu ni vichafu kama Mungu tayari amevifanya visafi.*”

Petro alipokuwa bado anashangaa na maono, Roho Mtakatifu alimnenea na kusema, “*Watu watatu wanakutafuta, nenda pamoja nao.*”

Petro alishuka chini na kukutana na watu hao. Watu hao walimwambia Petro kuwa kamanda wa Kirumi, Kornelio, alitaka kumuona. Wakati huu Petro alianza kuelewa maono. Alielewa kuwa Mungu hakuwa akimwonyesha wanyama katika maono lakini aina tofauti za watu aliowapenda sawa.

Maisha ya Petro yote yalikuwa mbali na Watu wa Mataifa (wasiokuwa Wayahudi), katika njia ile aliyepuka kula aina fulani ya wanyama. **Sasa Mungu alikuwa anamweleza kwamba ujumbe wa wokovu ulikuwa wa watu wote, hata Watu wa Mataifa.**

Siku iliyofuta Petro alienda na watu watatu na waumini kadhaa wa Yopa. Walipofika katika nyumba ya Kornelio walikutana na wengine wengi wakiwa wamekusanyika huko. Kornelio alimwambie Petro kuhusu maono yake.

Petro alifikiria, “*Hii ndio sababu nilikuwa na maono! Sasa naelewa kwamba Mungu hapendelei watu wengine juu ya wengine.*”

Petro alisema na Kornelio na wale wote waliokuwa nyumbani kwake juu ya Yesu na upendo wake, “Yesu ni Bwana wa kila kitu. Alikufa msalbani kwa ajili ya dhambi za watu wote na siku ya tatu alifufuka kutoka kwa wafu. Yu hai!”

Baada ya kusikia hayo yote, Kornelio na wale wote waliokuwa nyumbani kwake walimwamini Yesu. Mara tu Roho Mtakatifu aliwashukia. Waumini wa Kiyahudi walishangaa, “Roho Mtakatifu ameshukua juu ya Watu wa Mataifa pia?!”

Petro alifurahi! Aliwabatisa waumini wapya na akakaa na Kornelio siku kadhaa. Kila mtu alijawa na furaha.

Sasa tumejifunza jinsi Mungu anapenda watu wote. Habari Njema ya Wokovu ni ya kila mtu katika kila pembe ya dunia. |

### Kukariri

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonitura mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

Acha watoto waketi katika mviringo. Mpe mtoto wa kujitolea mpira. Mtoto anaanza mchezo kwa kusema neno la kwanza la mstari wa kumbukumbu kisha anarusha mpira kwa mtu mwingine na mtu huyo anasema neno linalofuata.

Hatua inarudiwa mara tena hadi mstari ukamilike.

Wale ambao hawawezi kukumbuka neno linalofuata katika mstari watoke “njie”.

### Kufunga

Ombo ukimshukuru Mungu kwa kumpenda kila mmoja kwa usawa. Mshukuru kwa watu wanaowaendea wengine na kuwaeleza juu ya upendo wa Mungu. Ombo kwamba Mungu atusaidie kupenda kila mtu na kuwaeleza Habari Njema ya Yesu.

Waambie watoto kila mmoja aorodheshe mataifa tofauti ambayo wanaweza kuwa wanaiombea katika wiki yote.


## **Zoezi la 32**

### **HABARI NJEMA KWA MTU WA ROMA**

**Maandiko:** Matendo ya Mitume 10

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi waelewe kwamba Mungu hana watu wa kupendelea. Anapenda kila mtu kwa usawa kwa kile pembe ya dunia. Mungu anataka watu wote wampokee kama mwokozi wao.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonituma mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)



**Habari Njema  
za**

**Yesu ni kwa  
watu wote.**

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Katika Antokia wafuasi wa Yesu waliiwtwa “Wakristo” kwa mara ya kwanza.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonituma mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

## Jitayarishe Kufundisha

Watoto wanajua vizuri inachomaanisha kuwa au kutokuwa sehemu ya kundi. Wanajaribu sana kukubalika, wangependa kuwa na marafiki wengi, na kujulikana kanisani na shulen. Mara nyingi, wanajihisi hawako muhimu kwa sababu hawafanya kitu “kikubwa.”

Kabla ya kuanza somo la leo, rejelea kwa ufupi masomo mawili yaliyopita.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

- Je, unajua ni kwa nini ulipewa jina ulilo nalo? (watoto wengine wamepewa jina la mshirika wa familia au tukio.)
- Je, unajua maana ya jina lako? (Acha wale wanaojuwa waeleze darasa. Chagua majina ya Kibiblia na ufundishe maana yake. Kwa mfano: “Dina’ inamaanisha haki, Petro inamaanisha mwamba”).

Maneno Muhimu:

\*“Mkristo.” Mtu anayepnda, anatii na ni wa Kristo, mwokozi.

**Barnaba na Paulo wahubiri Habari Njema**

(Mwigizo wa Matendo ya Mitume 11:19-29)

(Wavalishe watoto watakaoshiriki kwenye igizo wakiwa ndani ya mavazi ya kipekee ya zamani. uwa na nakala ya hati kwa kila muigizaji kusoma sehemu yake au wanaweza kuigiza sehemu wasomaji wakisoma hadithi).

Onyesho la 1

**Msimulizi:** Baada ya Stefano kupigwa kwa mawe hadi kufa waumini wengi waliwekwa gerezani na wengine wakakimbia kutoka Yerusalem hadi Antiochia kwa usalama. Antiochia haukuwa mji wa Wayahudi na hivyo wengi wa watu huko walikuwa wa Kimataifa (wasiokuwa Wayahudi). Mahali popote walikuwa wanafunzi wa Yesu waliendelea juu yake. Wakati hawa Watu wa Kimataifa waliskia Habari Njema, waliamini na kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Kule Yerusalem wanafunzi wa Yesu waliskia habari za idadi ya watu katika Antiochia wakuwa Wakristo! **Barnaba:** (Barnaba alisoma ujumbe kwenye karatasi lilikunjwa). “Sikiliza haya! Kuna kanisa mpia katika Antiochia ambalo linakua sana! Wanasema kuna watu wengi wa Kimataifa

wanaomfuata Yesu. Je, ni kweli?”

**Wanafunzi wa Yesu katika Yerusalem:** Barnaba, enda Antiokia – tueleze kinachoendelea!

#### Onyesho la 2

**Wanafunzi wapya wa Yesu katika Antiokia:** Mmekaribishwa sana, Barnaba! Tafadhali tufundishe mengi kumhusu Mungu. Tunataka kujua jinsi ya kumpenda na kumtii Mungu.

**Barnaba:** Mwabudu Mungu peke yake. Mumweke wa kwanza kila wakati. Katika kila jambo mnalosema au kufanya, tiini yale Yesu alifundisha.

**Msimulizi:** Watu wengi zaidi katika Antiokia walianza kumfuata Yesu.

**Barnaba:** Wanafunzi hawa wapya katika Antiokia wanataka sana kumwisha Yesu! Nahitaji kuwafundisha mengi, lakini nahitaji kwenda kuchukua msaada.

**Msimulizi:** Barnaba alisafiri kwenda Tarso. Alienda kusema na mwalimu wa Kiyahudi aliyeitwa Sauli. Hapo mwanzo Sauli alikuwa amewachukia na kuwatesa Wakristo, lakini sasa alikuwa mwumini wa Yesu. Jina lingine la Sauli lilikuwa Paulo.

#### Onyesho la 3

**Barnaba:** (Akizungmza na Paulo) Habari rafiki, u hali gani?

**Paulo:** Habari Barnaba! Je, kwa nini umfika Tarso?

**Barnaba:** Nahitaji msaada wako.

**Paulo:** Ninaweza kukusaidiaje?

**Barnaba:** Tunao wanafunzi wengi wapya katika Antiokia na wengi wao ni Watu wa Mataifa. Ninajaribu kuwasaidia kujua mengi juu ya upendo wa Mungu na vile wanapaswa kumtii. Njoo unisaidie kuwafundisha!

**Paulo:** Hilo ni jambo njema! Twende mara moja!

**Msimulizi:** Paulo na Barnaba wanaondoka kusafiri kwenda Antiokia.

#### Onyesho la 4

**Msimulizi:** Kwa mwaka mmoja Barnaba na Paulo walikuwa Antiokia wakiwahubiria wanafunzi wachanga wa Yesu. Watu waliskiliza na kujifunza jinsi ya kumpenda na kumtii Mungu. Punde is punde watu wa Antiokia walianza kuwafanya mzaha watu waliompenda na kumtii Mungu akiwaita “**WAKRISTO**”. Neno hili linaamanisha mtu ambaye ni wa KRISTO. Watu katika Antiokia waliwathihaki “Wakristo,” lakini “Wakristo” walikuwa na furaha sana kuendeleza jina hili maalum.

**Wakristo:** (Kusema pamoja) “Mkristo” ni mtu anayepokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Wakristo wanampenda na kumtii Mungu. Sisi, wanafunzi katika Antiokia tunaweza kuona kwamba sisi ni kama Yesu na ndio sababu tunaitwa “**Wakristo!**”

### Kukariri

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonitura mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

Andika mstari wa kumbukumbu kwenye ubao au karatasi ngumu. Waambie watoto warudie kuusoma kama mara tatu. Acha mtoto mmoja ajitolee kujificha si mbali sana na darasa. Wawambie watoto waliobaki kwa siri wachagua neno katika mstari na walifute. Acha watoto wasome mstari wa kumbukumbu lakini watakafikia kwa neno lililofutwa, badala ya kulisema, waambie wapige makofu. Mwambie mtoto anayejificha aseme neno ambalo marafiki wake waliruka.

### Kufunga

omba ukimshukuru Mungu kwa watu ambao wataeleza/kufundisha Habari Njema ya Yesu. Omba kwamba Mungu awasaidie kila wakati kusikiliza na kutii kile neno lake linatufundisha. Tuliendeleze jina hilo maalum la KIKRISTO kulingana na vile tunazungumza au kufanya mambo.

Peana nafasi kwa watoto ambao hawajampeka Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi.

Hatuwezi kuitwa kichwa hiki maalum cha UKRISTO kabla hatujapeana maisha yetu kwa Yesu, tunampenda, na kumtii. (Kama kuna mtu yejote, omba nay eye pia awe MKRISTO!).

## Zoezi la 33

### **HABARI NJEMA KWA WATU WA ANTOKIA**

**Maandiko:** Matendo ya Mitume 11:19-26

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Katika Antokia wafiasi wa Yesu waliitwa “Wakristo” kwa mara ya kwanza.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonitura mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)



WAMISHENARI

Tafuta maneno haya katika kinyang’anyiro kilicho hapo juu.

- Antokia
- Paulo
- Barnaba
- Wakristo
- Wamishenari
- Fundisha
- Mwalimu
- Omba
- Yesu

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi wajue kwamba kanisa ni sehemu ya mpango wa Mungu wa kuleta Habaari Njema ulimwenguni kote.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonituma mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

**Jitayarishe Kufundisha**

Watoto wanahitaji kuhisi kuwa ni muhimu katika kanisa la mtaa. Wanapaswa kujuu viongozi wao wa makanisa ni nani na wapate nafasi ya kuwajua. Hii pia ni sawa na wamishenari ambao Kanisa letu la Mnazareti linawatuma na kuwasaidia. Watoto wanapaswa kuwafahamu wamishenari kwa majina na picha zao. Wasaidie watoto wawasiliane na kuwatia moyo wamishenari. Wamishenari wameitwa na Mungu kwenda kuhubiri Habari Njema ya Yesu Kristo. Pesa ambazo tunaweka kwenye sadaka za kimishenari huwasaidia wamishenanri kutimiza mwito wa Mungu. Kuwaombea wamishenari pia ni sehemu ya mpango wa Mungu.

- Wapokee watoto kwa upendo.
- Rejelea kwa ufupi masomo matatu yaliyopita kabla kufundisha masomo leo.
- Zungumza na na watoto kuhusu changamoto za kuwa mwaminifu kwa Mungu.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Maneno Muhimu**

- Wamishenari - Watu walioitwa na Mungu na wametumwa na kanisa kwa taifa lingine kuwaeleza watu juu ya upendo wa Mungu.
- Mkristo – Wafuasi wa Yesu Kristo; ‘Kristo’ mdogo
- Habari Njema/Injili – Kushiriki juu ya Yesu Kristo
- Tamaduni – namna ambayo watu wanaishi na kile wanachoamini.

Safari yangu

Ninayoipenda

Keti kwa mviringo na mpira mdogo, ulio mwepesi.

“Nikikurushia mpira tueleze kuhusu safari ambayo umefanya. Kisha nirushie mpira. Kusafiri sehemu tofauti ni jambo ambalo wamishenari wanafanya mara nydingi.”

Wamishenari husafiri nchi zingine kueleza Habari Njema ya Yesu Kristo. Wanasaafiri ili kuhudumu kwa tamaduni zingine. Wamishenari wanajifunza kula aina tofauti za chakula na kuzungumza lugha tofauti za watu waliowakaribisha.

Katika somo lililopita tulijifunza kuhusu wafuasi wa Yesu Kristo katika Antiokia. Barnaba na Paulo

walikuwa baadhi yao. Wakati baadhi ya wafuasi hawa wa Yesu walikuwa wanamwabudu Mungu Roho Mtakatifu alinena, “Watenge Barnaba na Paulo wanitumikie. Nimewachagua kufanya kazi maalum.”

Wafuasi wa Yesu Kristo katika Antiokia waliomba, walifunga, na kuwatuma Paulo na Barnaba kama

wamishenari. Mwanzo wamishenari hawa walienda Selukia ya kusini. Walichukua mashua na kuelekea katika kisiwa cha Sipro ambapo walihubiri Neno la Mungu.

Paulo na Barnaba waliposafiri kwenye kisiwa, walikutana na Bar-Yesu. Mtu huyu alikuwa mchawi

na mwongo! Bar-Yesu alimfanya kazi mkuu wa kisiwa na alijaribu kumzuia asiwasikilize Paulo na Barnaba wakihubiri. Lakini mkuu alisositiza wahubiri; alitaka sana kusikia kuhusu Habari Njema ya Yesu.

Akiongozwa na Roho Mtakatifu, Paulo aliangalia moja kwa moja machoni mwa yule Bar-Yesu mwovu na akasema, Wewe ni adui wa yote yaliyo mema! Unawadanganya watu na kutumia kila aina ya ujanja. Je! Hautaacha kukasirisha njia za haki za Bwana? Sasa mkono wa Bwana uko juu yako. Utakuwa kipofu na hautaona jua kwa muda.”

Na hivyo ilitendeka! Mwovu Bar-Yesu, mchawi, alikuwa kipofu kabisa.

Akitazama hayo yote yaliyomtokea Bar-Yesu, mtawala huyo alishangaa! Akasema. Nataka pia kumjua huyu mtu Yesu”. Mtawala alisikiliza na kweli akawa mfuasi mpya wa Kristo pia.

Baada ya Kupro, Paulo na Barnaba walisafiri, wakirudi kwa miji nyingi ambayo walikuwa wamehubiri hapo mwanzo. Katika kila mahali walihimiza waumini wapya kusoma Maandiko, kukua katika imani yao, na kujifunza zaidi kuhusu Mungu. “Kumfuata Mungu mmoja wa kweli na ufanye mapenzi yake,” yalikuwa maagizo yao kwa wote. Katika kila mji Paulo na Barnaba waliwachagua viongozi wa kuwasaidia waumini wapya. Waliwaombea hawa wafuasi wapya wa Yesu na kisha kusafiri kwa meli kwenda Antiokia. Paulo na Barnaba walipowasili Antiokia, waliwakusanya washirika katika kanisa na kuwaeleza yote ambayo Bwana alikuwa ametimiza kupitia safari yao ya umishenari.

Paulo alilieleza kanisa katika Antiokia, “**Mlitutuma**. Mungu alifanya kazi kupitia kwetu. Sasa wengi wamekuwa wafuasi wa Yesu Kristo katika miji tofauti.”

## Zoezi

Uliza maswali juu ya safari:

- 1--- Je, ni nani waliokuwa kwenye safari? (Paulo na Barnaba)
- 2--- Je, ni nani aliywatumwa Paulo na Barnaba kwenye safari yao ya umishenari? (kanisa la Antiokia)
- 3--- Je, jina la mchawi alikuwa kipofu lilikuwa gani? (Bar-Yesu)
- 4--- Je, Paulo na Barnaba walifanya nini kwenye safari? (Walitembelea miji nyingi na kufundisha juu ya Yesu)

**Kanisa linawatuma** wamishenari. Wanaenda, wanafundisha, na kisha kurudi nyumbani kwao kutoa ripoti. Ni lazima tuwasaidie wamishenari wetu. Ni lazima pia tuombe kwamba Mungu alinde na kuongoza kazi ya umishenari katika sehemu zate za ulimwengu.

## Kukariri

“Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonitura mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

## Kufunga

Pamoja na watoto, imbeni wimbo, “Akiniita, nitaitika.”

Waombee wamishenari, hasa wale walio katika sehemu za hatari. Muombe Mungu awalinde na kusaidia kazi wanayofanya. Omba Mungu awaite watoto kuwa wamishenari.

## Zoezi la 34

### **HABARI NJEMA KWA WATU WOTE**

**Maandiko:** Matendo ya Mitume 13:1-12; 14:21-28

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi wajue kwamba kanisa ni sehemu ya mpango wa Mungu wa kuleta Habaari Njema ulimwenguni kote.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi Yesu akasema, “Amani iwe kwenu! Kama vile Baba alivyonituma mimi, name nawatuma nyinyi.” (Yohana 20:21)

#### **Misheni ya Ajabu**

Panga vikudni hivi vya herufi ili kupata maneno unayohitaji kukamlisha sentensi zilizo hapo chini.

Andika maneno katika sehemu zinazofaa. Omiba kwa kile unachowea kufanya ili kuwasaidia wamishenari..

ABOME  
PANED  
ABOM  
ASMO  
AOT  
AEZLE

1.  ----- **juu ya upendo wa Mungu.**
2.  ----- **juu ya kazi ya wamishenari.**
3.  ----- **wamishenari kila siku.**
4.  ----- **ili kuwasaidia wamishenari kushiriki Yesu.**
5.  ----- **watu wote.**
6.  ----- **Mungu awaongoze.**

## **UTANGULIZI – KITENGO CHA 9**

### **REHEMA ZA MUNGU**

---

**Marejeleo ya Kibiblia:** Mwanzo 4:1-16; Mwanzo 6; Mwanzo 7:1-8:19; Mwanzo 8:20-9:19.

**Mstari wa Kumbukumbu wa Kitengo:** “Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.”  
(Danieli 9:9a)

#### **Malengo ya Kitengo**

##### **Kitengo hiki kitawasaidiwa watoto:**

- kuelewa upendo mkubwa Mungu kwa watu
- Kujuia kwamba Mungu anathamini rehema zaidi ya dhabihu
- Thamini mfano wa Mungu: Yeye ni mfano wa huruma na upendo.

#### **Malengo ya Kitengo**

**Somo la 35: Hadithi ya huzuni ya Kaini na Habilii**

**Somo la 36: Mtu mzuri katika ulimwengu mbaya**

**Somo la 37: Mungu Amuokoa Nuhu**

**Somo la 38: Mungu Hutimiza Ahadi**

Kitabu cha Mwanzo kina vifungu mwafaka vinavyoweza kuwasaidia watoto kuelewa kwamba rehema ni moja ya huduma ya Mungu muhimu zaidi na inayohitajika. Hadithi za kutamausha za Kaini na Habilii na wokovu wa Nuhu zinaonyesha upendo na haki ya Mungu kwa rehema kubwa. Leo watoto wanajifunza rahisi tamaduni za “jicho kwa jicho na jino kwa jino”; lakini Mungu anatutaka tuwe watu wa kusamehe. Hadithi hizi katika Biblia si za kutungwa; ni hadithi za kweli. Mungu hajabadilika. Masomo haya yanafundisha kwamba Mungu ni wa rehema, na kwamba anasema: “Nataka rehema na wala si dhabihu.” Mungu anatutaka tuwapende majirani wetu!

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Kaini alipuuza yale Mungu alisema na kuruhusu mambo mabaya yanwelekeze kufanya matendo mabaya.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.”  
(Danieli 9:9a)

## Jitayarishe Kufundisha

Hii inaonekana kuwa hadithi ya ajabu ya kuwaeleza watoto. Somo hili hakika ni juu ya uamuza wa kumtii na kumuasi Mungu. Tunakuwa na wivu haraka tukiamini kwamba mtu mwagine anapendelewa zaidi kutuliko, anapata kusikilizwa zaidi, au anafurahia thibitisho kubwa. Mawazo mabaya yanaweza kutuongza kutenda matendo mabaya. Tunaporuhusu mawazo mabaya kukaa katika mawazo yetu, tunaweza kujipata katika hali mbaya zaidi. Mungu anaweza kutusaidia na kutulinda kwa kutenda matendo yoyote mabaya.

Tumzungumzie Mungu kwa uwazi. Tukimtii, atatusaidia.

- Andaa vifaa vya mafundisho ambavyo utatumia kwa somo hili na utayarische darasa lako kabla watoto hawajawasili.
- Kumbuka kuwaalika wageni na kukusanya ujumbe wao (namba za simu za wazazi) ili kuwasiliana nao wakati wa wiki.

Maneno muhimu:

- Tii: - kutenda yale Mungu anataka tutende
- Dhambi: - kumuasi Mungu na amri zake.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Chukua vipande viwili vya makarasi magumu. Kwenye kipande kimoja andika kwa kalamu nyekundi “SIMAMA – HATARI” na kwenye kipande kingine andika kwa kalamu ya kijani kibichi “NENDA”. Wape watoto wawili washike karatasi.

Sema sentensi kadhaa; Zingine za watoto walio na mawazo mema na zingine za watoto walio na mawazo mabaya.

Kwa mfano:

*Peter ana vifaa vingi vya kucheza. John hana vifaa vya kucheza hata moja Peter anashiriki vifaa vyake vya kucheza na John.*

Mtoto aliye na neno “NENDA” analiinua kisha wanasema kwa sauti “NENDA!”

*Julian ana mpira mpya wa miguu. Kakake Paulo alikuwa na wivu na akaahidi kuuvunja.*

Mtoto aliye na neno SIMAMA – HATARI aliinue na waseme “SIMAMA – HATARI!”

Endelea kutunga baadhi ya sentensi zako mwenyewe kwa watoto kuamua kati ya SIMAMA au NENDA!

*Mawazo mabaya yanaweza kukuelekeza kwa matendo mabaya kama ilivyo kwa hadithi ya leo:*

Maisha kwa Hawa na Adamu yalikuwa tofauti baada ya kumuasi Mungu. Hawakuishi tena katika Bustani nzuri ya Edeni! Kazi yao ilikuwa ngumu, walipata maumivu na kuugua. **Mungu bado**

### **aliwapenda.**

Punde, Adamu na Hawa walipata watoto. Hawa alimwita mtoto wa kwanza Kaini, ambayo ilimaanisha ‘Mungu alinisaidia kuwa na huyu mtoto’. Mtoto wa pili aliitwa Habili. Adamu na Hawa waliwfundisha wavulana kuhusu Mungu. Wavulana wawili walikua wazima na wenye nguvu. Kaini aliamua kuwa mkulima na Habili aliamua kufugha ng’ombe.

Siku moja Habili alitoa kondoo kama sadaka kwa Mungu. Alichagua kwa uangalifu bora zaidi

aliyokuwa nayo kwa dhabihu. Kaini pia alitoa sadaka; mboga na matunda alikuwa amekua. *Mungualifurahishwa na sadaka ya Habili, lakini si ya Kaini.* Kwa nini Mungu hakufurahishwa na sadaka ya Kaini? Biblia haielezi. Lakini tunajua kwamba Bwana ni mzuri na kila kitu Anachofanya ni chema. Kitu hakikuwa sawa juu ya sadaka ya Kaini, au katika ile njia alimtolea Mungu. Kaini alikasirika na Mungu. Lakini Mungu bado alimpenda. “*Je, mbona umekasirika?*” Mungu alimwuliza Kaini. “*Ukitenda yaliyo mema nitafurahia na wewe. Usipotenda yaliyo mema utakuwa unatenda dhambi. Uwe mwangalifu. Ni chaguo lako kutenda mema au maovu*”.

Kaini alisikia yale Mungu alimwambia lakini aliendelea kufikiria juu ya hasira aliyokuwa nayo. Baada ya muda mchache, Kaini hakumpenda ndugu yake tena. Siku moja Kaini alimwambia Habili. “Twende uwanjani pamoja.”

Habili alikubali na wote wawili walienda uwanjani. Walipokuwa huko, Kaini alimwua ndugu yake Habili na kumzika. *Haya ndiyo yalikuwa mauwaji ya kwanza.*

Baadaye Mungu alisema na Kaini, “Je, Yuko wapi ndugu yako Habili?”

“Sijui!” Kaini alisema. “Ni kazi yangu kumlinda Habili?”

“Najua kile umetenda,” Mungu alisema. “Wewe ni mbaya. Kuanzia sasa hakuna jambo litakuwa jepesi kwako. Utatangatanga kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Hatia hii ilikuwa kubwa mno kwa; kwa sababu alifanya uamuzi mbaya!

Kaini alikuwa amepuuza yale Mungu alisema na kuacha mawazo mabaya yamwongoze kutenda matendo mabaya. Hata kama Kaini alikuwa ametenda jambo libaya, Mungu aliendelea kumpenda na akaahidi kumlinda.

### **Kukariri**

“Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)

Anzisha mstari kwa darasa. Waambie watoto wafikirie juu hisia ambayo inawakilisha kila neno. Rudia mstari kwa hisia hadi waukariri mstari.

### **Kufunga**

Omba ukitoa shukrani kwa kila mtoto darasani, wazazi wao, kaka na dada na marafiki. Mshukuru Mungu kwa maisha yao ya kiroho na uhusiano wao na Mungu. Mshukuru Mungu kwa watoto wanaofika kanisani. Omba kwamba watoto watakuwa watiifu kwa Mungu, wazazi wao, kwamba watakuwa wazuri kwa nduguna dada zao/marafiki, na watakuwa na mawazo mema kwa Mungu na wengine.





## Zoezi la 35

### HADITHI YA HUZUNI YA KAINI NA HABILI

**Maandiko:** Mwanzo 4:1-16

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Kaini alipuuza yale Mungu alisema na kuruhusu mambo mabaya yamwelekeze kufanya matendo mabaya.

**Memory Verse:** “Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Nuhu aliamua kutii, hata wakati mtu mwengine hakufanya hivyo.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)

**Jitayarishe Kufundisha**

Watoto wachukue muda zaidi na watoto wa umri wao. Wanaathiriwa sana na wenzao. Kwa vile wanatumia muda zaidi na watoto wengine, wanakuwa na wasiwasi sana juu kile watoto wa umri wao au wenzi wa darasa wanafikiria na kuwathibitisha. Si rahisi kuwa tofauti na wengine wa kikundi; hasa siku hizi ambazo ni za maadili yaliyochafuliwa katika jamii.

Watoto wanalamizika kuamua chaguo lao. Je, sisi kama walimu wa watoto, tunawezaje kuwashawishi watoto kumtumaini Mungu kati hali ambayo wako tayari kumtii wakati marafiki wao wanawaambia wafanye kinyume?

Muombe Mungu akusaidie umwakilishe Nuhu katika ile hali ya kwamba watoto watamtamani na kutaka kutenda kama yeye. Nuhu alisimama peke yake mbele ya ulimwengu wa dhambi na vita.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Andika kwenye vipande vya karatasi majina ya wanyama na ndege ambayo ni rahisi kwa watoto kutambua, kwa mfano: paka, mbwa, ndovu, sima, nguruwe, kondoo, sungura, panya, punda, kuku, bata, njiwa, n.k. Tengeneza seti mbili za kila mnyama ili watoto wawili na paka, wawili simba, wawili mbwa, na kadhalika.

Mpe kila mtoto kipande kimoja cha karatasi na kilicho na jina la mnyama au ndege juu yake. Waambie watoto wasiliweke wazi au wasiaeze wengine ni mnyama gani waliye naye.

Chagua sehemu fulani katika sehemu yako ya kufundisha kuwa Safina. Mwalimu asimame kwenye lango la safina.

Watoto wajifanye kuwa ndege/mnyama; wakifanya sauti ya ndege/mnyama huyo watembee, na kutenda kama nyama/ndege. Waruhusiwe kutumia maneno yoyote. Lengo ni kwa watoto kutafuta mtu mwengine darasani ambaye ni mnyama/ndege sawa na vile walivyo.

Wakimpata mwenzio, wawili hao waje na wamwulize mwalimu, “Je, tunaweza kuingia ndani ya safina?”

Watoto hao wawili wataonyesha mwalimu vipande vyao viwili vya karatasi. Wanaweza tu kuingia ndani ya safina kama makaratasi yao yanaonyesha ndege/mnyama anayefanana.

Cheza hadi watoto wote wawapate  
wenzao.

*Mchezo huu unatukumbusha hadithi ya his Nuhu ambayo tunajifunza leo..*

Somo la leo linazungumzia jinisi watu duniani walitenda kwa mapenzi yao wenyewe. Kulikuwa na vita! Chuki! Kifo! Kila mahali Mungu aliangalia aliona watu wakitenda vile walipenda badala ya

kutenda wema. Ubinafsi wao ulikuwa mwingi kuliko upendo na wema kwa Mungu.

*Mungu alihisi uchungu mwingi sana na kuteseka moyoni Mwake. Hakuna aliyemtii Mungu au kutenda lililo jema. Hakuna mtu, ile mtu moja; Nuhu! Nuhu alipenda na kila wakati alijaribu **kumtii** Mungu.*

Mungu hakufurahia na hangeruhusu ulimwengu uendelee katika hali hiyo. Kwa huzuni, Mungu aliamua, “*Ni lazima niangamize ulimwengu huu na kila kitu ndani yake kwa gharika kubwa.*”

Mungu akasema, “*Nuhu, ulimwengu umejaa vita na maovu. Nitaangamiza kila kitu kwa gharika kubwa. Lakini nakuahidi kwamba nitakuokoa wewe na familia yako. Ili kuokolewa unahitaji kujenga safina; mashua makubwa. Zulia safina yako; weka vyumba vitatu ndani yake, mlango pande zake, na dirisha juu yake. Utakapokamilisha chukua wanyama/ndege wawili – kila kiumbe kilicho na uhai cha kiume au kike ndani ya safina. Weka chakula cha kutosha kwa ajili yako, familia yako, na kila kiumbe kilicho na uhai ndani ya safina.*”

Lazima Nuhu awe alishangaa kwa maagizo yote ambayo Mungu alimpa! Hakuwa na wazo lolote la gharika au safina aliyokuwa anaenda kujenga. Lazima Nuhu awe alikuwa na maswali mengi ya kumwuliza Mungu, lakini alimtumainia. Aliamini katika yale Mungu alisema, na AKATII.

Nuhu kwa haraka alianza kujenga safina. Pengine wana watatu wa Nuhu; Shemu, Hamu na Yafethi walimsaidia. Nuhu alijenga safina kwa miaka nyiningi!

Watu wote waliopita walitazama kile Nuhu alikuwa anafanya. Biblia haisemi kile walifikiria. Walipokuwa wakitazama Nuhu alifanya kazi na kutangaza ujumbe wa Mungu: *Bwana anawapa nafasi ingine ya kuokoka. Atamuokoa mtu ye yeyote anayetubu maovu yao (mabaya) na kuomba msamaha.* Lakini hakuna aliyesikia.

Mwishowe, safina ilikamilishwa. Nuhu, familia yake, na wanyama wote walilazimika kuingia ndani ya mashua kubwa. Nuhu alimtii Mungu kwa kila kitu. Nuhu hakujua kitakachotokea baadaye. Aliuja tu kwamba Mungu atamlinda yeye na familia yake, alikuwa ameahidi.

*Kama Nuhu tunahitaji kuchagua **kumtii** Mungu, hata wakati hakuna mtu anayetii.*

## Kukariri

“Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a) Andika mstari. Acha watoto waurudie mara kadhaa.

Waambie watoto watengeneze mviringo. Simama katika mviringo na urushe mpira nyororo kwa mtoto. Mtoto huyo atakuja katikati ya mviringo na aseme mstari na kisha arushe mpria kwa mtoto mwagine. Rudia mchezo hadi wote waseme kulingana na muda. Wasaidie walio na shida ya kusema mstari.

## Kufunga

Ombo na watoto ukimshukuru Mungu kwa kuwa mwenye rehema na msamaha. Muombe Mungu atusaidie kumtumainia na **kumtii**. Waombee hao watoto wadogo wanaopata ikiwa ngumu **kuwaitii** wazazi wao na walimu. Watie moyo watoto waombee kila mmoja wakati wa wiki.

## Zoezi la 36


### **MTU MWEMA KATIKA ULIMWENGU MBAYA**

**Maandiko:** Mwanzo 6

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Nuhu aliamua kutii, hata wakati mtu mwingine hakufanya hivyo.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)

## **Chagua Kutii**



**Jibu maswali yafutayo:**

- ◆ Je, Nuhu **alimtii** Mungu?
- ◆ Je, unawezaje **kutii** wakati uko shule?
- ◆ Je, unawezaje **kutii** wakati uko nyumbani?

**Fikiri juu ya jambo ambalo unaweza kufanya  
wiki hii ili **kumtii** Mungu.**

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Wale wanaompenda Mungu na kumtii watapata upendo wake na ulinzi katika njia ya kipekee.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)

**Jitayarishe Kufundisha**

Watu wanaomwitikia Mungu kwa tumaini na utiifu watapata upendo wake ambao wengine hawapati. Wengine wanakataa kutii na ndio sababu matokeo mabaya yanawajia. Nuhu, kama kila mtu, alitenda dhambi. Lakini kando na watu wengine waliomchukia na kumpuuza Mungu, Nuhu alimpenda Mungu na alitaka kumtii. Alipofanya hivyo, Mungu alimplinda. Bwana atafanya vivyo hivyo kwa watoto darasa wanaompenda na kumtii.

- Kabla ya darasa, kata seti 2 za kadi 26 kutoka kwa karatasi yoyote ngumu. Andika herufi za alfabeti kwenye kadi – herufi moja kwa kila kadi. Fanya seti 2 na uziweke zote ndani ya begi au kikapu.
- Rejelea kwa ufupi masomo mawili yaliyopita na uwaambie watoto waeleze jinsi Mungu amewalinda wakati wa wiki.

**Maneno Muhimu: Tii na Dhambi**

Andika maneno muhimu “tii” na “dhambi” kwenye kadi mbili. Ficha kadi hizo zilizo na maneno muhimu darasani. Waambie watoto watafute maneno mawili muhimu ya kitengo. Wakipata kadi waambie maana ya utiifu na dhambi. Uliza maswali ju ya maneno, kwa mfano:

1. Je, ni watu wagani waliohusika sana katika somo la kwanza la kitengo hiki? (Kaini na Hibili)
2. Je, Hibili alimtolea Mungu sadaka gani? (Kondoo). Je, alitenda dhambi au alitii? (Alitii)
3. Je, Kaini alimfanya nini ndugu yake Hibili? (Alimwua Hibili). Je, alitenda dhambi au alitii? (Alitenda dhambi)
4. Je, Nuhu alistahili kufanya nini? (Alijenga safina)
5. Je, alikuwa na maagizo jinsi ya kujenga safina? (Ndio, Mungu alimpa maagizo)
6. Je, ni wanyama wangapi wa kila aina ambao alistahili kuwaweka kwenye safina? (Mbili)
7. Je, ni nani aliyeingia na Nuhu ndani ya safina? (Familia yake)
8. Je, Nuhu aliweka nini ingine ndani ya safina? (Chakula kwa wote)
9. Je, Nuhu alitii? (Ndio, alitii)

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Waambie watoto waketi katika mviringo wacheze "Mchezo wa Safina Safina." Ukiwa unapitisha begi za herufi kutoka kwa mtoto mmoja hadi mwingine sema, "Safina Safina" je, mnao wanyama wangapi? Rudia jambo hilo mara kadhaa.

Wakati utaacha kuimba, mtoto aliye na begi atachukua herufi na kutaja wanyama wengi atakavyoweza ambao jina lake litaanza na herufi hiyo kabla ya kuhesabu 10. Andika kwenye ubao jina la kila mnyama bila kurudia kwa mfano: herufi C: - Paka, ngamia, mamba n.k.

Endelea kucheza hadi kila mtoto awe na nafasi ya kuhusika.

Fikiria ni wanyama wangapi Nuhu angeweka ndani ya safina, wawili wa kila aina. Kulikuwa na wanyama wengi!

Hadithi ya leo la Biblia inatueleza jinsi Mungu alimwokoa Nuhu, familia yake, na wanyama wengi. Ilimchukua Nuhu na familia yake zaidi ya miaka 100 kujenga safina. Mwishowe ilikamilika!

Tena Mungu alisema na Nuhu. "*Katika siku saba nitatuma mvua juu ya nchi. Itanyesha kwa siku 40 mchana na usiku. Wewe, mke wako, na wanao watatu, na wake zao wataingia safina. Chukua wanyama wawili wa kila aina na uwaweke ndani ya safina. Chukua jozi saba za wanyama wasafi; hawa ni wanyama ambao Mungu aliwaona wanatosha) kutoa dhabihu kama sadaka*".

Nuhu alifanya kila kitu ambacho Mungu alikuwa amemuamrisha. Kwa wiki mzima wanyama walifika na Nuhu atiwasaidia kuingia ndani ya safina. Nuhu na familia yake waliingga na Mungu alifunga mlango! Alitaka kila mtu awe salama. Ilianza kunyesha.

Wiki moja, mbili, tatu; mvua haikusimama! Maji yakaanza kupanda na kuongezeka, zaidi na zaidi. Ilianza kufunika mimea, miti, nyumba, na hata milima. Watuna viumbe vyote vivilivo na uhai kwenye nchi vilikuwa! Wale tu ambao hawakufa walikuwa Nuhu, familia yake, wanyama ndani ya safina, na viumbe vyaa baharini vivilivoishi ndani ya maji.

Baada ya siku 40 usiku na mchana mvua iliacha kunyesha. Mungu alikuwa anatengeneza nchi kuwa tayari tena kwa Nuhu, familia yake, na wanyama. Mungu alipuliza upepo ili kukausha nchi. Nuhu alitaka kujua vile nchi ilikuwa kwa hivyo alimtuma kunguru nje. Ndege alirudi kwa sababu hapakuwa na mahali popote palipokuwa pamekauka ambapo angejenga kiota. Baadaye Nuhu alituma njia lakini pia alirudi kwa sababu bado hapakuwa na mahali palipokauka. Asubuhi iliyoofuata Nuhu alituma njia kwa mara nyingine. Wakati huu alirudi na tawi la mzeituni katika mdomo wake. Habari njema hii kwa Nuhu na Familia yake! Maji yalikuwa tayari chini ya miti. Wiki baadaye Nuhu alituma njia tena. Wakati huu njia hakurudi.

*Nuhu alifikiria. "Nchi lazima iwe imekauka ili kwamba njia anaweza kutembea"* Je, Nuhu angefungua mlango wa safina? Hapani, alilazimika kusubiri Mungu amuagize.

Mwishowe siku nzuri ilifika! Baada ya Mungu kufunga mlango nyuma ya Nuhu, familia yake, na wanyama kwa mwaka mmoja na siku 10 Mungu alizungumza na Nuhu tena, "Toka ndani ya safina! Toa familia yako na wanyama nje".

Mungu aliwaambie waishi katika nchi na kuwa na watoto na kwamba wanyama na ndege wataongezeka. Kwa furaha Nuhu, familia yake, wanyama, na ndege walitoka ndani ya safina. Walianza maisha mapya duniani. Moyo wa Nuhu ulijaa furaha, upendo, na sifa kwa Mungu.

Mungu anawapenda watu wote duniani. Jinsi Bwana alitamani watu wangesema, "Utusamehe matendo mabaya ambayo tumefanya!" Tunapompenda na kumtii Mungu tutapata upendo na ulinzi wake kwa njia ya pekee. Siku hizi Yesu ndiye Safina la wokovu. Tunapomkubali kama Mwokozi Mungu atatukomboa kutoka kwa kifo na maangamizo yanayoambatana na hukumu ya dhambi.

## Kukariri

"Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha." (Danieli 9:9a)

Chagua dereva wa teksi. Dereva huzunguka darasa akiokota watoto wengine ambao wanahitaji safari. Njia pekee ya kupata safari ni kulipa nauhi. Badala ya kulipa pesa, lazima walipe kwa kusema mstari wa kumbukumbu. Yeyote anayesema sawa ataruhusiwa kuingia teksi

## Kufunga

Ombo na watoto kwamba Mungu atiwasaidia wawe watiifu kwa neno lake na kufanya kila kitu kinachompendeza. Watie watoto moyo waombee kila mmoja wakati wa wiki.


## Zoezi la 37

### MUNGU AMUOKOA NUHU

**Maandiko:** Mwanzo 7:1-8; 19

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Wale wanaompenda Mungu na kumtii watapata upendo wake na ulinzi katika njia ya kipekee.

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha." (Danieli 9:9a)



## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba wakati Mungu anafanya **ahadi**, tunaweza kuwa na uhakika kwamba ataitimiza.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)

## Jitayarishe Kufundisha

Nilikuwa mmoja wa watoto wenye bahati kwa sababu nilijua kwamba ikiwa wazazi wangu **waliniahidi** kitu, wangetimiza; hali mbaya tu ndizo zinaweza kuwazuia kutimiza **ahadi** zao kwetu watoto. Ukweli ulikuwa mkazo katika nyumba yetu, na uliwekwa kwa vitendo na baba, mama na sisi watoto. Ninahuzuniwa kwa watoto wale ambao husikia kila wakati "Ninaahidi" na kisha wanatambua kwamba ahadi haikutimizwa.

Ni msingi mdhaifu sana kwa wale wanaotamani kumtumainia Mungu.

Unapofundisha somo hili juu ya Nuhu kumbuka kwamba kutakuwa na watoto darasani mwako wanaojua kutoka kwa ujuzi wao **ahadi** zisizotimizwa ni gani.

- Katika somo hili lote wakumbushe watoto kwamba Mungu ni tofauti kutoka kwa mtu mwingine ye yote anayefanya **ahadi**. Yeye ni Mungu. Hakuna jambo linalompinga au kumzuira kutimiza **ahadi**.
- Wakaribishe watoto kwa upendo. Hakikisha kwamba darasa ni safi kabla watoto hawajawasili. Acha watoto wajue kwamba unawapenda.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Waulize watoto: Je, ni nani hufanya **anachoahidi?** (watoto watazungumzia juu ya wazazi wao, waalimu, au Mungu)

Je, tunajihisi aje wakati mtu anatimiza **ahadi** alizofanya?

Je, tunajihisi aje wakati mtu hatimizi **ahadi** walizofanya?

Katika hadithi ya leo tunaenda kujifunza jinsi Mungu anatimiza **ahadi** yake.

Nuhu na familia yake walikuwa ndani ya safina kwa mwaka mmoja na siku kumi; muda mrefu! Wakati huo tuko na . . . (taja likizo ambazo ziko katika nchi yako). Krismasi, Mwaka Mpya, Pasaka, na mambo mengi yanayotendeka katika mwaka mmoja na siku kumi. Nuhu na familia yake walikuwa ndani ya safina wakati huo wote. Walisubiri na kusubiri kwa siku ambayo wataondoka ndani ya safina na kuanza maisha mapya kwenye nchi. Mwishowe siku hiyo nzuri ilifika! Wakati siku hiyo maalum ilifika Mungu alinena na Nuhu akasema, "*Ondokeni ndani ya safina.*"

Kwa starehe kuu Nuhu, familia yake, na wanyama wote walitoka ndani ya safina na kuaza kuishi kwenye nchi. Nuhu na familia yake walimtii Mungu.

Fikiria kwamba ulikuwa pamoja na Nuhu wakati huo wote. Je, ni jambo gani la kwanza ambalo ungependa kufanya unaporudi kwenye nchi kavu? (Waruhusu watoto kujibu).

Nuhu alijua kwamba Mungu alitimiza **ahadi** Yake ya kumlinda pamoja na familia yake kutoka kwa

gharika kubwa. Moyo wake ulijaa shukrani na sifa kwa Mungu. Jambo la kwanza Nuhu alifanya likuwa kujenga madhabahu ya kumwabudu Mungu! Alitafuta mawe na kuyaweka juu.

(Waonyeshe watoto madhabahu inavyofanana; chora madhabahu kwenye ubao au panga mawe/vipanda vya kuni.)

Kisha Nuhu alichinja baadhi ya wanyama wasafi na ndege ambao Mungu alikuwa alikuwa ameamua na kuzitoa kama dhabihu. Nuhu alitoa sadaka kuonyesha Mungu upendo na shukrani zake. Hili lilimpendeza Mungu!

Mungu akasema, “*Sitatuma tenda gharika ingine juu ya nchi. Nataka wewe na watoto wako mwe na watoto. Naka ndege na wanyama wote wazae na kuja nchi.*”

Mungu alimwambia Nuhu awe akila nyama kutoka kwa wanyama na ndege. Pia alimwambia ale kutoka kwa mimea. Mungu almwagiza Nuhu, familia yake, na watu watakaoishi baada yao kwamba wasiwaumize (kuwaua) wenzao. Mungu akasema, “Nitamwadhibu yule atakayemwua mwenzake”.

Tena, Mungu alimwambia Nuhu na familia yake kwamba **ahadi** iliyofuata ilikuwa kwao na kizazi chao kitakachokuja baada yao. Ilikuwa pia ya wanyama na ndege waliokuwa ndani ya safina. Mungu alipokuwa akisema mara tu kitu kizuri kilitokea angani. Ilikuwa robo mviringo uliokuwa na rangi za urembo.

(Onyesha kipande cha karatasi kilichokatwa kwa robo mviringo na vipande vya rangi katika rangi tofauti za upinde.)

Wakati Nuhu na familia walitazama upinde wa rangi, Mungu aliwaambia, “*Sitailaani nchi tena na gharika, au kungamiza kila kitu kilicho na uhai tenda, kama vile tulivyofanya. Nimeweka upinde angani .... Wakati mwengine ninapoleta mawingu juu upinde wangu utaonekana na kisha nitakumbuka agano langu na wewe.*

(AGANO - **ahadi** iliyowekwa kati ya Mungu na watu)

*Hakutakuwa na gharika ya maji kuharibu kila kiumbe kilicho na uhai. Nitatimiza ahadi yangu milele.”*

Nuhu aliamini katika **ahadi** ya Mungu. Mungu alikuwa ametimiza **ahadi** zote alizozifanya. Alikuwa amemlinda Nuhu na familia yake. Mungu alihakikisha safina ilielea na kwamba maji hayakuingia ndani. Aliwalinda hata watu na wanyama hawakuogopa. Mungu alikuwa amethibitisha maelezo yote. Alilinda mimea na kuruhusu upepgo kupiga ili nchi ikauke. Mungu alikuwa amewalinda hadi ile siku aliwaambia waondoke ndani ya safina. Nuhu angeendelea kutumaini kwamba Mungu angetimiza **ahadi** zake zote. Tunaweza kuwa na hakikisho kwamba wakati Mungu anafanya ahadi ataitimiza.

## Kukariri

“Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)

Baada ya marudi kadhaa ya mstari wa kumbukumbu gawa darasa katika timu mbili na uwaambie watengeneze mistari miwili. (Ni bora kufanya zoezi hili katika uwanja ulio wazi) Ipe kila timu bendera ya kutikisa. Unaposema “Nenda” mtoto wa kwanza wa kila timu, pamoja na bendera yao mkononi, akimbie hadi mwisho na aseme mstari wa kumbukumbu kwa sauti. Kisha warudi kwa mbio kwenye timu zao wapeane bendera kwa mtoto mwengine na kadhalika. Cheza hadi timu moja – mshindi-akamilishe. Kamilisha kwa kurudia mstari wa kumbukumbu pajoa.

## Kufunga

Ombo pamoja na watoto ukimshukuru Mungu kila wakati kwa kutimiza **ahadi** zake. Ombo kwamba watoto wanaweza kila wakati kumtumainia Mungu katika kutimiza kile **ameahidi**. Ombo kwamba wazazi waweze kuwa mifano bora kwa watoto wanapotimiza **ahadi** zao.

## **Zoezi la 38**

### **MUNGU AFANYA AHADI**

**Maandiko:** Mwanzo 8:20 – 9:19

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba wakati Mungu anafanya **ahadi**, tunaweza kuwa na uhakika kwamba ataitimiza.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Wewe Bwana Mungu wetu una huruma na msamaha.” (Danieli 9:9a)

**Mungu  
alifanya ahadi  
kwa Nuhu na  
watu wake. Je,  
unajua ahadi  
hiyo ilikuwa  
gani?**

## **UTANGULIZI – KITENGO CHA 10**

### **WATUMISHI WA MUNGU WAAMINIFU**

**Marejeleo ya Kibiblia:** Ruthu 1-2, 3-4; 1 Samweli 1:1-2:11, 18-21; 2:12-17, 22-26; 3

**Mstari wa Kumbukumbu wa Kitengo:** “Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)

#### **Malengo ya Kitengo**

##### **Kitengo hiki kitawasaidi watoto:**

- Kuendeleza roho ya utumishi kwa Mungu
- Kujifunza kwamba Mungu anatutaka tuwe watumishi waaminifu
- Kujifunza kwamba Mungu anatumia watumishi waaminifu kutimiza mipango yake duniani
- Kutambua mifano mizuri ya watumishi waaminifu katika Biblia

#### **Masomo ya Kitengo**

**Somo la 39: Ruthu**

**Somo la 40: Boazi**

**Somo la 41: Hana**

**Somo la 42: Samweli**

Mungu anawathamini wale wanaomtumikiwa kwa uaminifu. Ana shukrani kubwa kwa wanaoona mahitaji ya wengine ana wanafanya yasiyowezekana ili kuwapa.

Masom ohaya yanatoa nafsi kwa watoto kulinganisha ubinafsi wa ulimwengu na nia ya kumtumikia Mungu ambayo anatuomba.

Tuweza kuelewa kwamba wale wanaong’ang’ana kumtumikia Mungu. Utumishi kwa wengine huleta furaha miyoni mwetu.

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba  
Mungu anatutaka tuwe watumishi  
waaminifu

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa  
uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo  
makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)

**Jitayarishe Kufundisha**

Watoto uhisi kuthaminiwa na kushukuriwa wakati wanachangia kwa mazoezi ya kila siku.

Watoto uhisi hitaji la kufanya kazi pamoja kuonyesha kwamba wako waaminifu kutekeleza majukumu; wanaanza kuendeleza uwezo wao kuwa watumishi waaminifu. Somo hili litawasaidia kuelewa kile inachomaanisha kuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu.

Watoto wataelewa kwamba Mungu anataka kutumia uaminifu wetu kuwabariki watu wengine.

Pokea watoto kwa furaha na kuwakaribisha wale wanaohudhuria kwa mara kwanza.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Anza darasa kwa kuimba pambio za sifa. Andaa watoto kusikiliza ukweli wa Kibiblia ukitumia baadhi ya mazoezi yafuatayo:

Tamka herufi za uaminifu:

Kabla ya darasa chora kwenye kipande cha ubao au kipande chochote kigumu cha karatasi herufi zote za alfabeti na ukate.

Andika neno “uaminifu” mara mbili na ukate herufi moja. Changanya herufi zote na uziweke kwenye kikapu kikubwa.

Gawa darasa katika timu 2. Ipe kila timu kipande cha karatasi ngumu na gundi. Elezea kila timu wababalishane katika kuchagua herufi kutoka kwa kikapu kikubwa. Lengo ni kutafuta herufi zinazounda neno “uaminifu” na kuzibandika kwenye karatasi zao ngumu. Timu ambayo inakamilisha kwanza itakuwa mshindi.

Uliza: Je, ni katika njia gani ambayo tunaweza kuonyesha uaminifu kwa Mungu? (kuhudhuria kanisa, kuomba, kuwatii wazazi wetu n.k.)

**Ruth**

**u**

Hadithi ya leo ni juu ya Ruthu, mtumishi mwaminifu wa Mungu.

Kila wakati tunasikia neno “Ruthu” piga makofi mara moja.

Kila wakati tunasikia neno “Naomi,” piga makofi mara mbili.

Zamani, wakati watu wa walitawaliwa na waamuzi na wala si wafalme, kulikuwa na njaa katika nchi ya Israeli. Watu hawakuwa na chakula cha kutosha. Kwa sababu hiyo, Elimeleki, mke wake Naomi,

(piga mikono mara mbili) na wana wao wawili walienda kuishi sahemu ya mbali na Moabu. Baada ya muda Elimeleki alikufa. Wanawe wawili wakua na wakaoa wanawake Wamoabu: Ruthu (piga makofu mara moja) na Orpa. Miaka kumi baadaye wana wawili wa Naomi (piga makofi mara mbili, na uendelee vivyo hivyo) pia walikufa. Naomi alihuzunika kwa sababu aliachwa peke yake katika nchi mgeni mbali na nyumbani.

Naomi alimwambia Ruthu (piga makofi mara mbili) na Orpa, “Nitarudi nyumbani kwangu; Nimesikia kwamba Mungu amebariki Israeli na sasa kuna chakula.”

“Tutaenda pamoja na wewe,” mkwe wa Naomi alimwambia.

Naomi alijibu, “Watoto wangu mrudi mkaishi na familia zenu. Mmekuwa wema sasa kwa wanangu na kwangu. Mungu awarehemu na kuwaandalia waume wapya.” Naomi aliwakumbatia kabla hawajaondoka lakini walianza kulia kwa huzuni.

“Mungu awe na wewe!” Orpa alisema akimkumbatia mkwe kwaheri na akaelekea Moabu. “Tazama Ruthu” asema Naomi. “Orpa anarudi kijijini kwao kuwa na familia yake; nenda naye.” “Sitaenda,” Ruthu alisema. “Sitakuacha. Popote uendapo nitaenda na wewe; watu wako watakuwa watu wangu na Mungu wako atakuwa Mungu wangu.”

Wakati Naobi aliona kwamba Ruthu hakuwa anaenda kubadilisha mawazo yake aliacha kumsisitiza. Wanawake wawili walielekea njiani kwenda Israeli na kuwasili Bethlehemu wakati mavuno yalianza. Walipofika Bethlehemu Naomi na Ruthu walichukua muda wa kutazama wavunaji wakikata nafaka. Waliwaona wavunaji wakiwaruhusu watu maskini wawafulate nyuma wakichukua nafaka iliyosalia kwenye nchi. Kwa kukosa chakula, Ruthu alifanya vivyo hivyo. Aliwafuata wavunaji, kwa haraka akichukua nafaka ilioyanguka. Ruthu alijua alihitaji kufanya kazi kwa bidii ili wawe na chakula cha kula.

Wakati Ruthu alifanya kazi bila kusimama, Boazi, mmiliki wa shamba, alikuwa akisimamia mavuno. “Je, huyu mwanamke ni nani?” Boazi alimwuliza msimamizi wa wavunaji.

“Jina lake lilikuwa Ruthu; alitoka Moabu pamoja na Naomi,” msimamizi alijibu. “Ruthu amefanya kazi siku yote bila kupumzika.”

Boazi alienda mahali Ruthu alikuwa akifanya kazi na kusema, “Usifanye kazi katika shamba lingine; mtu anaweza kukuumiza. Ni bora kufanya katika mashamba yangu ambapo utakuwa salama.”

“Wewe ni mkarimu!” Ruthu alimwambia. “Kwa nini umekuwa mkarimu kwa mgeni?”

“Nimesikia jinsi ulivyo mkarimu kwa Naomi!” Boazi alisema.

Wakati Ruthu alirudi nyumbani, alimwambia Naomi juu ya Boazi. “Boazi ni jamaa ya mume wangu,” Naomi alimwambia. “Nafurahi kwamba alikutenda wema. Usiogope kufanya kazi katika mashamba yake; atakulinda.”

*Ruthu alimtii mamake mkwe na kuendelea kukusanya nafaka karibu na watumishi wa Boazi.. Alimtumikia Mungu kwa uaminifu kwa kumsaidia mamake mkwe. Katika njia hii, Mungu anataka sisi tuwe watumishi waaminifu.*

## Kukariri

“Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)

Andika mstari wa kumbukumbu kwenye karatasi nzito na ukate katika vipande kadhaa. Waambie watoto wabadilishane katika kuwiweka herufi pamoja na usome mstari wa Biblia kwa sauti. Andika muda wa kila mtoto anayeweka mstari pamoja.

## Kufunga

Omiba pamoja na watoto kwamba Mungu atawabariki ili wamtumikie kwa uaminifu. Omiba kwamba tuwe waaminifu kwa Mungu ili aweze kutumia uaminifu wetu kuwabariki wengine.

## Zoezi la 39

**Maandiko:** Ruthu 1 na 2

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Mungu anatutaka tuwe watumishi waaminifu

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)



Mwaminifu



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Mungu anawatumia watumishi wake waaminifu kutimizia mipango yake duniani.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)

**Jitayarishe Kufundisha**

Watoto wanafahamu kwamba wanategemea ulinzi wa wazazi wao. Wanajua kwamba wazazi wao wanawapa chakula, mavazi, na paa inayowafunika. Wengi wa watoto wako wanaishi katika nyumba ambayo wanahisi salama, wanashukuru kwa upendo na ulinzi wa wazazi. Baadhi ya watoto watateseka kwa sababu wazazi wao hawatimizi majukumu yao. Inaweza kuwa vigumu kuzungumza na hawa watoto juu ya ulinzi wa Mungu. Ni muhimu kwamba darasa lako, na masomo ambayo watoto wanapokea kanisani, ni njia ambayo Mungu hutumia kuwaonyesha watoto jinsi anawalinda. Tumia hadithi ya Boazi kuwafundisha watoto kwamba Mungu anahitaji watumishi waaminifu na watiifu ambao wako tayari kuwa vyombo vya baraka kwa wengine.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Utunzaji wa Mungu na utoaji kwa Ruth na mama mkwe wake, Naomi ni thihirisho kwa kusoma sura za kwanza za hadithi ya Ruthu. Wasiwasi wa Naomi kwa siku zijazo za mkwewe mdogo ziliibuka katika sura ya tatu. Yoshua aligawa nchi kwa makabilia kumi na mbili ya Israeli. Lakini hakuna mtu aliyemiliki nchi, kwa sababu ilikuwa sehemu ya urithi wa familia. Katika Mambo ya Walawi 25:23, Mungu alisema, “Nchi isiuzwe kabisa, kwa sababu ni mali yangu.”

Ikiwa mtu huyo alihitaji kuuza mali ilikuwa ni wajibu na jukumu la jamaa wa karibu kuinunua ili ibaki katika familia. Naombi alijuwa kwamba Boazi alikuwa wa jamaa yake ya karibu na alitaka achukue jukumu, sio tu kwa ardhi, bali pia kwa Ruthu. Boazi aliwafanya Ruthu na Naombi yale hao wenyewe hawangeweza kupata; aliokoa mali hiyo, akarudisha jina la wanawake hawa, na kutoa kwa maisha yao ya baadaye. Boazi alifuata hatua zote za kidini zilizohitajika za kumsaidia Ruthu na mamake mkwe. Alikuwa mtiifu na alitimiza mapenzi ya Mungu kwa kumchukua Ruthu kama mke wake na kuwa sehemuya kizazi cha Mfalme Daudi.

**Ulinzi wa Upendo**

Tafuata mmea mdogo au picha ya mnyama wa nyumba kwa ajili ya zoezi hili. Waonyeshe watoto wako mmea au picha na ueleze kwamba hivi ni viumbe hai vinavyohitaji ulinzi maalum ili kuishi. Jadili jinsi ya kulinda mimea au wanyama wa nyumbani. Kwa mfano: mmea unahitaji maji na jua, na samaki anahitaji mahali maalum ili kuishi, chakula na maji masafi ili apumue.

*Je, ninini ingetendeka kama ningesa hau kulinda mmea wangu na mnyama wangu wa nyumbani?* (Wangkuwa wagonjwa au kufa).

*Kama tu vile mmea wangu (au mnyama) anahitaji ulinzi maalum sisi pia tunahitaji kulindwa. Hadithi yetu ya Biblia leo inatueleza jinsi Mungu alimtumia Boazi, mtumishi wake mwaminifu, kuwalinda Ruthu na Naomi.*

Tengeneza vikaragosi rahisi ukitumia soksi, mifuko, n.k. vinavyowakilisha Naomi, Ruthu, na Boazi ili kueleza hadithi. Andaa eneo rahisi ukitumia kasha na unaweza kuitumia kwa maonyesho ya baadaye.

## **Boazi Amsaidia Ruthu**

Kila siku Ruthu alienda katika viwanja wa mtu aliyeitwa Boazi kuchukua nafaka. Boaz alikuwa mkarimu kwa Ruthu, alimruhusu ale na wanawake waliomfanyia kazi, na kuhakikisha kwamba wafanyi kazi wake wote waliacha nafaka ya kutosha kwa Ruthu kuchukua. Ruthu na Naomi walimshukuru Mungu kwa kumleta mtu kama Boazi awasadie. Hata hivyo, kulikuwa na jambo ambalo lilimtia Naomi wasiwasi:

Ruthi alikuwa mwanamke mdogo na alihitaji mume ambaye angempenda, amlinde, na kumpa nafasi ya kuwa na familia yake. Siku moja Naomi alizungumza na Ruthu na kusema, "Nakutakia mema. Ningependa sana uwe na familia yako. Boazi ni wa jamaa ya karibu ya familia yetu. Usiku wa leo, atakuwa anatenganisha nafaka katika ghala lake lazima uende umuone. Nitakueleza utakachofanya." Ruthu alivalia mavazi yake mazuri zaidi na kwenda kumtafuta Boazi. Alisubiri hadi Boazi aliacha kufanya kazi na kupumzika. Walipokuwa peke yao ruthu alimwambia, "Wewe ndiwe mlinzi wa familia yetu. Tafadhalii, ningependa unilinde kwa kunioa."

"Usiogope," Boazi alisema. "Nitakulinda. Mimi ni wa jamaa yetu ya karibu na watu wote wanajua wewe ni mwanamke mzuri. Lakini uko na jamaa mwingine wa karibu kuniliko mimi. Nitaenda kumzungumzia asubuhi. Akitaka kukusaidia, utakuwa sawa. Ila sivyo nitakuo na kukulinda."

Asubuhi iliyofuata Boazi alienda kuzungumza na jamaa yake. Alikutana naye na watu wengine kumi wa umri ya juu kwenye lango la mji na kumwuliza mtu huyo kama angetaka kununua sehemu ya arthi iliyokuwa ya Naomi na kumuoa Ruthu.

"Sitaki kunua arthi au kumuoa mkwe wa Naomi," jamaa wa karibu alisema.

Katika Israeli kulikuwa na tamadanuni kwamba watu wawili walifanya mpango juu ya mali kila mmoja alilazimika kuvua viatu vyake na kumpa mwingine. Boazi aliwaeleza wazee na kuwaambia kwa sauti, "Siku hii ninyi ni mashahidi kwamba nimenunu arthi ya Elimaleki, Kilion, na Mahloni. Nimemchukua Ruthu, Mmoabu, ili kumfanya mke wangu. Yeye ni mjane wa Mahloni na nimeamua kumuoa ili kuhifadhi familia."

Mwishowe, Ruthu na Boazi walioana. Baadaye walimpata mtoto mrembo aliyeitwa Obedi. Kila mtu alifurahia sana juu ya kuzaliwa kwa mtoto. Wakati Obedi alikua, alipata watoto na kisha akapata wajukuu. Mmoja wa wajukuu aliua jitu kubwa lililoitwa Goliati. Alikuwa Mfalme Daudi, ambaye alikuwa wa kizazi cha Ruthu na Boazi. Miaka nyingi baadaye mtoto mwingine alizaliwa ambaye pia alikuwa wa kizazi cha Ruthu na Boazi. Mtoto huhu pia alizaliwa Bethlehemu na kulala katika hori la ngo'ombe. Mungu alizawadi uaminifu wa Ruthu na Boazi kwa kuwaruhusu kuwa sehemu ya familia ya Mfalme Daudi, lakini zaidi ya yote, ya Bwana Yesu.

## **Zoezi**

Igiza hadithi ya Ruthu na Boazi

Utahitaji: mavazi ya kufunga, nafaka ya mahindi au ngano, mdoli, na blanketi.

Onyesho la 1. Naomi amwambira Ruthu kwamba aende amtafute Boazi

Onyesho la 2. Ruthu azungumza na Boazi na kumpa nafaka apelike nyumbani

Onyesho la 3. Boazi azungumza na watu katika lango la mji

Onyesho la 4. Ruthu na Boazi waoana

Onyesho la 5. Naomi amlinda mtoto Obedi

## **Kukariri**

"Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea." (1 Samweli 12:24). Tumia maneno uliyounda katika somo lililopita kurejelea mstari wa kumbukumbu. Ficha vipande katika sehemu tofauti ya darasa kabla ya wanafunzi kuwasili. Acha watoto watafute vipande na kuvikusanya pamoja. Kila mmoja anaweza kurudia mstari wa kumbukumbu pamoja. Kama kuna watotot wa kujitolea ambao wamejifunza maneno kwa moyo, waambie wayaseme.

## **Kufunga**

Wakumbushe watoto neno muhimu la kitengo hiki, "Uaminifu". Unda mviringo, shikaneni mikono, na mkamilishe darasa kwa kuimba sifa inayozungumza juu ya uaminifu wa Mungu. Usisahau kuwapa watoto vikaragozi walivyotengeneza leo. Wavitumie kuwaeleza marafiki wao na familia yale wamesoma leo.

## **Zoezi la 40**

### **BOAZI**

**Maandiko:** Ruthu 3 na 4

**Lengo la Somo** Wasaidie wanafunzi kujua kwamba Mungu anawatumia watumishi wake waaminifu kutimizia mipango yake duniani.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)

## **Boazi Amuoa Ruthu**



Boazi alikuwa mwaminifu. Boazi alimtii Mungu. Mungu alimtumia Boazi kumlinda Ruthu na Naomi. Boazi alifanya mambo mangi mazuri.



Mungu, Tafadhalii nisaidie niwe mwaminifu. Nisaidie ili niwasaidie wengine.

Kwa upendo \_\_\_\_\_ Jina lako

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kutumaini katika uaminifu wa Mungu.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)

## Jitayarisha Kufundisha

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utahitaji kutumia katika somo hili na ujaribu kutayarisha darasa kabla ya wanafunzi wako kuwasili.
- Kumbuka kuwakaribisha wageni na kukusanya ujumbe wao wa kuwasiliana na wakati wa wiki.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

**Hana - 1 Samweli 1:1-2:11, 18-21**

Waambie watoto waje na mdoli au vazi la kufunga kutoka nyumbani. Funga vazi lililofungwa katika fundo ili kutengeneza mtoto. Mshike mtoto katika mikono yako na useme: Hadithi ya leo ya Biblia ni juu ya mwanamke anayeitwa Hana. Hana alikuwa na huzuni nydingi sana kwa sababu hakuweza kupata watoto.

Eleza Hadithi ya Biblia wakati kila mtu anashika midoli za watoto.

Hapo zamani palikuwa na mtu aliyeitwa Elkana ambaye alikuwa na wake wawili. Wakazi wa zamani iliruhusiwa kwa mtu kuwa na wake wawili. Mke mmoja aliitwa Penina na mwingine aliitwa Hana. Hana alimpenda Mungu, lakini alikuwa na huzuni sana. Hana alitaka watoto kwa moyo wake wote. Kwa upande mwingine Penina alikuwa na watoto wengi na kila wakati alimdhihaki Hana.

Kila mwaka Hana na mume wake Elkana walifanya safari ndefu ya kwenda kumuabudu Mungu katika hekalu na kutoa dhabihu. Siku moja Elkana akiwa anaomba, Hana alianza kulia. “Mungu, wewe utawala vitu vyote. Tafadhali usinisahau, sikia ombi langu. Tafadhali niruhusu nipate mtoto. Naahidi nitakupa huyu mtoto awe mtumishi wako na nitakupenda milele.”

Ndani ya hekalu kulikuwa na kuhani aliyeitwa Eli ambaye alilinda nyumba ya Mungu. Eli alikuwa ameketi karibu na Hana akimtazama. Hana alipokuwa akiomba kinywa chake kilionekana kusonga bali maneno yake hayakusikika kwa sababu alikuwa akiomba moyoni mwake. Eli alifikiria kwamba Hana alikuwa mlevi wa mvinyo, kwa hivyo alimsongea na kusema na yeye. “Achana na mvinyo.”

“Sijakunyuwa chochote. Nilikuwa nikimuomba Bwana kwa sababu niko na tatizo kubwa na nina huzuni nydingi Hana alijibu.

Eli alimwambia, “Nenda kwa amani na Mungu wa Israeli akujalie kile unachokiomba.”

Hana alipotoka ndani ya hekalu, alijihisi bora kiasi na kutaka kula. Asubuhi iliyofuata baada ya kumwabudu Mungu, Elkana, Hana, na familia yote walirudi nyumbani. Mungu alisikia maombi ya Hana na punde tu Hana alipata mwana wa kiime ambaye alimwita Samweli. Hana alifurahi sana kwa sababu Mungu alikuwa amejibu maombi yake. Muda ulipofika wa kurudi Shilo kumwabudu Mungu na kutoa dhabihu, Hana alibaki nyumbani na mtoto Samweli.

Hana alimwambia Elkana, “Samweli atakapokua, nitarudi Shilo na wewe na kumuacha Samweli

katika hekalu ili amtumikie Bwana kama nilivyoahidi.”

Miaka ilisonga haraka. Ingawa Samweli alikuwa bado mdogo Hana alikuwa tayari kurudi Shilo na kutimiza ahadi yake kwa Bwana. Hana alimpeleka mwanawе mchanga kwеnyе nyumba ya Mungu. Baada ya Elkana kutoa dhabihu yake kwa Hana alimpeleka Samweli kwa Eli.

Hana alisema, “Mimi ni yule mwanamke ambaye nilikuja kumuomba Bwana miaka kadhaa iliyopita nikiomba huyu mtoto. Sasa nimerudi kutimiza ahadi yangu kwa Mungu na kumtoa Samweli kwa utumishi wa Mungu. Mradi tu Samweli anaishi, atakuwa wa Mungu.”

Wakati Hana na Elkana walirudi nyumbani, Samweli alibaki Shilo na kuanza kumsaidia kuhani Eli katika kazi ya hekalu. Ingawa Samweli hakuishi nyumba kwao Hana bado alimpenda na kila mwaka, alimtengenezea vazi mpya na kumpeleka.

Eli alijua kwamba Mungu alipendezwa kwa vile Hana alikuwa ametimiza ahadi yake kwa hivyo alimpa baraka maalum. Mungu alikuwa mkaribu kwake na akampa wana wengine watatu na binti wawili. Alipomwona Samweli akitumika katika hekalu, alikumbuka wakati wote jinsi Mungu alijibu maombi yake.

### **Kukariri**

“Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)

Unda mviringo. Mkizunguka kwa mviringo rudia mstari wa kumbukumbu mara nyingi; neno moja baada ya lingine. Mwambie mtoto kwa wakati mmoja aende katikati ya mviringo na aseme mstari wa kumbukumbu peke yake.

### **Kufunga**

Kwa ufupi rejelea maneno muhimu ya kitengo hiki na ukusanye sada. Watie moyo wanafunzi wako kuwa waaminifu na watiifu kwa Mungu wakati wa wiki wakiomba na kuwatii wazazi na walimu wao. Wakumbushe kwamba darasa linalofuta ni la mwisho katika kitengo hiki kwa hivyo kuhudhuria ni muhimu. Sema kwaheri kwa maombi.


## **Zoezi la 41**

### **HANA**

**Maandiko:** 1 Samweli 1:1-2:11, 18-21

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kutumaini katika uaminifu wa Mungu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)



**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu anatutaka tumsikilize na kumtii katika kila uamuzi tunafanya.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliowatendea.” (1 Samweli 12:24)

**Jitayarishe Kufundisha**

Utiifu ni neno ambalo watoto wanalielewa vizuri. Watoto wamejifunza kwamba wakati wanakosa kutii kunakuwa na matokeo mabaya. Watoto wamejifunza tena kwamba wanapotii kuna tuzo yake. Kuwafundisha watoto kutii ni hatua muhimu ya kuweka hali ya kiasi na nidhamu. Tunapowafundisha watoto kuwatii wazazi na walimu wao, tunawafundisha pia Mungu. Utiifu ni sehemu muhimu ya uaminifu. Samweli alikuwa mtiifu kwa Mungu na kwa sababu hiyo Bwana alimtumia kufanya mambo ya ajabu. Samweli alijifunza kumsikiliza Mungu. Watie watoto moyo wawe wasikilivu kwa sauti ya Mungu na kutii mapenzi yake.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia**

Kabla ya Neno la Mungu kuwepo kwa mtindo wa kuandika Bwana alitumia njia tofauti za kuwasiliana na watu wake; kuitia ndogo, maono, au matukio ya kiasili. 1 Samweli 3:1 inasema, “Kijana Samweli alipokuwa anamtumikia Yehova mbele ya Eli; katika siku hizo neno la Yehova lilipatikana kwa uchache na maono yalikuwa kila wakati.”

Mungu alipata ndani ya Samweli mtumishi mwenye bidii na mtiifu ambaye angeweza kuwasiliana naye, “mtoto Samweli aliendelea kukua, akazidi kupendwa na Mungu na watu” (1 Samweli 2:26). Mwanzo Samweli hakutambua mwito wa Mungu. Ushauri wa Eli wa hekima ulimsaidia Samweli kutambua sauti ya Bwana na kuja la kufanya na ujumbe aliopokea. Samweli aliwasiliana kwa uaminifu ujumbe wa Mungu kwa Eli. Kutoka wakati huo Samweli alitambuliwa na kuthibitishwa kama nabii wa Mungu.

**Sikiliza Mwito!**

Waweke watoto katika vikundi viwili; moja ya ‘mzazi’ na ingine ya ‘mtoto.’ Wafunike watoto macho. Watawanye wazazi darasani kote.

Unaposema “SASA!” watoto wawatafute wazazi wao wakiongozwa tu na sauti ya wazazi. Wale wanaoigiza kama ‘mzazi’ waite hadi ‘mtoto’ wao awapate.

Rudia mchezo mara kadhaa, ukiwaruhusu watoto kubadilishana majukumu.

Angazia umuhimu wa kutambua sauti ya Baba wetu wa mbinguni.

**Sauti Usiku**

Kuhani Eli alikuwa na wana waliotenda mabaya na kuvunja sheria za Mungu. Ingawa wana Eli walijua amri za Mungu, hawakutaka kumtii. Eli alianza kusikia malalamishi juu ya tabia za wanawe wawili. Eli alijaribu kukosoa tabia za wanawe lakini hawakumsikiliza na wakaendelea kutenda maovu maconi pa Mungu.

Wakati huo Samweli aliendelea kukua na kuwa na nguvu katika kumwogopa Bwana.

*Tengeneza vitanda viwili; moja ya Eli na ingine ya Samweli. Chagua vijana wawili waigize hadithi unapoileza.*

Usiku mmoja Eli na Samweli walienda kulala kama kawaida. Punde tu Mungu alimwita Samweli. Samweli alikuwa hajawai kusikia sauti ya Mungu kwa hivyo hakutambua na akafikiria ni Eli aliyekuwa anamwita. Samweli aliamka kwa haraka kutoka kwa kitanda chake na kukimbia mahali Eli alikuwa. “Niko hapa. Uliniita nifanye nini?” Samweli aliuliza.

Eli alijibu, “Sikukuita; rudi ukalale.”

Tena Samweli alisikia sauti ikimwita, "Samweli!"

Samweli alikimbia kwa Eli. "Mwanangu sijakuita. Rudi ukalale."

Mara ya tatu sauti ilimwita Samweli. Eli sasa akagundua kile kilichokuwa kikitendeka; Mungu alikuwa anamwita Samweli. "Rudi kitandani," Eli alimjibu Samweli. "Sauti ikikutia tena sema, "Nena Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikiliza."

Samweli alirudi kitandani. Aliposikia sauti ikimwtia tena alijibu kama vile kuhani alikuwa amemweleza.

Mungu alimpala Samweli ujumbe wa huzuni sana wa Eli. "Mwambie Eli kwamba naenda kuadhibu familia yake. Lazima nitafanya hivyo kwa sababu wana wa Eli walikuwa wanatenda vibaya na Eli hakuwakomesha."

Wakati Mungu alikuwa amemaliza kusema Samweli alirudi kulala hadi asubuhi iliyofuata.

Asubuhi kijana mdogo aliogopa kumweleza Eli yale Mungu alikuwa amemweleza lakini kuhani alimwita ili amweleza ujumbe aliopokea kutoka kwa Bwana. "Nieleze kila kitu Bwana amekwambia. Mungu wetu atakuadhibu vibaya kama utaficha neno lolote kutoka kwangu," Eli aliagiza.

Samweli alipomweleza Eli kila kitu Eli alisikiliza kwa makini. "Yeye ni Bwana na atafanya yaliyo memba," kuhani alijibu.

Mungu alikuwa na Samweli alipoendelea kukua. Aliendelea kuzungumza naye na kumpa ujumbe za Waisraeli. Hivi karibuni watu wote wa Israeli walijua kwamba Samweli alikuwa nabii ambaye Mungu alikuwa amemchagua.

### Rejelea Mchezo

Andika maswali yafuatayo kwa vipande vya karatasi na uvifunge kwa nguvu.

1. Je, wana wa Eli walikuwa wanafanya nini?
2. Je, watu wa mji walimwambia nini Eli?
3. Je, wana wa Eli walifanya nini wakati aliwaambie waache tabia zao mbaya?
4. Je, Samweli alikuaje tofauti na wana wa Eli?
5. Je, Samweli alisikia nini?
6. Je, Samweli alifanya nini wakati alisikia sauti ikimwita?
7. Je, Eli alimwambia Samweli afanye nini akisikia sauti tena?
8. Je, Mungu alimwambia Samweli nini?
9. Je, mama ya Samweli alikuwa nani?
10. Je, Samweli alishi wapi?

Weka kila kikunjo ndani ya baluni isiyo na hewa. (Au weka makaratasi madogo ndani ya kasha au begi.) Puliza baluni na karatasi zikiwa ndani. Waambie watoto wapasue baluni na kujibu maswali.

### Kazi ya mikono

Chapisha Ukarasa za Zoezi za somo la 42 kwa kila mtoto.

*Je, mtoto aliye katika mchoro ni nani? (Samweli)*

Kwa ufupi rudia na watoto kile Samweli alisikia kutoka kwa Mungu. Cheza muziki polepole wakati watoto wako wanapaka picha rangi. Watoto wanaweza kutumia kazi zao zilizokamilika kuzibandika kwenye mlango wao wa chumba cha kulala wakati wanazungumza/kumuomba Mungu hivyo kuepuka kusumbuliwa.

### **Kukariri**

"*...na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.*" (1 Samweli 12:24)

Waambie watoto ambao wamejifunza mstari wa kumbukumbu kwa kukariri waje mbele na wauseme. Peana zawadi kidogo (penceli, pipi, n.k.) kwa wale wanaoweza kusema mstari.

Waalike wazazi wasikiliza watoto wao wakisoma masomo haya manne.

### **Kufunga**

Shukuru kila mtoto kwa kuhudhuria darasa la leo na ufanye kutajwa maalum kwa wale waliohudhuria mwezo wote. Tangaza mada ya kitengo kinachofuta: "Nguvu za Mungu za Ajabu." Omiba ukiwakumbusha watoto kwamba wanapaswa kuwa watumishi waaminifu wasikilivu katika kusikia sauti ya Mungu.


## **Zoezi la 42**

### **SAMWELI**

**Maandiko:** 1 Samweli 2:12-17, 22-26; 3

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu anatutaka tumsikilize na kumtii katika kila uamuzi tunafanya.

**Memory Verse:** “Basi nyinyi mcheni Bwana na kumtumikia kwa uaminifu kwa moyo wenu; kumbukeni yale mambo makuu aliyowatendea.” (1 Samweli 12:24)



**Namsikiliza  
Mungu**

## **UTANGULIZI – KITENGO CHA 11**

### **NGUVU ZA MUNGU ZA AJABU**

---

**Marejeleo ya Kibiblia:** Kutoka 3-4; Kutoka 13:17, 15:2; Kutoka 16:1-17:7; Esta 1:1-4:17; Esta 5-8

**Mstari wa Kumbukumbu wa Kitengo:** “Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.” (Zaburi 46:1)

#### **Malengo ya Kitengo**

##### **Kitengo hiki kitawasaidia watoto:**

- Kutambua kwamba Mungu anazo nguvu zaidi ya shujaa wa filamu na televisheni
- Kujuia kwamba nguvu za Mungu si za kujifanya, bali ni za kweli
- Kujuia kwamba Mungu hukutana na mahitaji ya watoto wake
- Kumtumainia Mungu wakati wa magumu
- Kujifunza kwamba Mungu anazo nguvu za kuwalinda watoto wake kutoka kwa hatari wanayopatana nayo.

#### **Masomo ya Kitengo**

**Somo la 43: Mungu Ampa Musa Misheni Maalum**

**Somo la 44: Mungu Awaokoa Watu Wake**

**Somo la 45: Mungu Akutana na Mahitaji ya Watu Wake**

**Somo la 46: Mungu Awalinda Watu Wake**

**Somo la 47: Mungu Aonyesha Nguvu Zake**

Watoto wanapenda hadith za mashujaa ambao dakika ya mwisho, wanawaokoa “watu wazuri”.

Kama unaweza kuwasilisha hadithi ya Biblia, kwa mashaka na hisia (bila kuzidisha), watoto hawasahau miujiza na maajabu ya Mungu.

Sisitiza hatua zifuatazo:

1. Kando na vitabu bandia vya Batman, Superman, Spiderman, na vingine; wahusika wa Biblia walikuwa wa kweli.
2. Kwa kuelewa tunaye Mungu aliye na nguvu isiyopungukiwa inapaswa kuondoa hofu na kutujaza na tumaini kwake.
3. Haijalishi maisha magumu yanavyoweza kuwa, Mungu anaweza kutusaidia. Hakuna jambo lililo ngumu na Yeye.

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba wakati Mungu anatupatia misheni maalum, atatusaidia kuitimiza.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.”  
(Zaburi 46:1)

## Jitayarisha Kufundisha

Hii ni sehemu ya kwanza katika awamu ya masomo 5 kuhusu nguvu za Mungu za ajabu. Imba wimbo na watoto: *Mungu wangu ni mkubwa, mwenye nguvu na mkuu*

*Hakuna jambo Mungu asiloweza kufanya (kwako!)*

2x

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utahitaji kutumia somo hili na ujaribu kutayarisha darasa kabla ya wanafunzi wako kuwasili.
- Kumbuka kuwakaribisha wageni na kukusanya ujumbe wao wa kuwasiliana na wakati wa wiki.
- Mahudhurio ya Shule ya Jumapili na kuwasili mapema ni muhimu sana. Andaa chati ya mahudhuri ya wanafunzi wako na upeana zawadi kidogo kwa wale wanaohudhuria Jumapili zote 5.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Andika neno “mwujiza” kwenye ubao.

Mwujiza – *tukio la ajabu linalotendeka wakati Mungu anaonyesha nguvu zake na hakuna maelezo mengine.*

Katika kitengo hiki chote tutajifunza juu ya miujiza ambayo Mungu alitenda kuwaweka watu wake huru.

Cheza Yeye ni Nani??

- Je, ni nani alizaliwa na kuishi Misri wakati wa utotonii mwake?
  - Je, familia ya nani ilimficha akiwa mtoto?
  - Je, ni nani alikuwa na dada aliyeitwa Miriamu?
  - Je, ni nani alikua katika jumba la kifalme la Farao hadi alipokuwa mtu mzima?
  - Je, ni nani aliyekuwa mchungaji wa kondoo katika jangwa la Midiani kwa miaka 40?
- Wote waseme kwa sauti: MUSA!!!

Mungu Ampa Musa Misheni Maalum

Katika Kutoka 3 tunasoma kuhusu yaliyomtokea Musa wakati alikuwa akichunga kondoo “**Baa Baa!**”. Kondoo “**Baa Baa!**” walilia wakati Musa aliwaongoza “**Baa Baa!**” kwenye jangwa moto lililokauka. Musa alitaka kuharakisha kwa sababu safari bado ilikuwa ndefu. Kondoo wote “**Baa Baa!**” walikuwa na kiu, wamechoka na joto nyingi. Mwishowe, walifika kwa mlima ambapo wangepumzika kidogo.

Musa aliona kitu ambacho kilimshanga.... kijiti kilikuwa kinawaka moto! Musa alikaribia ili kutazama alipoona jambo lisilokuwa la kawaida – moto hakuwa unachoma kijiti! Musa alichanganyikiwa. Kisha akasikia sauti kutoka kwenye kijiti ikiita jina lake, “MUSA, MUSA!”

Kwa mshangao, Musa alijibu, “Niko hapa.” “Usije karibu,” sauti ilisema. “Vua Viatu Vyako, Kwa

Sababu Mahali Unaposimama ni Mahali Patakatifu”

Kwa haraka, Musa alivua viatu na kusimama wima. Akiwa anatazama kijiti kilichokuwa kikiungua kwa macho makubwa, hangeamini yale aliyokuwa anaona na kusikia. “Mimi ni Mungu Wa Abrahamu, Isaka, na Yakobo,” sauti kutoka kwa moto ilisema. “Ee Bwana!” Musa alisema, akificha uso wake, kwa sababu aliogopa kumwangalia Mungu.

Mungu alisema, “Nimeona Jinsi Watu Wangu Wanateseka Misri. Naenda Kuwaokoa na Kuwapeleka Kwenye Nchi Nzuri Inayoitwa Kanaani. Ninakutuma Kwa Farao Ukawalete Watu Wangu, Waisraeli, Kutoka Misri.” “Mimi?” Musa aliuliza. “Je, kwa nini Farao, mfalme wa Misri, amsikilize mtu kama mimi?” Na Mungu alisema, “Nitakuwa Pamoja Na Wewe. Hii Itakuwa Ishara Kwako. Wakati Utakuwa Umewaondoa Misri, Mtamwabudu Kwenye Mlima Huu.”

Musa aliogopa, “Nitasesma nini kama Waisraeli wataniuliza, ‘Je, Nani aliyekutuma?’

Mungu akasema, ““Mimi Ndimi Niliye’. Waambie Waisraeli ‘Ndimi Niliye Amenituma Kwenu.”

“Je, viongozi wa Israeli wakose kuniamini?” Musa aliuliza “Unashika Nini Mkononi Mwako?”

Mungu aliuliza. “Fimbo,” Musa alijibu.

“Itupe Chini,” Mungu alimwagiza. Musa aliiupata chini na ikageuka kuwa nyoka, na akaikimbia. “Ichukue Kwa Mkia,” Mungu alimwambia Musa. Musa alimshika nyoka na ikarudi kuwa fimbo katika mkono wake.

Mungu akasema, “Hivyo Waisraeli Wataamini Kwamba Bwana, Mungu wa Fathers Zao, Amekutokea.” Kisha Mungu akasema, “Ingiza Mkono Wako Kifuani Mwako.” Hivyo Musa alitii na alipoutoa nje ulikuwa na ukoma! “Sasa Urudishe Kifuani Mwako,” Mungu akasema. “Ukoma umetoweka!” Musa alijibu. Kisha Mungu akasema, “Kama Waisraeli Hataamini Katika Mwujiza Wa Kwanza, Wataamini Mwujiza Wa Pili. Lakini Kama Hawataamini, Chukua Maji Kutoka kwa Mto na Umwage Kwenye Nchi. Maja Yatabadilika Na Kubadilika Kuwa Damu.” “Lakini Mungu, Mimi ni kigugumizi,” Musa alisema. Mungu alijibu, “Je, Si Mimi Niliyekupatia Maneno? Nitakusaidia Kusema na Nitakufundisha Yale Utakayoyasema.” “Aa Mungu, tafadhal, mtume mtu mwagine!” Musa aliomba. Mungu alijibu, “Mchukue Haruni Pamoja Nawe, Yeye Anajua Kuongea. Nitawasaidia Nyote Wawili Kusema na Nitawafundisha La Kufanya. Chukua Fimbo Hii Mkononi Mwako Ili Utende Miujiza Nayo.” Mwishowe, Musa alimtii Mungu. Musa alifanya kila kitu kama vile Mungu alikuwa amemwagiza. Watu walielewa kwamba Bwana alikuwa amesikia maombi yao na angewaweka huru kutoka kwa utumwa.

## Zoezi

*Mungu Hutusaidia!*

Musa alihisi uoga sana wakati Mungu alimwambia amweleze Farao awaake Waisraeli huru kutoka Misri. Joti alikuwa binti mdogo aliyeimba vizuri. Mwalimu wa Joti alimwuliza awaongoze watoto kwa kuimba. Kama tu Musa, Joti alihisi uoga.

Wote Musa na Joti walizungumza juu ya uoga wao kwa Mungu; Musa kibinaksi na Joti kupitia maombi. Mungu aliwaahidi kwamba atakuwa pamoja nao, kuwasaidia. Je, nini kilitendeka? Mungu aliwasaidia kufanya kile aliwaambia wafanye. Waambie watoto wachore picha ya Musa akizungumza na Farao au wachore picha ya Joti akiongoza kwaya ya watoto.

## Kukariri

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.” (Zaburi 46:1) Chora muhtasari wa kichaka kinachowaka na upake rangi na rangi angavu. Kata kadi zilizo umbo kama moto wa moto. Andika neno moja la mstari wa kumbukumbu kwa kila kadi. Changanya kadi na uwape watoto. Waambie watoto wayaweke maneno katika utaratibu sawa kwenye kijiti. Rudia zoezi hili mara kadhaa na watoto tofauti hadi iwe rahisi kwa watoto kuyaweka maneni vizuri. Weka bango mahali panapoonekana kwenye chumba.

## Kufunga

Wakati unasafisha vifaa vya leo, imba:

*Safisha, safisha, kila mtu afanye sehemu yake.*

*Safisha, safisha, kila mtu kila mahali.*

Uliza mahitaji yoyote ya maombi na sifa. Funga kwa muda wa maombi.

“Watoto kumbukeni, Mungu anazo nguvu za kuwasaidia kufanya CHOCHOTE anachowaambia mfanye!

Rudi kwenye Shule ya Jumapili Jumapili Ijayo.”

## **Zoezi la 43**

### **MUNGU AMPA MUSA MISHENI MAALUM**

**Maandiko:** Kutoka 3 na 4

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba wakati Mungu anatupatia misheni maalum, atatusaidia kuitimiza.

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu." (Zaburi 46:1)



*Ninaogopa  
kuimba katika  
kwaya ya watoto.*



*Tafadhalii,  
Mungu, nisaidie  
nisiogope.*



*Mungu wetu  
ni Mkubwa*

Mungu wetu ni Mkubwa



Mungu hutusaidia kufanya yale Anatuambia tufanye

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba  
Mungu anazo nguvu za kutusaidia katika  
mambo magumu

## Mstari wa Kumbukumbu

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu,  
msaada wa karibu wakati wa taabu.”  
(Zaburi 46:1)

## Jitayarishe Kufundisha

Watoto wanapenda hadith ya miujiza. Ukombozi wa kimiujiza wa Waisraeli katika Kutoka 14 utawaruhusu wajifunze mengi juu ya **NGUVU** za Mungu. Watoto wengine wanaweza kuumia katika hali za vita vya kinyumbani au utengano wa wazazi wao. Wengine wanaweza kuwa wanaomba mwujiza utendeke katika familia yao. Kupitia somo hili imarisha ujasiri na imani ya watoto kwamba Mungu anazo **NGUVU** za kuwasaidia kutatua matatizo magumu zaidi.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Chukua rekodi ya mahudhuria kwenye chati yako. Wakumbushe watoto zawadi ambazo watapewa kwa mahudhuria mazuri. Omba. Toa shukrani kwa Mungu kwa wiki iliyokamilika na ile itakayoanza. Wakaribishe wageni. Wasaide watoto wahisi starehe na wengine.

Baada ya miaka mia moja, Waisraeli hatimaye waliwekwa huru kutoka kwa utumwa. Mungu aliwaondoa Misri hadi Kanaani kupitia jangwa moto, lilokauka. Watu wa Israeli walihisi kuachwa na Mungu na wakapoteza imani yao. Walifikiria hata ingekuwa bora wajenge minara na kuteswa na Wamisri! Aliwapitisha jangwani ili kuwalinda na maadui. Mungu hatuachi peke yetu; Yeye huenda mbele yetu kufungua njia. Yeye huenda mbele yetu kufungua njia. Bwana alitumia minara ya mawingu na moto kuwaongoza Waisraeli kupitia jangwani. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba **NGUVU** za Mungu zitakuwepo wakati wote katuongoza na kutusaidia. Tubaki imara katika imani yetu na kumtumaini Mungu kwenda mahali popote anataka twende.

**Mungu Rescues His Watu**

Je, Ni Nani Atanisaidia? Jadili: “Je, ungemwomba nani msaada kama ungefanya hivyo...

- Ulipotea mjini na hungeweza kupata familia yako? (mgeni, mlinzi, au askari.)
- Mtu alijaribu kukuumiza shulen? (mwalimu, mwalimu mkuu, au mfanyakazi wa shule)
- Unajaribu kuunda kitu ambacho kilikuwa kigumu kwako? (wazazi wako, rafiki mkubwa, au ndugu/dada yako mkubwa)
- Ulikuwa na swali juu ya Mungu? (wazazi wako, mchungaji wako, au mwalimu wa Shule ya Jumapili)
- Ulihisi huzuni au kushushwa moyo? (Mungu, wazazi wako, au rafiki yako)”

**Shikwa!**

Wachague 3 watoto. Waambie wale warefu wasimame wakiangaliana, washikane mikono, na kwa upole wamkumbatie mtoto wa tatu katika mikono yao.

Mwambie mtoto wa tatu: “Umekwama. Je, unaweza kupata njia ya kutoka huko, bila kuwaumiza marafiki wako?”

Leo tutasikia juu ya kikundi cha watu amba walinaswa bila njia ya kutokea; walikuwa na uhakika kwamba watakufa na kwamba ni Mungu peke yake angewaokoa. Fungua Biblia kitabu cha Kutoka 13:17. Tumejifunza vile Mungu alimpa Musa misheni maalum na jinsi alimsaidia Musa kuikamilisha.

Leo tutajifunza kile kilichotokea wakati Waisraeli hatimaye walitoka Misri.

### ***Uokoaji kwenye Bahari ya Shamu***

Fikiria kuwa mtumwa, katika nchi geni, ukifanya kazi kwa bidii kila siku, kutengeneza matofari, kubeba mawe mazito – yote chini ya jua kali. Hivyo ndivyo watu wa Israeli waliishi kabla Mungu alimtuma Musa kuwaokoa. Ilimchukua Mungu kuleta mateso mengi kwa Farao kabla ya kukubali kuwaacha waende. Watu wa Israeli walifurahi sana. Mungu alikuwa amewaaahidi atawapeleka kwa nchi nzuri, Kanaani. Kila mtu alimsifu Mungu kwa sababau hatimaye wangkuwa huru kutoka kwa utumwa wa Wamisri. Waisraeli waliondoka kwa furaha na mizigo yao yote. Lakini Mungu hakuwapeleka kwenye nchi ya Kanaani kupitia njia fupi, iliyio rahisi. Mungu aliweka mpango maalum wa kuwaongoza Waembrania kwenye nchi ya Kanaani. Mungu alitoa safu ya mawingu kuwaongoza wakati wa mchana na nguzo ya moto kuwaongoza usiku. Walipofika kwenye ukingo wa Bahari ya Shamu watu hawangeweza kusonga tena. Watu waliweka kambi hapo na hapo ndipo matatizo yalianzia:

“Wamisri wanakuja!” Mtu alipiga kelele.

Farao alikuwa amebadilisha mawazo yake na alitaka watumwa wake warudi. “Wanakaribia! Angalia vumbi magari yao yanainua!” Waisraeli walilia. “Tungebaki Misri!” Wengine walipaza sauti. “Musa, kwa nini ulituleta haka tufe hivi?”

Mungu alikuwa amemwambia Musa kwamba Wamisri watafuata, lakini Musa pia alijua kwamba Mungu alikuwa na **NGUVU ZAIDI**. Musa aliwahakikisha watu waliogopa, “Msiogope; tazama na mtaona – **NGUVU za Mungu** zitatuzuia na hatari!”

Sauti ya farasi na magari ilikaribia! Ilipoanza kuwa usiku Mungu aliweka safu la mawingu katikati ya Waisraeli na Wamisri. Watu wa Israeli wangeweza kuona wakiendelea na safari, wakati Wamisri walikuwa gizani.

Kando ya Bahari ya Shamu Mungu alimwamuru Musa, “**INU A FIMBO YAKO**.” Musa alitii. Upopo ulivuma kwa nguvu hata ikafungua bahari mara mbili, ikiunda pahali pakavu kwa Waisraeli kuvuka. Asubuhi na mapema, Watu wa Israeli walianza kuvuka Bahari ya Shamu.

Walipotazama nyuma Waisraeli waliona kwamba Wamisri walikuwa wakiwafuata! Waliogopa. Kisha wakamuona Musa akisababisha magurudumu ya magari ya Wamisri kukwama na kuvunjika. Wamisri walipiga kelele, “Tuwaepuke Waisraeli; Mungu wao anapigana juu yetu!”

Watu wa Israeli walipofika salama upande mwininge wa kingo, Mungu alimwambia Musa ainue fimo yake tena. *Waaa!* – maji yalirudi kwenye sahemu zao. Bahari iliwafunika askari wote Wamisri, farasi zao, na magari yao. Kupitia **NGUVU** kuu za Mungu, aliwaokoa watu wake. Musa na watu wake wote walimsifu Mungu na kusherehekeea: “*Mungu ni nguvu yangu na wimbo wangu, kutoka kwake kuna wokovu. Yeye ni Mungu wangu. Namsifu.*”

### **Zoezi**

#### ***Uokoaji wa Ajabu***

Je, ni katika njia gani ambayo Mungu aliwakoa Waisraeli? Je ni nini kilifanyika kwa Wamisri? Je, ni nini kilisababisha maji ya bahari kufunguka mara mbili?

Jaza nafasi zilizo wazi na maneno haya: **NGUVU, OMBA, HUZUNI, MUNGU, BORA**

Jadi na Benta walikuwa na \_\_\_\_\_. Mama yao alikuwa mgonjwa. Baba yao alisema, “\_\_\_\_\_ anazo **NGUVU** za kumsaidia mama.” Jadi, Benta, na Baba \_\_\_\_\_ mama yao, “Tafadhali, Mungu, msaidie Mama ahisi \_\_\_\_\_. ” Mama hakuhisni bora haraka. Jadi, Benta, na Dad waliendelea kuomba. Siku moja baba aliletu habari njema, “Mama yuko bora kiasi, atarudi kwa hali ya kawaida hivi karibuni.” “Nafurahi kwamba Mungu anazo \_\_\_\_\_ za kutusaidia! Asante!” Jadi, Benta, na Baba walisema.

### **Kukariri**

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.” (Zaburi 46:1) Jaribu kutafuta picha ya ngome kutoka kwa kitabu au jarida uwaonyeshe watoto. Enzi za zamani, wafalme walijenga ngome hizi ili kujilinda dhidi ya maadui. Walitumia mawe makubwa kujenga kuta kubwa ili hakuna mtu angeweza kuingia. Wakati wa vita, walio ndani ya ngome walikuwa salama. Vivyo hivyo, mstari wetu wa kumbukumbu katika kitengo hiki unatukumbusha Mungu ni kimbilio na nguvu yetu. Tusiogope. Kusanya mawe. Jenga ngome yako. Andika mstari wetu wa kumbukumbu kama ukumbusho.

### **Kufunga**

Mshukuru Mungu kwa yale watoto wamejifunza. Waalike kwa darasa la wiki linalofuta wajifunze mengi juu ya **NGUVU** za Mungu.

## Zoezi la 44

### MUNGU AWAOKOA WATU WAKE

**Maandiko:** Kutoka 13:17-15:2

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu anazo nguvu za kutusaidia katika mambo magumu

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu." (Zaburi 46:1)

**"Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu."**  
**(Zaburi 46:1)**



## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu hukutana na mahitaji ya watoto wake. Amini **NGUVU** zake, usilalamike.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.”  
(Zaburi 46:1)

## Jitayarisha Kufundisha

Kwa muda mrefu, Mungu alitulinda, sisi watoto wake. Kama vile Mungu amekutana na mahitaji yetu, tunajifunza kuamini **NGUVU** zake za ulinzi zaidi.

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utahitaji kutumia somo hili na ujaribu kutayarisha darasa kabla ya wanafunzi wako kuwasili.
- Kumbuka kuwakaribisha wageni na kukusanya ujumbe wao wa kuwasiliana na wakati wa wiki.
- Chukua rekodi ya mahudhurio kwenye Chati yako ya Mahudhurio – kumbuka kwamba baada Jumapili 5 zawadi za mahudhurio zitapeanwa!

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Waambie watoto waketi katika mviringo kwenye sakafu na wafunge macho yao. Tupa pipi zilizofungwa karibu na watoto. “Watoto, kwa hesabu ya watatu mnawenza kufungua machoyenu, na kuchukua pipi moja kila mtu. Kama utachukua zaidi ya moja, utapoteza zote. MOJA, MBILI, TATU – FUNGUA MACHO YAKO!”

Baada ya watoto kuchukua pipi, waulize: “Je, kuna ye yeyote aliye na pipi moja? Kama mtu ana pipi **moja** au zaidi, mwambia akurudishie pipi zote walizo nazo.”

“Je, ilikuwa vigumu kufuata maagizo yangu na kuchukua pipi **moja** tu?”

“Ni muhimu kufuata maagizo, la sivyo tunaweza kuwa na matatizo.”

Waisraeli walikuwa na shida kufuata maagizo ya Mungu.

Let kipande cha mkate uliozeeka na kuwa na ukungu kiasi.

“Wakati mwingine tunaenda dukani, tunaweza kununua mkate zaidi ya ile tunakula. Wakati mkate unazeeka hupata ukungu na kunuka. Singependa kula huu mkate, je wewe?

Katika hadithi ya leo tutasikia juu ya baadhi ya watu ambao hawakufuata maagizo na jambo mbaya likatendeka kwa chakula chao:

Somo la leo linazungumzia njia maalum ambazo Mungu alilinda watu wake wakati walikuwa jangwani wakielekea Kanaani, Nchi Ya Ahadi. Waulize watu wawili wadogo katika umati wako waigize mchezo ufuatao kwa watoto. MUSA anafaa kuva vazi na kubeba fimbo. MUNGU aanapaswa kuwa na sauti kubwa, lakini ajifice machoni pa watoto.

MUSA: “Kuondoka kwetu kwa miujiza kutoka Misri kupitia Bahari ya Shamu kulikuwa tu mwanzo wa safari ndefu kwetu Waisraeli. Mungu alituongoza kutoka sehemu moja hadi nyingine kupitia jangwa la joto. Wakati mwingine hapakuwa na maji ya kutosha. Hilo lilipotokea, watu walilalamika. Laiti wangemtumainia Mungu badala ya kulalamika kila wakati!

Wakati mmoja Mungu alitupeleka mahali pazuri palipoitwa Elimu. Hapo tulipata miti nyingi ya

*mitenda na maji. Baada ya hiyo tulisafiri kwenda Jangwa la Dhambi ambapo tulikosa chakula. Watu walilalamika tena, ‘Kwa nini Mungu hakutuacha tukae Misri ambapo tulikuwa na chakula. Hapa tutakufa!’  
Nilimuomba Mungu, na akaniambia:’*

MUNGU: “Nitawatumia Wote Mkate Wangu Maalum Ambao Utashuka Kutoka Angani Kila Asubuhi. Nitatuma Kware Mchana Ili Kuwapa Nyama Ya Kula. Kila Asubuhi Kusanya Chakula Ya Kila Mtu Katika Nyumba Zenu – Ya Kutosha **Tu** Kwa Siku Hiyo. Usichukue Kitu Kingine Chochote. Siku Ya 6 Ya Wiki Mtakusanay Mara Mbili Ili Muwe Na Chakula Cha Kutosha Kwa Siku Ya Sabato.”

MUSA: “Kama tu vile Mungu alivyotuambia, asubuhi iliyofuata tulipata vipande vyta mkate (mana) karibu nasi. Ilikuwa tamu, kama asali. Tulifurahi sana. Lakini wengine wetu hawakufuata maagizo ya Mungu. Wengine walichukua mana zaidi kuliko ilivyo hitajika siku hiyo. Asubuhi iliyofuata kulikuwa na harufu mbaya na minyoo katika hema letu kutoka mkate uliooza. Siku ya sita tulihitajika kukusanya mana ya kutosha ya siku mbili. Tena, wengi hawakufuata maagizo ya Mungu. Siku ya Sabato hawakupata mana na wengine wakaachwa na njaa. Mungu aliwapa mana kutoka mbinguni siku sita za wiki kwa siku arobaini ambazo tulikaa jangwani.

Siku ilifika wakati tulipaswa kusonga. Tulisafiri na hatimaye tukapiga kambi katika Refidimu; sehemu hii haina maji! Tena, watu walilalamika wakiniliza kwa nini alikuwa alituleta hapa kufa. Tena, niliomba kumwuliza Mungu msaada wake. Mungu aliniambia niwapeleke viongozi wa Watu wa Israeli kwenye Mlima wa Horebu na kupiga jiwe fulani kwa fimbo yangu. Nilitii na, sasa maji masafi yalitiririka kutoka kwa mawe. Kama tu ilivyo Mungu wetu mkuu aliwaonyesha watu kwamba alikuwa na NGUVU na utawala juu ya kila kitu!”

### Zoezi

*Mungu Hutimiza Mahitaji!*

Chora vitu ambavyo Mungu amewapa watoto.

Kama tu vile Musa alimwuliza Mungu akutane na mahitaji ya Watu wa Israeli tunaweza kufanya hivyo.

Mchague mtu awe katibu wa darasa. Mwambie katibu aandike rekodi yoyote ya mahitaji ya maombi ambayo darasa liko nayo. Wiki zinazofuata, mwambie katibu aandike rekodi jinsi Mungu amejibu mahitaji ya maombi ya darasa lako.

### Kukariri

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.” (Zaburi 46:1) Waambie watoto wasimame katika mviringo na warudi nyuma. Kwa kila hatua wanafaa kusema neno la mstari wa kumbukumbu. Rudia.

### Kufunga

Ombo ukitoa shukrani kwa Mungu kwa vipaji na ulinzi wake. Kama wanafunzi eleza sifa zao na mahitaji ya maombi. Katibu wa Darasa anapaswa kuandika chini. Kila wakati mshukuru tunapopokea majibu ya Bwana. Kumbuka jinsi Mungu yuko pamoja nasi, kila wakati akitulinda, na kila wakati akitusaidia katika kila hali. Mtumainie Bwana; Yeye yuko nasi kila wakati.

Ongeza hitaji hili la maombi kwa orodha ya maombi ya darasa: Waombee watu wote ulimwenguni wanahojitaji chakula na maji masafi ya kunywa.

Waalike watoto waje darasani tena Jumapili ifuatayo wajifunza mengi zaidi juu ya **NGUVU** za Mungu!

## **Zoezi la 45**

### **MUNGU HUKUTANA NA MAHITAJI YA WATU WAKE**

**Maandiko:** Kutoka 16:1-17:7

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu hukutana na mahitaji ya watoto wake. Amini **NGUVU** zake, usilalamike.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.” (Zaburi 46:1)

**Je, Mungu ametupatia  
nini ingine?**

**Chora kitu ambacho Mungu amekupatia.**

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kumtumaini Mungu, hata katika wakatu mgumu.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.”  
(Zaburi 46:1)

## Jitayarisha Kufundisha

**NGUVU** za Mungu wetu ni bora! **NGUVU** za Mungu wetu hutusaidia, zinatulinda, zinatupatia ujasiri wa kumtumainia. Katika somo hili lote, tutajifunza kumtumainia Mungu wakati wowote tunahisi kuwa katika shida.

- Andaa mapema vifaa vya mafundisho ambavyo utahitaji kutumia katika somo hili na ujaribu kutayarisha darasa kabla ya wanafunzi wako kuwasili.
- Kumbuka kuwakaribisha wageni na kukusanya ujumbe wao wa kuwasiliana na wakati wa wiki.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Mwalimu, kabla ya darasa soma Esta 1:1-4:17.

Changanya Herufi

Andika kwenye ubao herufi zifuatazo: TSAE.

“Jaribu kupanga herufi kutafuata jina la mhusika wa Biblia ambaye tutajifunza katika masomo mawili yanayofuata,” (ESTA)

Taji

Weka vitu kadhaa vya mikono ambavyo unavyo. Weka ukanda wa karatasi (sentimia 15 au zaidi) kwenye kichwa cha kila mtoto. Weka alama mahali ambapo kipande lazima kilingane ili taji itoshee kichwa cha mtoto vizuri.

“Andika jina kando ya karatasi yako na utengeneze upande mwagine taji nzuri.”

Unganisha mwisho wa ‘taji’ na mkanda.

“Je, ni nani hutumia taji?” (wafalme na malkia.)

“Je, wafalme na malkia hufanya kazi gani?” (wanatawala nchi, huwasaidia watu, wanahakikisha kila kitu kinafanya kazi vizuri, n.k.)

Katika Hadithi ya leo ya Biblia tutajifunza kuhusu Mfalme Ahasuero na Malkia Esta.

Tutajifunza kuhusu mwanamke hodari aliyemtumainia Mungu kuwasaidia watu wake; jina lake lilikuwa Esta.

Mfalme wa Uajemi, Mfalme Ahasuero, aliweka karamu. Aliwaalika maafisa wote muhimu wa ufalme waje ili waone Malkia mrembo Vashti. Lakini Malkia Vashti alikataa kuhudhuria!

Mfalme Ahasuero alikasirika sana na akaenda kwa washauri wake, “Je, nitafanya nini na malkia? Hakunitii na kuhudhuria karamu!”

Washauri wa Mfalme Ahasuero walijibu, “itakuwa bora kumtafuta mwanamke mwagine atumike kama malkia. Usimruhusu Vashti abaki kama malkia.”

Mfalme alifikiria hili lilikuwa wazo bora na akaanza kumtafuta malkia wa baadaye.

Kulikuwa na mtu Myahudi aliyeishi Uajemi ambaye alikuwa na mpwa mrembo. Aliitwa Mordekai naye

mpwa aliiwa Esta. Siku moja watumishi wa Mfalme Ahasuero walienda katika nyumba ya Mordekai na wakamuona Esta. "Alikuwa mrembo sana! Tumpeleke kwenye nyumba ya kifalme."

Esta hakuwa na la kufanya ila kwenda katika nyumba ya mfalme. Kila siku Mordekai alienda kwenye bustani za nyumba ya kifalme kumwangalia mpwa wake. Mfalme Ahasuero alifurahia kuwa na malkia wake mpya.

Siku moja Mordekai alienda kumwangalia Esta alisikia askari wawili wakipanga kumwua Mfalme Ahasuero. Mordekai mara moja alienda kumuona Esta na kumwambia kila kitu alichokisikia.

Katika ufalme wa Mfalme Ahasuero kulikuwa na afisa mmoja ambaye aliiwa Hamani. Mfalme Ahasuero alimpenda Hamani sana hata akawaamuru watu wote kumpigia Hamani magoti. Mfalme Kila mtu alifanya hivyo, ila tu mtu mmoja ... Mordekai. Mordekai alikataa kupiga magoti mbele ya Hamani kwa vile alikuwa Myahudi na angepiga tu magoti mbele ya Mungu.

Hamani aikuwa na hasira, "Kama adhabu nitamwua Mordekai na watu wa Kiyahudi wote!" Hamani alifikiria mpango na kwenda mbele ya Mfalme Ahasuero, "Watu wa Kiyahudi hawana heshima kwako na hawatii sheria zako! Ningependa kuwalipa watu wawawue watu wa Kiyahudi."

"Okoa pesa yako," mfalme alisema. "Hapa kuna hii pete ambayo itafanya mpango huu kuwa rasmi ya kwamba wewe na mimi tumena. Fanya utakavyo na hao watu!"

Hivyo, Hamani aliandika sheria mpya: "Tarehe 13 ya mwezi wa 12, watu wote ni lazima wawaue Wayahudi watawapata na kuchukua mali yao." Hamani alitia alama sheria na pete ya mfalme na kuituma kwa mikoa yote.

Wakati Mordekai alisikia habari hizi, alikasirika sana, akafunika kichwa chake na majivu, na kuvalia mavazi yaliyozeeka. Watumishi wa Esta walimwambia, "Mjomba Mordekai yuko nje analia na anataka kukuona. Aliniambia nikwambie kuhusu amri iliyotolewa juu ya watu wa Kiyahudi. Mordekai alimuomba Esta azungumze na mfalme amuombe usaidizi.

Esta alilia, "Siwezi kwenda. Nikienda bila mwaliko, Mfalme Ahasuero ataniua!"

Mordekai alisisitiza, "Ukinyamaza tutakufa, hata wewe. Na nani anayejua bali umeingia katika kiwango cha ufalme kwa wakati kama huu?"

Esta alimwuliza Mordekai na watu wengine wa Kiyahudi wasile chochote kwa siku tatu, lakini mwombee. Esta alimlilia Mungu kwa usaidizi. Mordekai, Esta, na watu wa Kiyahudi waliomba na kufunga kwa siku tatu.

Je, nini kingewatendekea? Je, mtu angesimamisha mpango wa Hamani mbaya? Hakikisha umerudi wiki ijayo kusikia hadithi iliyosalia!

## Zoezi

### Siogopi

"Chora picha, au andika hadithi juu ya kitu ambacho unaogopa."

Waambie watoto waeleze michoro yao. Zungumza juu ya uoga wao na utumie hadithi ya Esta kuwatia moyo wamtumainie Mungu. Weka kikapu au ndoo ya taka katikati mwa darasa.

"Kila mmoja apite karibu na kikapu na urarue mchoro wako wakiona, 'Siogopi. Namtumainia Mungu.'"

## Kukariri

"Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu." (Zaburi 46:1) "Kila mtu afunge macho yake." Andika mstari wa kumbukumbu kwenye ubao. "Watoto, fungueni macho yetu na msome mstari kwa sauti."

"Fungeni macho yenu tena." Futa baadhi ya maneno.

"Fungeni macho yenu na mjaribu kusema mstari wote." Rudia zoezi ukifuta maneno kila wakati hadi maneno yote yafutwe na kwa pamoja mnawenza kusema mstari wote wa Biblia kwa akili.

## Kufunga

Je, ni nani alimtumainia Mungu katika hadithi yetu ya leo? (Esta) Esta alimtumainia Mungu amsaidie kumwendea Mfalme Ahasuero.

Mtumainie Mungu wiki hii. Zungumza na familia yako kuhusu kile mmejifunza katika Hadithi ya leo ya Biblia. Wiki ijayo tutapata kusikia hadithi yote ya Malkia Esta na NGUVU za Mungu. Usikose!

## **Zoezi la 46**

### **MUNGU AWALINDA WATU WAKE**

**Maandiko:** Esta 1:1-4:17

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kumtumaini Mungu, hata katika wakatu mgumu

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu." (Zaburi 46:1)

**Ninaweza kumtumainia  
wakati  
wote nahitaji msaada.**

Ninaweza kumtumainia \_\_\_\_\_ wakati wote nahitaji msaada.

Malkia Esta



## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba  
Mungu anazo **NGUVU** za kuwalinda  
watoto wake kutoka kwa hatari.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu,  
msaada wa karibu wakati wa taabu.”  
(Zaburi 46:1)

## Jitayarishe Kufundisha

Watoto wanapenda mashujaa wanaoweza kuwashinda maadui kwa kupaa, kuwanyamazisha maadui wao, kutoonekana, kuona kupertia kwa ukuta, n.k. Wakati mwingine watoto hata hujifanya kuwa hao mashujaa.

Watoto wanahitaji kujifunza kwamba ni Mungu pekee yake aliye na **NGUVU** za kufanya chichote kuu. Mungu anataka kutumia **NGUVU** zake kupertia kwetu kufikia ulimwengu unaoishi katika giza. Muombe Roho Mtakatifu awasaidie watoto kuelewa **NGUVU** za Mungu ni zaidi ya ufahamu na ziko kwa wote wanaomtumaini Mungu.

Zawadi za Shukrani za Mahudhurio ya Uaminifu! – Kwa vile hili ni somo la mwisho la kitengo hiki – **NGUVU ZA MUNGU ZA AJABU**, peana kitu kama kadi ndogo za shukrani au mistari ya Biblia kwa watoto kuwashukuru kwa mahudhurio ya uaminifu.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Katika hadithi ya leo Esta yuko karibu kufika mbele ya mfalme na yuko tayari kwa lolote litakaloweza kutokea kwake. Sheria ilisema kwamba mtu ambaye hajakaribishwa akimwendea Mfalme Ahasuero (awe ni Malkia Esta au la) walinzi walipewa amri kali ya kumwua mtu huyo. Jambo pekee ambalo lingewasimamisha walinzi lilikuwa kama mfalme alipeana fimbo yake kwa mgeni.

Malkia Esta: Ili kutimiza kusudi lake la uungu Mungu alichagua kufanya kazi kupertia mwanamke mdogo wa kawaida, Esta. Utiifu wa ujasiri wa Esta kwa Mungu uliokoa maisha ya watu wa Kiyahudi. Mordekai: Mordekai alitumainia **NGUVU** za Mungu na kukataa kuinama mbele ya Hamani mwovu. Imani ya mjomba Mordekai ilimtia Esta moyo wa kumtii Mungu.

## Fuata Maagizo ya Mfalme!

Katika mchezo huu waalimu watawakilisha mfalme na watoto watumishi wao. Watoto wasimame upande-kwa-upande, bega-kwa-bega katika mstari laini. Mfalme awaangalie watoto, akiwa mbali kidogo. Mfalme aamrishe watumishi wake, kwa mfano: “Sam, chukua hatua tatu ndogo mbele,” “Mary, chukua hatua 4 za kuruka nyuma,” n.k. Mfalme au malkia anaweza pia kuuauliza watumishi kuruka, warudi nyuma, n.k. Mtumishi anatii magizo ya mfalme. Rudia mchezo mara kadhaa.

## Esta 5-8

Kabla ya darasa, andika kwenye ubao wa ishara: ‘MUNGU ANATAWALA!’

“Je, nani anaweza kukumbuka kile tumejifunza wiki iliyopita kutka kwa hadithi ya Malkia Esta; Esta 1-4? Tunapoendelea na hadithi, wakati ninaonyesha maneno haya, seme kwa sauti: MUNGU ANATAWALA!”

*Esta alikuwa mtu wa kufikiria sana; mwisho alisimama na kusema, “Lazima nimtafute mfalme.” (Onyesha maneno, “MUNGU ANATAWALA!”) Esta alikuwa akiomba na kufunga. (MUNGU ANATAWALA!) Hakuna aliyeruhusiwa kwenda kumuona mfalme bila mwaliko. Bado Esta alijua Mungu yuko pamoja na yeye na baada ya siku 3 alienda kumuona mfalme. (MUNGU ANATAWALA!)*

*Mfalme Ahasuero alifurahi sana kumuona Esta mrembo na akampa ruhusa aseme na yeye. Alimgusa Esta kwa fimbio yake akiyaokoa maisha yake. (MUNGU ANATAWALA!)*

*Mfalme Ahasuero aliuliza, “Je, kuna tatizo gani mfalme? Niombe chochote utakacho nami nitakupa ... hata kama ni nusu ya ufalme wangu!” (MUNGU ANATAWALA!)*

*Esta alijibu, “Mfalme Ahasuero, Nimeandaa karamu kwa ajili yako na kwa Hamani. Je, utakuja?” Mfalme na Hamani walikuwa na wakati mzuri sana kwenye karamu ya malkia! (MUNGU ANATAWALA!) Wakati fulani jioni mfalme aliuliza, “Esta, je, nikufanyie nini?”*

*Esta alijibu, “Naomba nikuulize jambo muhimu. Tafadhli mlete Hamani pamoja nawe tena kwa chakula cha jioni kesho usiku na kisha nitalijibu swalil lako.”*

*Hamani aliringa sana kuandamana na mfalme! Akilini mwake alikumbuka jinsi Mordeka alikuwa amekataa kumwinamia, ‘Je, Mordekai anafahamu ukuu wangu!!!’*

*Hamani alimringia mke wake, “Malkia Esta alikuwa amenialika kwenye karamu! Mimi ni mtu mkuu! Ni lazima nifikirie njia ya kumuonyesha Mordekai ukuu wangu!*

*“Mwambie tu Mfalme Ahasuero amwue Mordekai!” mke wa Hamani alipendekeza.*

*Hamani alipenda mpango wa mke wake kwa hivyo alikuwa na mbaao kubwa iliyokuwa imejengwa tayari kumsulubisha Mordekai.*

*Usiku huo Mfalme Ahasuero angeweza kulala. Alimwuliza mmoja wa watumishi wake alete Kitabu cha Mambo ya Walawi cha Kifalme amsomee. (MUNGU ANATAWALA!) Wakati mtumishi wa mfalme alisoma sehemu ambayo Mordekai alikuwa amesaidia kuokoa maisha ya mfalme, Mfalme Ahasuero aliuliza, “Je, tulifanya nini kumzawadi Mordekai kwa kuyaokoa maisha yangu?”*

*“Hakuna Bwana,” mtumishi aliuliza. Kisha Mfalme Ahasuero alisikia kelele na kuuliza, “Je, ni nani aliye uwanjani?” “Ni Hamani,” mtumishi aliuliza.*

*Mfalme Ahasuero aliamuru Hamani aingie ndani naye mfalme aksauliza, “Hamani, je, tutamzawadi nini mtu ambaye mfalme anataka kumheshimu?”*

*Hamani alifikiri mfalme alikuwa anamaanisha kumtukuza yeye, “Mpe mavazi mazuri, farasi mwenye nguvu, na umvishe taji ili wote waone.” Mfalme Ahasuero alijibu, “Hilo ni wazo nzuri sana, Hamani. Fanya haraka na uyatende hayo yote kwa Mordekai.”*

*Hamani alikasirika sana, lakini alifanya kila kitu ambacho mfalme alimwambia.*

*Jioni hiyo watumishi walifika kumpeleka Hamani kwenye chakula cha jiono pamoja na mfalme na malkia. (MUNGU ANATAWALA!) Walipokuwa kwenye karamu mfalme aliuliza Esta tena hitaji lake lilikuwa gani. Esta alisema ombi kwa Mungu; alikiri mbele ya mfalme kwamba alikuwa Myahudi na jinsi alikuwa amehatarisha maisha yake na yale ya watu. (MUNGU ANATAWALA!) Esta alimwomba tafadhali abadilishe sheria.*

*Mfalme alifanya kile Esta alimwomba na kutengeneza sheria mpya ya kuwaweka watu wa Kiyahudi salama. (MUNGU ANATAWALA!) Hamani aliadhibiwa kwa matendo yake maovu kwenye mbaao ile ile alikuwa amejenga kwa ajili ya Mordekai. Mordekai na watu wa Kiyahudi walikuwa na sherehe kubwa wakimsifu Mungu. Mungu alikuwa amewaokoa kutoka kwa kifo fulani. (MUNGU ANATAWALA!)*

## Zoezi

### NGUVU kuu za Mungu

Keti katika mviringo na mvae taji iliyotengenezwa katika somo lililopita. Fikiria kwamba sisi ni wafalme au malkia. Kama tu vile Malkia Esta aliwasaidia watu, zungumzia jinsi tunaweza kuwasaidia watu. Hata kama hatutakuwa wafalme au malkia wenye nguvu, tunaweza kuwasaidia majirani, kwa mfano: kuokota taka kutoka kanisani, kumsaidia mtu mzee, kusaidia na kazi za nyumbani, n.k.

## Kukariri

“Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu.” (Zaburi 46:1) Zungumza na mchungaji wako au kiongozi wa Huduma ya Shule ya Jumapili juu ya kuwapa watoto nafasi ya kusema mstari wao wa kumbukumbu katika ibada ya kuabudu.

## Kufunga

Watie moyo watoto wamtumainie Mungu katikati ya matatizo. NGUVU za Mungu ni kuu kuliko kitu kingine chochote. NGUVU za Bwana ziko kwa wote wanaomtumaini na kumtii.

## Zoezi 47

### MUNGU AONYESHA NGUVU ZAKE

**Maandiko:** Esta 5 - 8

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu anazo **NGUVU** za kuwalinda watoto wake kutoka kwa hatari.

**Mstari wa Kumbukumbu:** "Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu, msaada wa karibu wakati wa taabu." (Zaburi 46:1)



**Tumia maneno katika kasha la neno kukamilisha sentensi.**

1. **alifanya kazi**

**kupitia kwa Esta ili kuwaokoa watu wake.**

2. **ya Mungu**

**inaweza kufanya kazi kupitia kwangu.**

3. **Ninaweza**

**katika nguvu za Mungu wakati wote na kila mahali.**

## **UTANGULIZI – KITENDO CHA 12**

### **HADITHI YA KRISMASI**

---

**Marejeleo ya Kibiblia:** Mathayo 1:18-25; 2:1-12; Luka 1:26-38, 2:1-20; Yohana 3:16; 1 Yohana 4:9

**Mstari wa Kukariri wa Kitengo:** “Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yejote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

#### **Malengo ya Kitengo**

##### **Kitengo hiki kitawasaidia watoto:**

- Kuelewa umuhimu wa kumtii Mungu
- Kuelewa kwamba kila mtu anahitaji Mwokozi, Yesu Kristo
- Aamshe ndani yao roho ya uinjilisti
- Kuelewa kwamba Mungu hufurahia sifa na ibada za watoto wake

#### **Malengo ya Kitengo**

**Somo la 48: Zawadi ya Utiiifu**

**Somo la 49: Zawadi ya Mwokozi**

**Somo la 50: Zawadi ya Sifa**

**Somo la 51: Zawadi ya Kuabudu**

Msimu huu wa Krismasi tujifunze, au tukumbushwe:

- Kwamba wakati tunatii uongozi wa Mungu mambo huenda vizuri kuliko wakati tunakosa kutii.
- Kuzungumza juu ya Yesu na marafiki au watu wa jamaa yako ambao hawamjui Bwana.
- Kwamba bila Mungu maisha yetu yako tupu, ya huzuni na bila tumaini.
- Kwamba Mungu anataka tuwe na muda na yeye kila siku.
- Kwamba Mungu anapenda kusikia maneno ya kuabudu na shukrani kwa baraka nyingi anatumwagia katika maisha yetu.

## Lengo la Somo

## Mstari wa Kumbukumbu

Help the wanafunzi to wish to obey Mungu.

“Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili ye yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

## Jitayariske Kufundisha

Tumesikia hadithi ya Krismasi mara nyingi hata inaonekana kuwa ya mazoea na kawaida. Kinyume, mwujiza wa Krismasi ni hadithi ya watu wawili wanaojulikana wakitii mwito wa Mungu juu ya maisha yao. Utiifu wako hakuwa rahisi. Walikuwa wanadamu na waliogopa.

Hadithi ya Maria:

Katika Luka 1:26-38 Mariamu alisikia kutoka kwa Malaika Gabrieli kwamba atakuwa mama wa Mwana wa Mungu wa pekee. Mariamu aliogopa kuzaa mtoto “maalum” kama huyo. Pia, Mariamu hakuelewa angekuwaje mjaa mzito kwa vile hakuwa ameolewa. Gabrieli kwa utulivu alimweleza jinsi Mungu angefanya mwujiza huu kupitia Roho Mtakatifu. Mariamu aliamini ujume wa Malaika, akakubali kumtii Mungu, na kukubali jukumu lake katika mpango wa Mungu.

Hadithi ya Yusufu:

Katika Mathayo 1:18-25 Yusufu alikuwa na tukio kama hilo la Mariamu. Wakati ujaa uzito wa Mariamu ulithibitishwa Yusufu alijua kumuoa kungeleta aibu ya wazi kwa hivyo alilazimika kukatiza uchumba wao. Lakini katika ndoto malaika alimwelezea jinsi mambo haya yalikuwa mpango wa Mungu kwao na kwa ulimwengu wote. Wakati Yusufu aliamka, alijua alihitajika kumtii Mungu na kumkubali Mariamu kama mke wake.

Tunaweza kuona muundo huu huu katika juhudhi zetu za kumtii Mungu. Tunasikia mwito wa injili. Kisha hofu yetu ya asili inaibuka – hofu ya mabadiliko, hofu ya yasiyojulikana – na inatufanya tuache na kuwa na wasiwasi. Roho Mtakatifu anatufundisha ukweli (Yohana 14:26, 16:13), hofu yetu huwa kimya, tunatii, na tunamfuata Kristo. Baada ya wokovu wetu, hatua hii inarudiwa mara nyingi Mungu anapotuomba tuchukue hatua mpya za imani.

Hapa kuna baadhi ya mawazo ya kuwasaidia watoto kukubali muundo huu wa utiifu:

- Waeleze hadithi nzuri za injili katika njia ambayo wataelewa.
- Wafariji watoto wadogo wanapolia
- Wasaidie watoto kujua wakati Roho Mtakatifu anasema nao, wakubali mwito wa Mungu katika maisha yao, na kufanya agano ya kutii na kumfuata Mungu.
- Wasaidie watoto waelewe tamaa ya Mungu ya kuwaokoa na kuwaongoza katika maisha yao yote.

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

## Zawadi Muhimu

Leta kifurushi kizuri darasani. Ndani ya kifurushi weka kadi iliyo na neno ‘UTIIFU’ juu yake.

*Je, unapendelea kutoa au kupokea zawadi? Matendo ya Mitume 20:35 inasema kwamba ni baraka kutoa kuliko kupokea. Tunaenda kusoma juu ya zawadi tunazoweza kumpa Yesu.*

Fungua kifurushi na utafute neno ‘UTIIFU.’

## Utiifu - Mathayo 1:18-25

Zawadi ya Mariamu na Yusufu

“Muda hupita haraka sana,” Mariamu alifikiria. “Kwa miezi michache tu, Yusufu na mimi tutaoana.”

Mariamu alikuwa mwanamke aliyempenda na kumtii Mungu. Mariamu alikuwa rafiki wa seremala mdogo aliyeitwa Yusufu. Siku moja, Mariamu alikuwa ameketi nyumbani wakati ghafla mbele yake mtu alitokea akiwa amevalia mavazi yaliyong'aa. Kwa uoga Mariamu alifikiria, "Huyu aweza kuwa nani? Je, huyu ni Malaika, mjambe wa Mungu?"

Huyu alikuwa hakika Malaika Gabrieli, "Habari Maria. Usiogope. Mungu anakupenda sana na yuko pamoja nawe."

Mariamu aliogopa sana. Macho yake yalikuwa wazi kwa mshangao. Mariamu aliendelea kumkazia macho Malaika Gabrieli aliyekuwa amesimama mbele yake. "Mungu amependezwa na wewe na amenitura nikupatie Habari Njema. Hivi punde jambo maalum litatendeka kwako. Utakuwa na mtoto na utamwita Yesu. Atakuwa Mfalme Mkuu, Mwokozi wa ulimwengu wote!"

Mariamu alijaribu kuelewa kile Malaika alikuwa anasema, "Je, hii inawezekanaje?" Mariamu aliuzima.

"Mariamu," Malaika Gabrieli alisema. "Mtoto atakayezaliwa atakuwa ameumbwa na nguvu za Mungu. Mungu anaweza kufanya mambo ambayo mtu mwingine hawesi kufanya. Utamzaa Mwana wa Mungu." Wakati Malaika alipoondoka Mariamu alimsifu na kumtukuza Mungu kwa moyo wake wote. Mariamu alimtumainia Mungu na kukubali kutii mipango yake kwa uwezo wake wote. Ingawa hakuelewa kila kitu, Mariamu alifurahi kuchaguliwa kuwa mama wa mtoto maalum. Mariamu alienda kumtafuta Yusufu na kumwambia kila kitu kilichotokea na Malaika.

Yusufu hakufurahi kamwe. Ingawa alimpenda rafiki wake wa kike Yusufu aliamua hangemuoa Mariamu. Usiku huo, Yusufu alipokuwa amelala, Malaika wa Bwana alimjia na kusema, "Yusufu, mwana wa Daudi, usiogope kumuo mpenzi wako Mariamu. Huyu mtoto ni wa Roho Mtakatifu. Mariamu atakuwa na Mwana na lazima umwite Yesu. Atakuwa Mwokozi wa ulimwengu."

Wakati Yusufu aliamka, alijua lazima amtii Mungu. Yusufu alienda kwa Mariamu, "Nimemuona Malaika wa Mungu pia. Nitakuoa."

Mariamu au Yusufu hawakuelewa kilichokuwa kinatendeka, lakini wote walimpenda Mungu. Wote Mariamu na Yusufu walitaka kutii kwa kuwa tayari kuwa wazazi wa dunia wa Mwana wa Mungu wa pekee; Yesu. Mariamu na Yusufu wangkuwa sehemu ya mipango ya Mungu ya kuleta Mwokozi wa ulimwengu.

#### **Je, Unatii?**

Andika maneno 'rahisi' na 'ngumu' kwenye sehemu tofauti ya sehemu ya kufundisha.

*Je, sentensi hizi ni rahisi au ngumu kutii? Onyesha jibu lako.*

- Baba anakupatia pesa na kusema. "Nenda ukajinunulie soda." Rahisi kutii? Au ngumu" Onyesha jibu lako.
- Mama anasema, "Osha vyombo." Rahisi au ngumu?
- Mwalimu wako anasema, "Kamilisha kazi yako nyumbani ya kesho."
- Mjomba wako anasema, "Jifunze mistari sita ya Kumbukumbu ya Biblia."
- Bibi yako anasema, "Usile pipi."
- Baba anasema, "Usitazame televisheni kwa nyumba ya rafiki yako."
- Mwalimu wako wa Shule ya Jumapili anasema, "Zungumza na mtu juu ya Yesu wiki hii."

Je, ni kwa nini wakati mwingine inakuwa rahisi kutii na wakati mwingine haikui rahisi?

Mungu anatutaka tuwe watifiu Kwake hata wakati inakuwa vigumu wakati mwingine.

#### **Kukariri**

"Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili ye yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele." (Yohana 3:16)

Juu ya kadi 7, chora kasha 7 za zawadi na uandike sehemu ya mstari wa kumbukumbu wa kitengo hiki kwa kila kadi, kama vile iliyoweka na mistari [/];

*"Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu/ hata akamtoa/ Mwanawe wa pekee/ ili ye yeyote amwaminiye/ asipotee/ bali awe na uzima wa milele." /*

Mbele ya wakati ficha kadi. Waambie watoto watafute kadi na wajaribu kuzipanga kwa utaratibu. Kadi hizi zitakusaidia kwa masomo nne ya kitengo hiki.

#### **Kufunga**

Sema kwaheri kupitia kwa maombi, ukimshukuru Mungu kwa kutufundisha Kumtii.

Kama ishara ya upendo wetu kwa yesu, ni muhimu kumpa utiifu wetu wa kila siku.

Wiki ijayo tutakuwa tunajifunza kuhusu zawadi inginge ambayo tunaweza kumtolea Mungu.


## Zoezi la 48

### ZAWADI YA UTIIFU

**Maandiko:** Mathayo 1:18-25; Luka 1:26-38

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi watake kumtii Mungu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yejote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)



Je, unaweza kumpa Mungu zawadi ya utiifu pia?

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kuelewa ni kwa nini tunahitaji Mwokozi.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yejote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

## Jitayariske Kufundisha

Inaweza kuwa vigumu kuwasaidiwa watoto kuelewa ni kwa nini zawadi ya Yesu kama Mwokozi wetu ni muhimu sana.

Kuokolewa kutoka wa nini?

- Ni lazima tuwe na hisia ya kuhitaji kuokolewa kutoka kwa dhambi zetu (mambo mabaya ambayo tumefanya).
- Ni lazima tujue kwamba tumetenda dhambi na tutamani kutubu. (kubadili moyo wetu kutoka kwa kutenda mabaya)

Somo la leo litatusaidia kuelewa ni kwa nini tunahitaji zawadi ya Mwokozi na ni kwa nini kuzaliwa kwa Yesu kulikuwa maalum. Maandiko yanatukumbusha umuhimu wa tamaduni ya Krismasi ya kupeana zawadi.

- Yohana 3:16 inatuonyesha mfano kamili wa zawadi bora ya Krismasi; kile aaminiye katika Mwana wa Mungu atapoka uzima wa milele.
- 1 Yohana 4:9 inatueleza kuhusu zawadi hii, lakini katika njia ya kibinagsi: *Mungu alionyesha upendo wake kwetu kwa njia hii; Alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni ili tuwe na uzima kwa njia yake.*
- Luka 2:1-7 tunapata zawadi hii maalum ya Mungu: the baby Yesu, Mwokozi wa ulimwengu.

Upendo mkuu wa Mungu ni zawadi bora ya Krismasi ambayo watu wanaweza kupoka. Biblia iko wazi katika kutueleza kwamba ... “Atawaokoa watu kutoka kwa dhambi.” (Mathayo 1:21). Baada ya kupokea zawadi nzuri, tunaweza kuipitisha kwa wengine pia. Ombo kwamba wakati wa msimu wa Krismasi tunaweza kuwafikia wengine na kuwaongoza kwa Kristo; hasa watoto!

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

Soma Luka 2:1-7; Yohana 3:16 na 1 Yohana 4:9.

Wakaribishe wanafunzi, hasa wale wanaotembea kwa mara ya kwanza. Chukua ujumbe wao wa mawasiliana ili uweze kuwasiliana nao. Imba nyimbo za sifa ili kuanza.

Kwa ufupi rejelea yale tumejifunza kuhusu zawadi ya UTIIFU wiki jana. Yeyote tayari anayejua mstari wa kumbukumbu kwa moyo afunque zawadi ya pili na kuisoma kadi iliyopatikana ndani kwa sauti, ‘MWOKOZI’. Leo tutajifunza kuhusu zawadi yetu bora zaidi, muhimu zaid ya wakati wote; zawadi ya Mwokozi. Hatia! (Fungia Lebo)

Chagua mtoto wa kujitoea awe na “hatia” ya kuwafanya wengine pia wawe na hatia anapowaguza. Yule mtoto anayeguzwa abaki ‘BARIDI’ hadi mwengine ‘asiyekuwa na hatia’ amguse kwa upole na kumweka huru. Wakati kila mmoja ni ‘MBARIDI’ mchezo utakuwa umekwisha na waanze tena kwa kuchagua mtoto mwengine mwenye “hatia”.

*Je, kwa nini hukuweza kusonga baada ya yule aliye na “hatia” kukugusa? (Kwa sababu nilikuwa mbaridi katika hatia yangu.)*

*Je, ulihitaji kufanya ni nini ili kuwendelea na mchezo? (mtoto ‘asiye na hatia’ aniguse.)*

Katika maisha halisi, sote tunafanywa kuwa na hatia kwa dhambi na hatuwezi kujifanya ‘kukosa kuwa na hatia’ tena. Mungu alifanya mpango kwetu kusamehewa dhambi zetu, hatia yetu ikaondolewa. Mpango huu unahusisha zawadi yetu bora zaidi, muhimu ya wakato wote; zawadi ya Mwokozi. Tumia Ukura 49A wa Zoezi kusaidia kufikira juu ya hadithi ya leo.

Weka vifaa vya watoto kwenye meza ili watoto wavione na kuviguza. Let mdoli kwa watoto kufikiria juu ya Mtoto Yesu.

*Je, ni kwa nini tunatumia vifaa hivi?* –watoto wanaozaliwa wanahitaji ulinzi maalum. Na je, kama Mariamu hakuwa na maji masafi ya kumuosha mtoto? Bila shaka hori ilikuwa na kelele na uvundo! Hii ilikusa sehemu ambayo Mwokozi watu alizaliwa; mahali pa unyenyekevu sana. Wavalishe watoto ili waigize sehemu za Mariamu, Yusufu, na wachungaji kondoo.

Leo tutasikia hadithi kuhusu mtoto maalum sana.

#### Zawadi Nzuri ya Mungu

Mjumbe wa Milki ya Kirumi, Kaisari Augusto, aliwasili akiwa juu ya farasi wake kwenye mji wa Nazareti, akachukua ngozi kutoka kwenye begi lake, na kuanza kusoma kwa sauti ili wote wasikie:

“Kaisari Augusto, mfalme mkuu, atachukua sensa. Anataka kuwahesabu watu wote katika ufalme wake. Kwa sababu hii, kila mtu lazima arudi kule alizaliwa!”

Mjumbe alifunga ngozi na kwenda katika mji mwininge kutoa matangazo hayo hayo. Ilikuwa karibu miezi 9 tangu malaika alimjia Maria na Yusufu. Mtoto alikuwa anaenda kuzaliwa hivi karibuni. “Ni lazima twenda Bethlehemu,” Yusufu alisema, “kwa vile familia yangu yote inatoka huko.”

“Familia yangu pia inatoka Bethlehemu,” Mariamu alisema.

Wote walipanga mizigo you kwa ajili ya safari. Wangehitaji chakula, maji, na blanketi za kulala. Mariamu pia alitayarisha mavazi ambayo alikuwa amemtengenezea mtoto. Ilikuwa safari ndefu ya kwenda Bethlehemu.

Baada ya siku kadhaa ya kusafiri hatimaye walifika Bethlehemu usiku. Yusufu alikimbia kutafuta mahali pa kulala. Marimau alikuwa amechoka sana kutoka kwa safari ndefu; hivi karibuni mtoto atazaliwa. Lakini nyumba ZOTE za wageni zilikuwa zimejaa na wageni wengine amba pia walikuwa wamerudi nyumbani kwo kujandikisha kwa ajili ya sensa.

Jozlilokuwa limechoka waliwasili sehemu ya mwisho ya mji. Ingawa kulikuwa kumejaa, mtunza nyumba ya wageni aliwaruhusu wala katika hori. Hapa si mahali ambapo Mariamu alitarajia mwanawawe atazaliwa. Familia ya Mariamu ilikuwa mbali sana na hawakuwa na marafiki wowote karibu nao. Hawakuwa hata na kitanda cha kulala.

Bado usiku huo, katika hori la ng’ombe huko Bethlehemu, Mtoto Yesu, Mwokozi wa ulimwengu! alizaliwa! Mariamu alimchukua mtoto katika mikono yake. Alimwosha, akamfunga ndani ya blanketi aliyokuwa amenunua na kumweka katika hori iliyopita nyazi safi ili alale. Usiku huo Mungu aliwapa wanadamu zawadi nzuri zaidi ya Krismasi: Yesu, Mwana wa Mungu – Mwokozi wetu.

Waulize watoto wainamishe vichwa vyao na kurudia maombi baada yako. Simama kila wakati ukiona alama hii: (/)

*Mungu Mpendwa, / asante kwa kutupenda. / Asante kwa kutuumba / mpango mzuri kwetu / na kwa kumtuma Yesu duniani. / Tunakusifu / na kukuabudu Mungu / kwa ajili ya zawadi hii nzuri / ambayo ultipatia / kupitia Mwanao Yesu, / Mwokozi wetu. / Amina.*

Kama utapenda, unaweza kufanya mwaliko zaidi wa kibinafsi kwa kila mwanafunzi ayatoe maisha yake kwa Kristo. Kama watoto watamkulali Yesu, tumia muda mchache baada ya darasa uombe nao kila mmoja.

#### **Kukariri**

“Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawewe wa pekee, ili ye yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

Tumia kadi ambazo ultengeneza wiki iliyopita iliyo na mstari wa Biblia. Ziweke ili watoto waweze kusoma mstari mara kadhaa. Ondoa kazi moja baada ya ingine, hadi kazi zote ziwe zimeisha na watoto wanawenza kusema Yohana 3:16 kwa kukariri. *Je ni nani anayeweza kussema mstari kwa kukariri?*

#### **Kufunga**

Waangazie wale walioomba ili kumkulali Yesu na uwaeleze umuhimu wa hatua hii ya imani. Tengeneza mahali pa kuwafanya uwanafunzi. Watie moyo watoto kuendelea kuhudhuria darasa zaidi ili kujifunza juu ya zawadi tunayomtolea Mungu. Shiriki mahitaji ya maombi na muombeane.



## **Zoezi la 49**

### **ZAWADI YA MWOKOZI**

**Maandiko:** Luka 2:1-7; Yohana 3:16; 1 Yohana 4:9

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kuelewa ni kwa nini tunahitaji Mwokozi.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yejote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)



#### **YESU MWOKOZI WETU**

Yesu alikuja duniani kama mtoto. Yesu alikua. Aliwasaidia watu kujua upendo wa Mungu. Kisha Yesu alikufa msalabani. Alifanya haya yote ili tusamehewa kwa mambo mabaya tuliyotenda. Hivi ndivyo Yesu anaweza kuwa Mwokozi wetu.

K – Kubali kwamba umetenda dhambi (umefanya maovu, umemuasi). Mwambie Mungu yale umetenda, sikitika kwa sababu ya mabaya umetenda, na uwe tayari kuacha. (Warumi 3:23 na 1 Yohana 1:9)

A – Amini kwamba Mungu anakupenda na alimtuma mwanawe Yesu akuokoe kutoka kwa dhambi zako. Ombo na upokee msamaha Mungu anakupatia. (Yohana 3:16 and Matendo ya Mitume 16:31)

M – Mkiri Yesu kama Mwokozi wako. Waeleze wengine yale Mungu amekutendea. Mpende Mungu na umfuate Yesu. (Yohana 1:12 na Warumi 10:13).

## Lengo la Somo

Wasaidie wanafunzi kutambua umuhimu wa kushikiri Habari Njema na watu wengine.

## Mstari wa Kumbukumbu

“Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yeoyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.”  
(Yohana 3:16)

## Jitayariske Kufundisha

Somo hili litawasaidiwa watoto kujifunza furaha ambayo wachungaji walihisi wakati walikutana na Yesu na jinsi walieleza Habari Hii pya kwa watu wengine.

Wachungaji hawakuwa na mengi ya kumpa Mtoto Yesu; pengine wanafunzi walihisi vivyo hivyo. Wasaidie waelewe kwamba wanaweza kumpa Yesu kile wachungaji walimpa katika hori la ng’ombe; sifa na tamaa yao ya kuwaeleza wengine Habari Njema ya Mwana wa Mungu.

Kuzaliwa kwa Mtoto Yesu; Masihi, yule aliyetumwa kuleta Habari Njema kwa maskini (Luka 4:18), alibadilisha wanadamu kabisa. Dunia haingekuwa vile vile tena.

Wachungaji wanyenyekemu walikuwa wa kwanza kujuu kwamba Mungu alikuwa ametimiza ahadi

yake na kwamba Masihi wao alikuwa sasa duniani kutimiza misheni yake. Kupitia hii, Mungu aliweka fikira kwamba Yesu alikuja kwa ajili ya kila mtu kutoka tajiri na mtu mwenye nguvu zaidi hadi maskini na mdhaifu.

Kwa haraka baada ya malaika waliwaeleza kuhusu kuzaliwa kwa Yesu **walikimbia** Bethlehemu kujiona wenyewe. Kisha, **walikimbia** kuwaeleza kila mtu kile walichoona! Furaha ya wachungaji na kufurahia kwoo juu ya kuwaeleza wengine ni mfano kwetu.

Tunapaswa tumpe Mungu SIFA zetu zote kwa sababu Yesu, Mwanawe, alikuja kuishi nasi, alikuja kutufia, na akarudi mbinguni katuandalia mahali! Hiyo ni zawadi bora zaidi tunaweza kuwapa wale wasiojua Habari Njema ya Yesu Kristo! Elezea kila mtu!!!

Imba nyimba za SIFA!

## Kuwasilisha Hadithi ya Biblia

## Zawadi Muhimu

Fungua kasha la zawadi ya tatu na utafute neno SIFA ndani yake. Zungumza juu ya zawadi mbili mlizojifunza hapo awali (UTIFU na MWOKOZI.) Leo tutajifunza kuhusu zawadi maalum ambayo kikundi cha wachungaji kilimpa Yesu: SIFA!

Mchungaji

Mbeleni, waalike vijana wavalie kama wachungaji wa wakati wa Biblia. Zungumza juu ya majukumu tofauti ambayo wachungaji walitekeleza; kuwalinda kondoo, kuwatetea kondoo kutoka kwa wanyuma wa mbuga, kutafutia mifugo chakula, kuwahesabu usiku. n.k.

\*Zadi – mvulana mchungaji mwenye nguvu.

\*Miriam – dadake Zadi. Miriam afurahia kuwa nje na wachungaji kuliko kukaa nyumbani akifanya kazi za nyumba!

## Zawadi ya Wachungaji

Zadi: Miriam, Miriam njoo haraka! Miriam, Ninalo jambo la kukueleza; jambo nzuri lilitotokea!

Miriam: Je, unazungumzia nini? Nieleza!

Zadi: *Jana usiku tulipokuwa tunazungumza tukiwalinda wanakondoo uwanjani, jambo lilitendeka la ajabu.*

Miriam: Eti nini? Nieleze!

Zadi: *Malaika!*

Miriam: Malaika? Zadi, je, uko na mauvivu? (Anagusa kichwa chake) Wewe mgonjwa?

Zadi: *Hapana, hapana, hapana, Miriam! Nakueleza ukweli. Katikati ya usiku malaika walionekana angani, wakivaa mavazi mazuri. Tuliogopa sana!*

Miriam: Hata nami ningeogopa pia.

Zadi: *Kicha akaja mmoja kwetu na kutuambia, "Msiogope. Ninawaletea habari njema ambayo italeta furaha kuu kwa watoto wote. Leo katika mji wa Daudi, Mwokozi amezaliwa; Yeye ni Kristo, Bwana. Hii itakuwa ishara kwenu: Mtampata mtoto amefungwa katika mavazi na amelala katika hori la ng'ombe."*

Miriam: Eti nini? Mtoto? Sielewi. Nieleze mengi; jambo la kufurahisha!... jambo la kutisha!

Zadi: *Kisha zaidi ya malaika walikuja. Walijaza anga wakimsifu Mungu wakisema, "Utukufu kwa Mungu katika mbingu ya juu, na amani duniano kwa wale wa ambao kibali chake kinawashukia."*

Miriam: Je, hii inamaanisha nini?

## Zoezi

### Shiriki Habari Njema

Andika njia zingine za kuwaeleza watu kuhusu Yesu; pengine mwaliike rafiki kwa ibada ya Krismasi, tembelea hospitali ili kueleza hadithi ya kuzaliwa kwa Yesu kwa watoto walio wagonjwa, tengeneza kadi za kuwapa watu wasiomjua Yesu, n.k.

### Nyimbo za Krismasi

Tengeneza vyombo vyta Krismasi ukitumia vifuniko vya chupa za soda za plastiki. Weka mbegu au mawe ndani ya chupa. Funga vifuniko kwa nguvu. Vyombo vyako vya kucheza viko tayari!

Njia ya kumsifu Mungu kuitia nyimba; kama tu vile malaika walivyofanya usiku wakati Yesu alizaliwa.

## Kukariri

"Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili ye yote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele." (Yohana 3:16)

Kabla ya darasa, ficha kadi ulizotumia katika somo lililopita. Wasaidie watoto kutafuata kadi hizo na kuzipanga kwa utaratibu. Rudia mstari ukiusema kwa sauti.

## Kufunga

Unda mviringo wa maombi na muombee mahitaji ya kila mmoja. Chukua nafasi ya msimu wa Krismasi wa kufuata mfano wa wachungaji. Waeleze wengine hadithi ya kuzaliwa kwa Yesu na mpango mkamilifu wa Mungu wa kuwaokoa wanadamu kutoka kwa dhambi zao. Imba nyimba za sifa. Waalike watoto kwa darasa litakalofuata la kutambua zawadi yetu ya mwisho.

## **Zoezi la 50**

### **ZAWADI YA SIFA**

**Maandiko:** Luka 2:8-20

**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kutambua umuhimu wa kushikiri Habari Njema na watu wengine.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yeoyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

Wachungaji walikuwa wakilinda kondoo wao usiku mmoja. Mara tu anga ilijaa nuru. Malaika alitokea. Wachungaji waliogopa. “Msiogope,” malaika alisema: “Ninawaletea habari njema za watu wote: Leo Mwokozi amezaliwa, yeye ni Kristo Bwana! Mtampata mtoto amevikwa nguo za kitoto na amelazwa horini.” Mara tu, malaika walijaza anga. Walikuwa wakiimba, “Utukufu kwa Mungu juu mbinguni. Amani na iwe duniani!” Kisha malaika wakaondoka. Wachungaji walisema, “Twendeni tukamuone mtoto.” Walienda Bethlehemu na wakapata horini ambapo Yesu alikuwa na Mariamu na Yusufu. Yesu alikuwa amelazwa horini. Wachungaji walimsifu Mungu na wakaeleza habari njema za kuzaliwa kwa Yesu kwa wale waliokutana nao. Na kila mtu aliyesikia hadithi yao alishangaa.

“Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yeoyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

**Lengo la Somo**

Wasaidie wanafunzi kutaka kujua na kutafuta njia za kumwabudu Yesu.

**Mstari wa Kumbukumbu**

“Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulmwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

**Jitayarisha Kufundisha**

Watoto wanaweza kujifunza KUMWABUDU Mungu! Ibada haimaanishi kuimba peke yake na macho yetu yakiwa yamefungwa na mikono yetu ikiwa imeinuliwa. Ibada ni nia ya moyo inayotokana na upendo tunaohisi kwa ajili ya Mungu.

Mamajui kutoka Mashariki walisafiri maili nyingi ili kwenda kutoa sio zawadi za mali bali pia kujitoa

kwa kwa Mtoto Yesu; Hii ilikuwa ibada! Mungu anapendezwa tunapoijinyenyekea mbele Yake. Mungu anatutaka tumpe Yesu zawadi zetu bora wakati wa Krismasi hii, zawadi ya KUMWABUDU.

**Kuwasilisha Hadithi ya Biblia****Zawadi Muhimu**

Rejelea zawadi zile zingine tatu; Utiifu, Wokovu, na Sifa.

Fungua kasha la nne ili kutambua kadi ambayo inaeleza zawadi ingine tunayoweza kumpa Yesu; “KUABUDU.”

Hili ni somo la mwisho la kitengo hiki na la mwaka.

Tayarisha sherehe ndogo ya Krismasi ya:

- Kusherekea Mtoto wa Bethlehemu, Yesu.
- Kuwashukuru watoto kwa mahudhurio na kuhusika kwao katika mwaka wote.

Watie watoto moyo waendelee kukumbuka na kukariri mistari ya Biblia. Rudia vifungi hivi kwa wazazi wao, babu na bibi na mafariki.

**Zawadi Tatu za Wafalme**

Kwa urembo funga kadi 3 zinazosema ‘dhahabu,’ ‘ubani,’ na ‘manemane na kuzificha darasani. Tafuta zawadi hizi ambazo mamajusi walimletea Yesu akiwa mtoto. Unapozifungua kazi eleza maana ya kila zawadi ambazo mamajusi walileta:

- dhahabu: ishara ya ukuu duniani
- Marashi: (ubani) ishara ya Mungu
- manemane: mafuta ya kuhifadhi mwili wa mfu (ikitabiria kusulubiwa kwa Yesu)

**Zawadi ya Kuabudu**

- andaa vifaa vya kuona ili kueleza somo hili.

Zamani kulikuwa na mamajusi waliozisoma nyota. Usiku mmoja waliona nyota kubwa iliyong’aa, “Nyota hii inamaanisha kwamba mtoto maalum amezaliwa,” mmoja wa mamajusi alisema. “Mtoto huyu atakuwa mfalme wa Wayahudi; twendeni tukamtafute na TUMWABUDU!” Mamajusi

walipanda juu ya ngamia zao na wakaenda safari ndefu.

Mamajusi walipofika Yerusalem, walienda kusema na Mfalme Herode; mkuu wa Yerusalem, "Je, yuko wapi mfalme wa Wayahudi aliyezaliwa? Tumeona nyota yake na tumekuja KUMWABUDU." Mfalme Herode alikuwa na wasiwasi aliposikia haya na akawauliza makuhani wake wakuu, "Je, yuko wapi mfalme mpya?"

"Atazaliwa Bethlehemu ya Yudea, mji wa Daudi," walijibu.

Mamajusi walichukua ngamia zao na kuelekea Bethlehemu. Nyota hiyo hiyo iliyong'aa ambayo walikuwa wameona iliwaongoza usiku. Baada ya muda nyota ilisimama juu ya hori ambapo Mtoto Yesu alikuwa. Mamajusi walifurahi sana! Walipomwona Yesu pamoja na Mariamu, walipiga magoti na KUMWABUDU. "Huyu ndiye Mfalme mpya," walisema kwa furaha. Mamajusi walimpa Yesu zawadi tatu maalum: dhahabu, marashi na manemane.

Punde mamajusi walirudi nyumbani kwao; walikuwa na furaha sana kwa sababu walikuwa wamekutana na Yesu, Mwokozi wa ulimwengu! Walifurahi kwamba waliweza kuleta zawadi zao za KUABUDU kwa Mtoto Yesu, Mfalme wa wafalme.

Mamajusi hawa wanatupa mfano wa IBADA ya kweli mbele ya Mwokozi wa ulimwengu. Na tuwe "Waabudu wa kweli" wa Kristo Yesu.

## Zoezi

### Nyota Iliyojificha

Kata tunda la tufaha mara mbili, upande kwa upande. Waonyeshe watoto nyota inayojiunda katikakati wakati unakata tufaha mara mbili. Watu wengine hufikiria kwamba nyota hii ni ukumbusho wa ile iliyowaongoza mamajusi mahali Yesu alikuwa. Tunafurahia Mungu alituma nyota hiyo maalum. Ni ishara ya kwamba Yesu si Mfalme wa Wayahudi tu, bali Mfalme wetu pia.

## Kukariri

1. Panga kuhusika maalum kwa wanafunzi walijifunza mistari ya kukariri; pengine uwape zawadi ndogo za kuwatia moyo kuendelea kusoma na kujifunza Neno la Mungu.

2. Mwulize mchungaji akupe nafasi ya kuwasilisha darasa lako na watoto waliojifunza mistari yote wanapoisema mistari imbele ya umati. Peana hati za kutambuliwa kwa watoto.

## Kufunga

Mshukuru Mungu kwa mwaka huu wa masomo, na kwa zawadi nzuri ya wokovu ambayo ametupatia kupitia Yesu. Watie moyo watoto kumtumainia Yesu kama Mwokozi wao binafsi.

Je, tutampa Yesu zawadi gani wakati huu wa Krismisi?

Waeleze watoto zawadi zako maalum zitakuwa gani kwa Yesu:

- Muda: kufundisha darasa, muda wa kuandaa, mahudhurio katika ibada, n.k.
- Maombi ya binafsi na ya wazi
- Matoleo: pesa, talanta
- Ibada: nyimbo za sifa, kuwaeleza wengien kuhusu Yesu

Ombea kila mmoja wa watoto hawa. Wakumbushe umuhimu wa kumtafuta Mungu kila wakati.

Kuwa na sherehe ya kuinua ambayo watoto wakubwa wanasonga katika darasa lingine.

## Zoezi la 51

### **ZAWADI YA KUABUDU**

**Maandiko:** Mathayo 2:1-12


**Lengo la Somo:** Wasaidie wanafunzi kutaka kujua na kutafuta njia za kumwabudu Yesu.

**Mstari wa Kumbukumbu:** “Maana kwa ajili hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili yejote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)

**Mwokozi ni neno muhimu. Mwokozi huwaweka  
watu huru kutoka kwa kitu kibaya. Yesu ni  
Mwokozi. Alikuja duniani kutuonyesha upendo  
wa Mungu. Alikufa kutuweka huru kutoka kwa  
dhambi zetu.**

**Sifa ni neno lingine muhimu. Kusifu ni  
kumwambia na kumuonyesha Mungu kwamba  
tunampenda zaidi mtu mwingine yejote na zaidi  
ya kitu kingine chochote.**

**Je, mamajusi wa Mashariki Walimsifu Yesu,  
Mwokozi?**





ISBN: 978-0-7977-1499-1  
P O Box 1288  
Florida 1710  
Republic of South Africa

